ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na

		Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 1 Juni, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha Baraza cha tarehe 22 Mei, 2017 Mhe. Suleiman Sarhan Said aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe sasa namuomba Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mhe. Mjumbe huyo, Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Samaki ambao wapo hatarini kutoweka kwa upande wa Zanzibar ni wale wale ambao duniani kote wako hatarini kutoweka nao ni kama wafuatao:-

1. Nguva
2. Papa
3. Kasa
4. Kisukuku

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 104

Utaratibu wa Kuwatumia Walimu wa Kujitolea

Mhe. Shaib Said Ali (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid): - Aliuliza**:**

Katika nchi mbali mbali, wanafunzi wanaomaliza masomo yao ya elimu ya juu wana utamaduni wa kujitolea kufundisha. Kwa kuwa katika skuli zetu hasa za sekondari zinakabiliwa na upungufu wa walimu hasa wa masomo ya sayansi. Na kwa sababu Serikali hutoa pesa nyingi kuwakopesha wanafunzi ambao ni vijana wetu ambapo kwa mzunguko wa kila muda kuna wanafunzi wanaomaliza masomo yao ambao kama wangeweza kujitolea wangepunguza tatizo la upungufu huo iwapo Serikali italisimamia ipasavyo na kisheria na kuleta faida kubwa kwa Serikali.

(a) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuweka sheria na masharti kwamba mtu yeyote anaeomba mkopo wa Elimu ya Juu ambae si muajiriwa wa Serikali baada ya kumaliza masomo yake akajitolea kufundisha kwenye skuli zetu kwa muda maalum.

(b) Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepokea walimu wangapi wa kujitolea kutoka nchi za nje kwa mwaka 2016 ambao wanafundisha katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 104 kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba skuli zetu zina uhaba wa walimu hasa wa sayansi. Pia Serikali inatumia pesa nyingi kulipia wanafunzi wanaosoma elimu ya juu. Katika miaka ya nyuma Serikali iliweka utaratibu wa kujitolea kwa vijana wanaomaliza masomo na kuajiriwa. Utaratibu huo baadae uliondolewa. Wizara inalipokea wazo la Mhe. Mwakilishi la kuanzisha utaratibu wa kujitolea, kuitumikia Serikali kwa vijana wanaopewa mkopo wa kusoma katika taasisi za elimu ya juu. Wizara yangu itafanya upembuzi yakinifu ili iweze kujua jinsi ya kuliendesha zoezi hilo.

(b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inapokea walimu wa kujitolea kutoka katika mataifa mbali mbali. Kwa mwaka wa 2016/17, kulikuwa na jumla ya walimu 36 wa kujitolea kutoka nchi za Cuba, Japan, Ujerumani, Korea na Nigeria. Ahsante

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja na nyongeza kama lifuatavyo.

Je, ni lini wataajiri vijana hawa wa elimu ya sayansi ili kupunguza tatizo hili kabla kuchukua watu hawa kutoka nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Tumesema kwamba utaratibu wa ajira uko wazi kwamba nafasi inapopatikana katika Wizara ya Elimu, tunaomba kibali na tukiruhusiwa tunaajiri. Sasa ni kweli kuna uhaba wa walimu wa sayansi na tumeshaomba kibali na tukipata kibali tutaajiri walimu wakati wowote.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuuliza swala moja na nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatiya lakini pili nimuulize swala dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, wakati akijibu swali lako alisema kwamba Wizara ilikuwa na mpango ya kuwaweka vijana kwa ajili ya kujitolea, lakini baada ya kuona kwamba kutakuwa na usumbufu vijana wale waliondolewa na ikabidi hamna namna ya kujitolea.

Mheshimiwa umesema kwamba umepokea vijana kutoka nje ambao wanakuja kujitolea kwa ajili ya kuisaidia Wizara. Je, kuwepo kwa vijana hawa kutoka nje hatuoni kwamba tunawanyima fursa wale ambao ni wazalendo wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba Serikali huwa inaagiza au inaomba ufadhili wa kusomesha kutoka nchi mbali mbali na katika nchi hizo kuna utaratibu wa raia zake kujitolea, wale wanaojitolea wakati mwengine tukiwaomba huletwa katika nchi zetu kutusaidia.

Lakini pia huwa tunawaomba katika maeneo mahsusi ambayo tuna upungufu wa vijana wetu, kwa mfano hawa ambao waliopo sasa, hawa tumewaomba kwa ajili ya kusomesha masomo ya sayansi ambao kila mmoja anajua kama Zanzibar kuna upungufu na hivi karibuni tutapata vijana wengine wa kujitolea kutoka Nigeria kwa ajili ya masomo mawili ambayo tuna upungufu mkubwa zaidi wa *mathematics* pamoja na *physics*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri huoni wakati sasa hivi umeshafika kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi na kuwapa motisha ili kupunguza tatizo hili na kama anavyosema sadaka huanza nyumbani kwanza au taa huwasha ndani ya nyumba kabla ya kuwasha nje.

b) Masomo hayo huwezi kusoma skuli popote ila kuwepo na vyoo, mvua za juzi zimeathiri sana Skuli ya Bwejuu na vyoo havipo na skuli yenyewe kufungwa. Je, lini utakwenda Bwejuu mimi na wewe kwenda kuangalia hali hiyo ili wapate kusoma masomo ya sayansi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Jaku maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Kwamba Wizara sasa hivi imeshaanza utaratibu wa kutoa motisha kwa vijana wanaofanya vizuri wa sayansi katika masomo ya kidato cha sita, tunawapatia ufadhili tumeanza na tutaendelea kuwapatia kila aina ya motisha hapo baadae hatua kwa hatua.

(b) Niko tayari wakati wowote kufuatana naye kwenda Bwejuu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuongezea majibu kidogo tu hili la vyoo vya Bwejuu Ofisi ya Halmshauri kwa kupitia fedha za Mfuko wa Mbunge wa Jimbo la Paje, tayari vyoo hivyo vinajengwa vya Skuli ya Bwejuu.

Taarifa

Mhe. Jaku Hasim Ayoub: taarifa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku kuhusu taarifa, nakuomba ukae.

Nam. 147

Mapato Yatokanayo na Mradi wa Menai

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza**:**

Watalii wengi hivi sasa wanatembelea fukwe za Kisiwa cha Kwale kilichopo chini ya Mpango wa MENAI na kukusanya mapato kutoka kwa watalii wanaoingia maeneo hayo.

(a) Je, mpango huu wa uhifadhi wa MENAI ulianza lini na utaishia lini.

(b) Je, ni kiasi gani cha mapato kwa upande wa MENAI (Fumba-Bweleo-Dimani) kilipatikana kwa miaka 3 iliyopita kuanzia mwaka (2014, 2015 na 2016).

(c) Je, katika mapato hayo, kiasi gani kilisaidia maendeleo ya vijiji vya Fumba, Bweleo, Dimani na Nyamanzi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini, kwanza naomba nimpe maelezo mafupi kabla ya kujibu swali lake (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kutokana na amani na utulivu uliopo hapa nchini, watalii huwa wanatembelea katika fukwe za visiwa mbali mbali ikiwa pamoja na Kisiwa cha Kwale kilichopo chini ya mpango wa hifadhi ya Ghuba ya Menai. Aidha, ni kweli watalii hao huwa wanalipa ada ya Dola 3 za Kimarekani kwa ajili ya kusaidia gharama za uendeshaji kwa jamii ndani ya maeneo ya hifadhi katika vituo vitatu muhimu (Fumba, Unguja Ukuu na Kizimkazi) na kutatua baadhi ya kero zao nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya Maeneo ya Hifadhi kifungu Nam. 19(1) na 19(3) asilimia 70 za makusanyo yanayopatikana zinatakiwa kutatua matatizo ya uendeshaji kwa Kamati za Jamii katika vijiji 27 vilivyopo katika hifadhi ya Ghuba ya Menai. Asilimia 30 inaipa uwezo Kamati Tendaji inawahusisha wenyeviti tu wote katika vijiji 27 kufanya maamuzi ya masuala ya kijamii watakayoamua kutekelezwa nje ya kazi za uvuvi mfano uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa skuli nakadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi inafanya kazi ya kuratibu na kusimamia Kanuni zifuatwe kwa kuhakikisha kwamba mpango huo waliojiekea wananchi wenyewe unatekelezwa bila ya kasoro, kutokufahamiana, kuhitilafiana na hatimae kugombana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 147 kama ifuatavyo:-

(a) Mpango huu wa uhifadhi wa Ghuba ya Menai ulianza rasmi mnamo mwaka 1997 na kufuatia marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya 2010, ilianzisha Kanuni mpya ya Maeneo ya Hifadhi L.N 81 ya mwaka 2014 inayoyaweka maeneo yote ya hifadhi ya hivi sasa katika Kanuni moja na yatakayotokea baadae kuwa endelevu na hivyo yataendelea daima.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Mapato yaliyokusanywa katika Kituo cha Fumba kwa wageni wote wapitao kituo cha Fumba kwa kipindi cha miaka mitatu (2014, 2015, 2016, na 2017) ni jumla ya T.shs 93,276,220/= (kiambatanisho A ambacho Mwakilishi nimempatia inaelezea kwa undani).

(c) Mhe. Mwenyekiti, katika mapato yaliokusanywa Hifadhi ya Ghuba ya Menai, vijiji vya Fumba, Bweleo, Dimani na Nyamanzi vilitumia mapato ya Menai kama inavyojionesha katika kiambatanisho B. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri swali langu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba katika lile jawabu ambalo tumepatiwa Mjumbe Mwakilishi alipitie, kwa masikitiko kiambatanisho A na B kama alivyovitaja Mhe. Waziri sikupatiwa. Kwa hivyo siwezi kuona ile *trend* ya makusanyo kama suala langu la msingi linavyosema.

Nilitaka kujua 2014 kiasi gani, 2015 kiasi gani, 2016 kiasi gani na hii kwa sababu hasa watalii wamekuwa wanaongezeka na mapato yanaongezeka. Sasa hii Mhe. Waziri namshukuru katoa *block sum* ya shilingi 93,000,000 *anyway,* nafikiri hayo tunaweza tukazungumza baadae.

Lakini sasa swali langu Mhe. Mwenyekiti, la msingi ni kama ifuatavyo:-

a) Maji ndio uhai wetu na sekta ya maji kwa kweli tunaisaidia kwa pembe zote mbili. Na hivi sasa Jimbo la Dimani na Vijiji alivyovitaja Mhe. Waziri vyote kuna matatizo makubwa ya maji kwa sababu ya *pumps* zile ku-*breakdown* mara kwa mara. Tunashukuru wameweza kukusanya Shs.93,000,000 na mwenyewe kasema kwamba madhumuni makubwa ya makusanyo haya ni kusaidia asilimia 30 uendeshaji pamoja na kutatua matatizo madogo madogo na asilimia 70 kwa uendeshaji mwengine.

b) Sasa namuomba kumuuliza Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vyema kukaa pamoja na Kamati za Maendeleo za Vijiji hivi hasa suala la

msingi zile *pumps* zina-*breakdown* mara kwa mara na Wizara ya Maji tunashirikiana nayo, lakini katika kutatua hayo matatizo, hizi pesa zikatumika vilivyo kusaidia vijiji hivi kutanzua tatizo la maji kwa kununua *pump, rather than* kukaa na wale wenyeviti wakawapatia *allowance* tu chai katika mikutano yao waliosema kama kuwaridhisha wanyamaze, lakini pesa nyingi kwa kweli zinakusanywa zaidi ya hapa.....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ulize swali

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Ahsante

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza.

a) Kwanza ni kweli nilitegemeza kwamba kile kiambatanisho umepata lakini nitazisoma hizo takwimu.

Mwaka 2014/2015 jumla ya pesa zilizokusanywa ni 31,621,300	
Mwaka 2015/2016 ni jumla milioni	35,823,120
Mwaka 2016/2017 ni milioni	25,861,800
Ndio jumla milioni	**93,276,220**

b) Kuhusu suala lake la maji Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu yapo kweli matatizo ya maji katika maeneo mengi sana Unguja na Pemba na nakushukuru sana hizi kamati kwamba zinasaidia pale ambapo kuna matatizo. Lakini nataka nikubaliane na Mheshimiwa wakati mwengine kwenye vijiji kuna mgongano sana katika suala la kusema wapi matatizo haya yatatuliwe kwa kutumia fedha hizi na ndio maana Wizara yetu inakubali kuwa *co-ordinator,* yale maamuzi yatakayotolewa katika kamati zenu, sisi tuko tayari kuyasimamia ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa.

Lakini kama unafikiri Mheshimiwa kuna matatizo, sisi tuko tayari kuja Wizarani ukae na sisi utueleze ili tuone ni vijiji gani na gani vina matatizo ili tukakae pamoja na kamati na wewe mwenyewe ukishiriki ili tuweze kutatua tatizo hili maji ambalo tunaweza kulitatua.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na vielelezo vyingi na pesa nyingi alizozitaja katika vijiji vyetu. Lakini nataka kumpa mfano *conservation area* za Pangani wamejenga Maabara na Skuli nyingi zinazoonekana wazi wazi kwa faida ya wananchi.

Je, anaweza akaliambia Baraza hili ni kitu gani kilichosaidiwa kutokana na Huba ya Menai katika vijiji vyote alivyovitaja, ni kitu gani cha wazi ambacho kinaonenaka kama kule Pangani walipojenga skuli na maabara yake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa swali lake Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri ningefanya vizuri kama ningewaletea miradi yote ambayo imefanyiwa na Menai badala ya kutaja kitu kidogo kidogo, na mimi namuahidi bora nimletee orodha nzima ili aone ni kiasi gani fedha hizi za msaada za jamii zimetumika ili kila mmoja aone hasa ni kiasi gani kimetumika na kama kuna haja kurekebisha tuweze kukaa pamoja kurekebisha, badala ya kusema mambo mafupi mafupi kama hivyo.

Nam. 13

Wachezaji wa Mpira wa Miguu wa Zanzibar Wanaocheza Nje ya Nchi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Nchi mbali mbali zimeendelea katika mchezo wa mpira wa miguu pamoja na sababu nyengine kutokana na kuwa na wachezaji wengi wanaocheza mchezo huo nje ya nchi zao.

(b) Je, ni wachezaji wangapi wa Zanzibar wanaocheza mpira wa miguu nje ya nchi.

(c) Zanzibar inafaidika vipi kwa kuwepo wachezaji nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Mchezo - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa nchi mbali mbali zimeendelea katika mchezo wa mpira wa miguu pamoja na sababu nyengine, lakini pia kuwa na wachezaji wengi wanaocheza nje ya nchi wanasaidia nchi zao kufanya vizuri.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wachezaji wengi kutoka Zanzibar wanacheza mpira wa miguu nje ya nchi lakini wanaotambulika rasmi ni wachezaji 21.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa wachezaji hao nje ya nchi kunaifanya Zanzibar kutambulika na kuonekana kupitia ramani ya michezo na hivyo kuchangia ujaji wa watalii na kadhalika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri amezungumza ana jumla ya wachezaji 21 wanaotambulika rasmi wanaocheza mpira nje ya nchi.

a) Je, atakuwa tayari kunitajia.

b) Leseni za wachezaji hao wanaoruhusiwa kucheza nje ya nchi zinatoka wapi, zinatoka *TFF* au zinatoka *FAT.*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Mchezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hawa ni wachezaji ambao wako nje na ametaka nimtajie, naomba sana nitamletea kwa maandishi na nitafuatilia kwa kina nimletee kwa maandishi.
b) Leseni za wachezaji hawa zinatoka katika nchi yetu hii hii ya Tanzania kwani kuna taratibu za wachezaji wetu ya kuwa na leseni na vibali kutoka katika nchi zetu na kuingia nchi nyengine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Naibu Waziri lakini katika majibu yake amesema kwamba kuwepo kwa wachezaji hao nje ya nchi ambao kunaifanya kuitangaza Zanzibar na kutambulika Zanzibar.

Lakini nchi mbali mbali duniani ambao huwa na wachezaji wa kimataifa, kuna mchezaji ambaye huwa balozi wa kuitangaza nchi yake.

Je, kwa Zanzibar ni mchezaji gani ambaye ametambulika rasmi kuwa balozi kwa kuitangaza Zanzibar katika sekta ya utalii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri kabisa.

Lakini napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni swali lake la kutaka ni mchezaji gani ambaye, kwanza nataka nimueleweshe kwamba

Zanzibar yenyewe haijawahi kusajili mtu ambaye anachezea nje, kwa sababu sisi si wanachama wa *FIFA* na kwa muda wote huo sisi hatukuwa wanachama wa *CAF*, tumeupata juzi tu na baada ya kukamilisha Katiba zetu ndio tunaweza tukafikia hatua hiyo ambayo amewaeleza.

Kwa hivyo pamoja na suala la Mhe. Abdalla Maulid Diwani alilouliza mwanzo ni *TFF* ndio inayofanya usajili kama alivyojibu kwamba Tanzania ilikuwa ni moja, kwa hivyo masuala yote yalikuwa yanafanywa na Tanzania kupitia *TFF*.

Lakini kwa mchezaji huyo aliyemtaka Mhe. Mwakilishi ni kwamba hatuwezi kusema jina fulani kwa sababu ni mchezaji wa Zanzibar, bado tubakishe ni wachezaji kwa wakati ule wa *TFF* chini ya Tanzania. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuona Mhe. Nassor Salum Ali kuhusu utaratibu nakuomba tukae Mhe. Ali Salum Haji tuendelee.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na Naibu Waziri.

Kama Mhe. Naibu Waziri alivyokiri kwamba masuala ya wachezaji sasa hivi yamekuwa yanasaidia nchi katika kuitangaza kwa mambo mbali mbali. Mimi nataka kuuliza swali dogo tu.

Serikali ina mipango gani ya kuanzisha skuli itakayochukua vijana wenye vipaji maalum na hususan vya soka ili kuweza kuwatunza, kuwaendelea na baadae tuje kuwa na vijana wazuri kama mfano wenzetu wa Tanzania Bara walivyoanzisha Skuli ya Makongo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Mchezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba napokea kuwa swali lake amelileta kwa njia ya ushauri na hili nalichukua tutalifanyia kazi, lakini naomba nimjibu zaidi tu kwamba tayari sasa hivi tumeshaanzisha ligi ambazo zitaibua vipaji kwa vijana wetu. Kati ya ligi hizi ni katika njia ambazo tumejipanga kuinua vipaji na kuwaenzi vijana hawa ili kuona kwamba tunapata wachezaji wazuri kwa ajili ya kutuwakilisha kimataifa.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Utaratibu

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kwa hisani yako

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Nassor Salum Ali: Mhe. Mwenyekiti, nikitumia Kanuni ya 37 naomba niinukuu.

“Waziri, au Mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi..."

Mhe. Mwenyekiti, swali langu wakati nauliza swali hili nilinukuu maneno ambayo aliyojibu Mhe. Waziri na nanukuu jibu lake ambalo amelijibu.

“Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa wachezaji hao nje ya nchi kunaifanya Zanzibar kutambulika na kuonekana kupitia ramani ya michezo na hivyo kuchangia ujaji wa watalii na kadhalika”.

Sasa kutokana na jibu lake ndio nikauliza ni mchezaji gani ambaye anatambulika kama balozi wa kuitangaza Zanzibar. Kwa hivyo nilikuwa nataka kujua ni mchezaji gani huyu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hayo majibu ameyatoa umesema kutokana na majibu ya Mhe. Waziri na majibu aliyokupa ni yeye, nahisi inatosha tu kuwa amekujibu.

Nam. 124

Utendaji Kazi wa Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi inafanyakazi vizuri sana kwa kufuata taratibu na sheria na kwa sasa wananchi wengi wameanza kufahamu umuhimu wa kuitumia vyema bodi hiyo.

(a) Je, ni mafanikio na changamoto gani ambayo serikali imezipata tokea kuanzishwa bodi hiyo.

(b) Je, kwa kipindi cha 2015/2017 bodi hiyo imeshahaulisha maeneo na nyumba ngapi na kuzipatia hati mpya kwa wahusika wapya.

(c) Je, kwa kipindi cha 2015/2017 Bodi imekusanya kiasi gani cha fedha ambazo zimeingia katika mfuko wa serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 124 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo**:-**

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Bodi imepata mafanikio na changamoto zifuatazo:

MAFANIKIO:

1. Kudhibiti uhaulishaji holela kwa wananchi
2. Kujenga uelewa kwa watendaji wa serikali na wananchi.
3. Kuweza kuweka kumbukumbu kwa njia za kisasa.
4. Kupunguza muda wa kujadili maombi ya uhaulishaji kutoka siku kumi na nne hadi siku saba.
5. Kuwasaidia wananchi kuingia katika mfumo sahihi wa kuhaulisha na kuwawezesha kupata hati za matumizi za maeneo yao
6. Kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi na kuyafanyia upangaji maeneo yanayoombwa kuhaulishwa ambayo hupimwa rasmi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi.
7. Kuzibaini ardhi za eka tatu, maeneo ya serikali na ardhi za kilimo zinazovamiwa na kutoa ushauri wa kuyadhibiti maeneo hayo.
8. Kubaini wawekezaji wasiofuata taratibu na kuiarifu serikali kuyafuatilia na kuchukua hatua.

CHANGAMOTO:

1. Muingiliano wa majukumu baina ya Bodi na taasisi nyengine. Mfano, Ofisi ya Wakfu.
2. Baadhi ya wananchi kutokuwa na uthibitisho wa kumiliki haki ya matumizi ya ardhi.
3. Kuwepo kwa baadhi ya wananchi ambao hawafuati taratibu za uhaulishaji na kuishia kufanya uhaulishaji kinyume na sheria kwa kufanya maandikiano baina yao au kufanya mikataba ya wanasheria.
4. Kuwepo kwa wananchi wengi wanaochukua fomu za maombi ya uhaulishaji na baadae hawazirudishi katika Ofisi za Bodi kwa hatua.
5. Wananchi kukiuka taratibu kwa kulipana wanapotaka kuuziana kabla ya kupata maamuzi ya uhaulishaji.

(b) Kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi Machi, 2017 Bodi imeidhinisha maombi ya uhaulishaji 1,326. Katika kipindi hicho maombi 1,404 yametolewa idhini ya uhaulishwaji kwa wahaulishwaji wapya. Utofauti huu wa idadi ya maombi yaliyoidhinishwa kutofautiana na vyeti vilivyotolewa ni kutokana na utaratibu wa kutolewa hati hufanyika mara baada ya waombaji kukamilisha taratibu za kulipia ada za uhaulishaji. Hivyo idadi hiyo ya vyeti inajumuisha pia maombi ya miaka ya nyuma ambao walikamilisha taratibu ndani ya kipindi hicho cha 2015 hadi 2017.

(c) Bodi imekusanya jumla ya wastani bilioni 2,100,000,000 kwa kipindi cha kuanzia 2015/2017 kwa wastani wa milioni 700,000,000 kwa mwezi, bali fedha hizo zinatumika kwa matumizi ya shughuli za Bodi, hivyo haziingii kwenye Mfuko wa Serikali. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa nimeona hapa kwamba Bodi imefanya kazi nzuri kwa ajili ya uhaulishaji, katika maombi 1,404 wamewapatia hati za ruhusa watu 1,326 ina maana ni maombi 78 tu ambayo hayakupatiwa hivyo vibali. Lakini kwanza nilitaka nijue ni sababu zipi ambazo zimesababisha hawa wasipate hivi vibali. Pia je, Bodi ya Uhaulishaji kwa kushirikiana na Idara ya Upimaji wana utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba yale maeneo mapya yanayojengwa sasa hivi wale wanafuata utaratibu wa ujenzi wa mipango miji hasa tukiangalia kwamba maeneo ya zamani mengi yamejengwa kiholela na bado ujenzi ule holela kwa maeneo ya hivi sasa inaonekana bado unaendelea.

Je, Bodi kushirikiana na Idara hii wana utaratibu gani. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Sababu kuna nyingi zinazopelekea kitu kisihaulishwe, miongoni mwake kama ambavyo nilikuwa nimesema kwenye upande wa mafanikio kwamba kupitia hii *process* tunabaini sasa kwamba hii ni eka tatu, hii ni ardhi ya kilimo na maeneo hayo yanakuwa hayahaulishwi.

Lakini pia kama tukigundua eneo lina utata ama mgogoro basi halihaulishwi. Lakini pia kama kanisikiliza kwa makini wakati nazungumzia mafanikio, basi nilisema kwamba kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi na kufanyiwa upangaji wa maeneo yanayoombwa kuhaulishwa ambao hupimwa rasmi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi. Tatizo ama changamoto iliyokuwepo ni

kwamba baadhi ya wananchi hawafiki katika maeneo haya, wanamalizana huko huko, lakini kama ingekuwa wote wanakuja basi kwa kiasi kikubwa hii migogoro ya ardhi ingepungua.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza Bodi kwa kazi nzuri inayofanya lakini pia namshukuru Waziri na watendaji wake kwa kusimamia vyema kupunguza au kuondoa kabisa migogoro katika yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha nyuma palikuwa na utaratibu mzuri Bodi inatangaza rasmi kwamba leo kipindi hiki tutafika eneo fulani kwa usajili wa mambo mbali mbali, lakini sasa hivi somo hilo halipo na wananchi wengi bado hawajasajiliwa na kupata usajili wa hati mpya.

Je, wizara kupitia Bodi hii ina mpango gani wa kuendeleza endelezo hilo ili wananchi wapate hati mpya kuondokana na matatizo hasa sehemu za Ng'ambu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu kwanza nipokee pongezi hizo lakini ni kwamba anachozungumzia Mhe. Mwakilishi ni usajili na sio uhaulishaji ni vitu viwili tofauti.

Bodi ya Uhaulishaji inafanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu lakini pia na usajili inafanya kazi kwa muijbu wa utaratibu. Sasa hivyo ni vitu viwili tofauti.

Nam. 83

Ugawaji wa Gari za Kubebea Wagonjwa (*Ambulance*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni Wizara ya Afya imepata msaada wa gari za kubebea wagonjwa (*Ambulance*) ambazo zinakusudiwa kutumika katika kuimarisha sekta ya afya nchini.

Je, utaratibu wa kuzigawa gari hizo za kubebea wagonjwa ukoje hasa ukizingatia baadhi ya maeneo kama Hospitali ya Makundichi hawana gari hiyo badala yake wanatumia gari ya jimbo jirani la Paje.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Paje pamoja na Mhe. Mwakilishi wao kwa uzalendo walionesha wa kuridhika *Ambulance* ya jimbo lao kutumika kwa kutoa huduma katika Hospitali ya Makunduchi pale inapohitajika. Hii imetuthibitishia kwamba wananchi wa Jimbo la Paje wana upendo na imani kubwa kwa wananchi wenzao wa majimbo yote.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hivi karibuni Wizara yangu ilipata msaada wa gari nne (4) ya kubebea wagonjwa (*Ambulance*) kupitia Shirika linaloshughulikia Idadi ya Watu Ulimwenguni (*UNFPA*). *Ambulance* hizo wizara yangu ilizigawa kama ifuatavyo.

Ambulance mbili ziliachwa kwa matumizi ya hospitali za Unguja na *Ambulance* mbili zilipelekwa Pemba kwa ajili ya matumizi ya hospitali za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, *Ambulance* mbili zilizowekwa kwa matumizi ya hospitali za Unguja nazo ziligaiwa kama ifuatavyo.

Ambulance moja ilipelekwa Makunduchi na *Ambulance* iliachwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na zote hadi sasa zinaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa. Hivyo, kutokana na mgao huu hospitlai ya Makunduchi sasa inahudumia wagonjwa ikiwa na *Ambulance* mbili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida tunapopata *Ambulance* au vifaa vya hospitali na kwa bahati vikawa havitoshelezi kwa mahitaji ya vituo vyetu na hospitali zote, Wizara hugawa kwa uchache wake kutegemea na mahitaji halisi na umuhimu wake katika hospitali husika. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuliona hilo na kwa niaba ya wananchi wa Paje ingawa sijawauliza lakini najua kama ulivyosema kwa niaba yao nimechukua pongezi hizo na kwa kweli Mhe. Naibu Waziri hili suala nilileta kabla *ambulance* hizo hazijagawiwa, baada ya kuleta swali hili kama kuwahimiza zimegawiwa nishukuru kwa hilo, kama kuwashituwa na ndio wajibu wetu sisi Wawakilishi. Maana yake timu ya mpira yule kocha ndiye anayeiona zaidi akiweko juu. Kwa maana hivyo naomba niulize swali moja dogo sana la nyongeza.

Ambulance zile iliyokwenda Makunduchi ni haki yake kwenda Makunduchi kwa kweli, na kazi inayofanywa kwa madaktari wa Makunduchi niipongeze kwa dhati chini ya uongozi wenu, lakini ilikuwa inahitajika bima pale. Sasa bima ile imepewa Wizara ya Afya au Mbunge au Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, *ambulance* ile iliyopelekwa katika Hospitali ya Makunduchi bima yake itafanywa au imefanywa na Wizara ya Afya, lakini Mwakilishi na Mbunge wa Jimbo husika ukiamua kufanya kwa ajili ya wananchi wako, kwa ajili ya serikali yako, uko *right* na tutakushukuru sana kuweza kutoa msaada kama huo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kuhusiana na suala mama lililoulizwa na Mhe. Jaku Hashim.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha na mimi nimefarajika sana kwamba Hospitali yangu ya Makunduchi imepata *ambulance*.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni dogo sana la nyongeza. Kunakuwa na malalamiko ya wananchi hususan wale wanyonge kwamba wanapohitaji kumleta mgonjwa mjini kwa *transfer* huwa wanachangishwa mafuta kuweza kuona *ambulance* hiyo inafanya kazi. Suala hili Mhe. Naibu Waziri analielewa na kama analielewa litaondoka lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa ni kweli hali kama hiyo huwa inatokea baadhi ya wakati, lakini kwa kawaida *ambulance* zile zimetengewa mafuta yake maalum, lakini kwa sababu ya mrundikano wa wagonjwa mara kwa mara kuhitajika kupelekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, basi mara nyengine mafuta humalizika na wananchi hutakiwa kuchangia kidogo ili kupeleka mgonjwa yule. Lakini si aghalabu sana inatokezea kama ni kwa bahati mbaya.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza niipongeze Wizara ya Afya kwa kupeleka magari mawili ya wagonjwa katika hospitali za Pemba. Napenda kuuliza swali dogo kwa Mhe. Naibu Waziri.

Je, ni hospitali zipi ambazo za Pemba zimepelekewa magari haya ya kubebea wagonjwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti ahsante. Hospitali za Pemba ambazo zina magari ya wagonjwa ni Hospitali ya Abdalla Mzee ina gari tatu za wagonjwa, lakini moja ni mbovu, Hospitali ya Wete ina gari tatu za wagonjwa lakini moja ni mbovu, Hospitali ya Chake Chake ina gari mbili za wagonjwa, Hospitali ya Vitongoji ina gari moja ya wagonjwa na Micheweni kuna gari mbili za wagonjwa na zote zinafanya kazi.

Utaratibu

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimeipongeza wizara kwa kupeleka magari mawili ya wagonjwa Pemba, nilitaka kujua haya magari mapya mawili yaliyopelekwa Pemba yamepelekwa hospitali ipi na ipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuombe radhi Mhe. Mwakilishi Hamad Abdalla Rashid Gerei wa Wawi kwamba kwa bahati mbaya sikumuelewa na sikujua kwamba sikumuelewa.

Hospitali mbili zilizopelekwa magari hayo Pemba, moja imepelekwa katika Hospitali ya Micheweni na gari moja imepelekwa katika Hospitali ya Chake Chake kwa sababu ilikuwa mbovu gari lake.

Nam. 31

Fidia kwa Wananchi Walioathiriwa na Ujenzi wa Barabara ya Mwanakwerekwe hadi Fuoni

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni, Waziri Mkuu alimwakilisha Rais wa Tanzania pamoja na kuhimiza kupewa kipaumbele Kampuni za ndani katika ujenzi wa barabara zetu, alitaka wananchi walioathirika katika ujenzi wa barabara hiyo walipwe fidia.

Kwa kuwa maelekezo ya Kiongozi wa Kitaifa ni wajibu kutekelezwa, ni lini wanachi hao watalipwa fidia zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ulipaji wa fidia kwa wananchi waliothirika katika ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni ni kwamba mnamo mwaka 1983 serikali iliweka michoro maalum yenye kuonesha eneo la hifadhi ya barabara. Katika hatua hiyo, wapo wananchi ambao nyumba zao zilikuwa tayari zimeshajengwa na pia wapo wananchi walioruhusiwa baadae kujenga katika maeneo hayo kwa kupewa hati miliki na serikali. Orodha za wananchi hao ipo na watalipwa mara tu taratibu za ulipaji wa fidia zitakapokamilika.

Aidha, kuna wananchi walioruhusiwa kujenga maeneo hayo kwa kuendesha shughuli zao za kibiashara. Wananchi hao walipewa hati ya muda (*lease*) kwa makubaliano ya kwamba maeneo hayo ni ya serikali na pale yatapohitajika basi wananchi hao wataondoka bila ya kufidiwa cho chote. Hivyo serikali haitawalipa fidia watu wa aina hii wala wale waliojenga bila ya kushirikisha au kuwa na hati miliki.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, awali ya yote nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na vile vile niipongeze kwa jinsi barabara ilivyokuwa nzuri kwa kupendeza kuondoa msongamano katika mji wetu. Lakini swali langu la nyongeza lina (a) na (b).

(a) Ni lini utaratibu huo utakamilika ili walipwe wale wanaostahiki bajeti ya mwaka huu 2017/2018 au 2018/2019.

(b) Pamoja na uzuri wa barabara ile, lakini bado ina changamoto ya kuilinda barabara ile. Kwa mfano, barabara ile sasa hivi inakosa mitaro kwa ajili ya kuondosha maji ambayo hayastahiki kukaa pembezoni mwa barabara ile ili kuona kwamba inadumu siku nyingi. Je, wizara yake ina mpango gani kuandaa mpango wa kuweka mitaro kwa kulinda barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kwamba lini tutawalipa kama nilivyosema tulikuwa katika taratibu na nina imani kubwa sana serikali yetu pale ambapo inahisi watu wanastahiki kulipwa haki yao basi tutawalipa na Inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu bajeti hii ya 2017/18 watu wale tutawalipa haki zao wanazostahiki. (*Makofi*)

b) Ile barabara kama alivyosema tumejenga kwa utaratibu maalumu na tumejenga baadhi ya mitaro kama tunavyojua, lakini sasa kuna baadhi ya sehemu ambazo kutokana na wananchi kwamba yale maji iwapo kama hatujajenga mitaro ingekuwa maji yale yanaingia kwenye nyumba zao. Kwa

hivyo tumeangalia kuna baadhi ya sehemu tutafanyia utaratibu wa kuangalia tujenge hiyo mitaro anayosema. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuwa ni mazuri, mimi nataka kujua tu, wananchi wa pale wangapi wanaostahiki kupata haki yao na wangapi wataokosa haki katika majibu yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba wale wanaostahili kupata malipo kutokana na mujibu wa muongozo niliosema wa mwaka 1983 ni watu tisa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi niipongeze wizara kwa kuhakikisha kwamba tumejengewa barabara nzuri ambayo inastahiki katika mazingira yetu tuliyokuwanayo. Lakini swali langu liko hapa, kwa kuwa kuna maeneo wananchi walivunjiwa wakati wa kujenga barabara zile na majibu yake tumeyapata kwa Mhe. Naibu Waziri.

Je, kwa kuwa hivi sasa kuna watu wanajenga katika ya karibu ya barabara na hatujui hatma ya miaka ishirini mbele au thalathini itakuwaje. Wizara ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi wale ili wasije wakapata hasara mbele

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake kama ifuatavyo.

Kwanza mimi niwapongeze watu wa Idara Maalum ya SMZ hasa Wizara hii ya TAMISEMI kwa sababu ni karibuni tu Mkuu wa Mkoa wa Mjni/Magharibi ametangaza kwamba wale wote waliovamia maeneo ya hifadhi ya barabara basi waondoke mara moja. Kwa hivyo mimi naomba utaratibu huu uendelee kwa Mikoa yote na sisi vile vile tutaweka utaratibu kuwaonesha zile hifadhi zetu za barabara ili wananchi wasiingie katika maeneo yale.

Lakini naomba tena Masheha na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ wasikubali kutoa vibali katika sehemu ambazo tayari zimeshapimwa na mipango miji na vijiji. Naomba sana hilo na wananchi wasikubali kuingia katika mtego huo kwa sababu hatuko tayari kuchukua fidia kwa watu wote watakaovamia barabara zetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 74

Marekebisho ya Barabara ya Madema-Michenzani-Bwawani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa matumizi ya barabara yamekuwa makubwa kutokana na kuongezeka shughuli za kimaisha na vyombo vya usafiri, kwa kuwa barabara ya kutoka Madema kuelekea Michenzani mpaka Bwawani ina nafasi kubwa katikati ambayo imewekwa nguzo za taa na bustani na kuchukuwa nafasi kubwa sana.

Kwa nini barabara hii haipunguzwi nafasi hiyo ya katikati kama ilivyo barabara ya Magomeni-Fuoni ili kutoa nafasi zaidi ya matumizi ya barabara hiyo kama vile maegesho ambayo yangesaidia kuongeza mapato kwa serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya kutoka Madema kupitia Michenzani mpaka *Muzamil Center* ni barabara mbili zilizojengwa kwa kuacha kati kati eneo lenye upana usiopungua mita nne. Eneo hilo hutumika kwa kufanya bustani ili kuipamba barabara hiyo pamoja na kuweka nguzo za taa.

Mhe. Mwenyekiti, barabara zilizopo zinatosheleza kupitisha gari pamoja na kuongezeka kwa gari kwenye mji wa Zanzibar. Tatizo kubwa la kuonekana barabara kuwa finyu ni kuwa wafanya biashara wenye gari kuegesha magari katika maeneo hayo wakati wanaendelea na biashara zao katika maeneo yale husika.

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wa Idara yetu ya UUB kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Zanzibar hivi karibuni waliitembelea barabara hiyo kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa namna ya kulitumia eneo la kati kati ambalo Mhe. Jaku Hashim aliulizia kwa lengo la kutimiza au kwa lengo la kuhakikisha kwamba gari zinaegeshwa sehemu zile. Tumekaa nao na wamesema kwamba wataangalia utaratibu ule na kama utawezekana basi tutafanya hiyo kazi ili kupunguza msongamano wa zile gari kukaa maeneo ya pembeni. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza.

Mita nne ni eneo kubwa Mhe. Naibu Waziri na pale serikali inapata mapato hasa ya Manispaa, imekuwa ikikusanya pesa tu na tujifunze katika barabara ya Fuoni kama swali langu la msingi lilivyo, lichukuliwe likazingatiwe zaidi, ile barabara imekuwa *busy* kubwa sana sasa barabara ile. Mote munalazwa magari sasa hivi na Manispaa mote wana-*charge* magari.

a) Je, ni lini watalifikiria suala hili wakalizingatie zaidi kuliko walivyozingatia hapo mwanzo.

b) Mmezingatia vipi katika ujenzi wao hasa barabara kuhusu walemavu hakuna alama zozote zinazowekwa za walemavu katika barabara zinazojengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake ya nyongeza mawili kama ifuatavyo.

a) Kama nilivyosema ni kweli ni usumbufu mkubwa sana na sisi tunashuhudia. Mimi nikiwa mdau sana kutumia barabara zile kwa sababu nyengine ziko katika jimbo langu, kwa hivyo ni karibuni tu nilizungumza na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani na ameniahidi kwamba wanaendelea na kazi ya kuhakikisha kwamba zile gari zinazokaa mule basi wanazichukulia hatua ili gari zile zisikae pale.

Tunajua kwamba Manispaa wanataka mapato lakini vile vile tunataka msongamano wa watu uondokane. Kwa hivyo kama nilivyosema mwanzo tumekaa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Mji Zanzibar na amekubali kwamba hata hilo pia litasaidia katika kuongeza wigo wa mapato. Kwa hivyo tuachie tupe muda ili suala tunalifanyia kazi na nina imani litakuwa kwa maslahi ya wananchi wetu.

b) Suala lake kuhusu walemavu kweli hili tumeliona na kuna kipindi Mhe. Mwantatu Mbaraka alizungumzia hapa barabara ya Mwanakwerekwe tuliyojenga. Kwa hivyo tutalichukua na kulifikiria zingatio maalum kwa sababu na sisi pia linatugusa hasa kwa watu wenye ulemavu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe maswali yalipangwa kwa siku yetu ya leo yamemalizika lakini kabla ya taratibu nyengine nilikuwa naomba

niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri yale majawabu ya maandishi wanawajibika wayalete ndani ya siku tatu kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza 40(4). Nilikuwa nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wasingoje kukumbushwa na Ofisi za Baraza, muhakikishe ndani ya siku tatu yale majawabu yamepatiwa ufumbuzi na yameletwa. (*Makofi*).

La pili Waheshimiwa Wajumbe michango naona inaendelea kuletwa hapa, kwa hivyo wale wote ambao wameleta michango yao, nawaomba wapeleke michango hiyo kwa maandishi kwa sababu nitawapa nafasi wale Wajumbe waliotajwa jana na baadae kuwapisha Mawaziri watoe ufafanuzi na leo hii inatakiwa hii bajeti ipitishwe.

Kwa hivyo nilikuwa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wameanza kuleta leo kwa ajili ya kuchangia, naomba wafuate taratibu hizo wachangie kwa maandishi.

Ahsanteni, katibu kinachofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh akifuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo na Mhe. Mohamed Said Mohamed ajitayarishe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii ya kukushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia wizara moja muhimu katika nchi yetu hii ya Kimapinduzi Zanzibar ambayo inaongozwa na mtoto wa Jemadari wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari, 1964 Balozi Ali Abeid Karume na Naibu wake Komred Mohamed Ahmada Salum.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua kwamba miongoni mwa Wizara muhimu kwa Zanzibar kwani ni wizara ambayo ina jukumu la kutujengea barabara zetu ili kuweza kupita pamoja na kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa wizara hii kwa kufanya kazi nzuri ya kuwaletea maendeleo ya barabara wakulima na wakwezi wa nchi hii, kwani ni wazi kwamba sasa zamani kule

kwetu Mchangani ilikuwa kuzileta embe shomari mjini ilikuwa ni mgogoro, lakini leo embe zinapovunwa tu Mchangani baada ya nusu saa au dakika kumi zimefika sokoni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa wizara hii nitaanza na Programu Ndogo ya Utunzaji na Matengenezo ya Barabara. Ninaamini katika wizara hii kuna Idara ya UUB, idara maafuru sana ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kujenga na kutunza barabara zote za Zanzibar, hii ndio kazi za msingi za idara hii na Idara hii ina watendaji wengi wanaolipwa mishahara na watalamu tena wataalamu wazuri waliosoma ndani na nje ya nchi.

Lakini masikitiko yangu makubwa Mhe. Mwenyekiti, tunapotaka kujenga barabara zetu hutafuta makampuni ya nje ili waje kujenga barabara zetu hali ya kuwa idara ipo, baadhi ya vifaa wanavyo na watu wapo. Lakini wanatafuta makampuni ya nje kuja kujenga barabara zetu ambazo zinatu-*charge* pesa chungu nzima. Kama tutaendelea na utaratibu kama huu Mhe. Mwenyekiti, wa kuyatafuta makampuni ya nje kuja kutujengea barabara zetu, mimi naamini maendeleo ya Zanzibar tunapotaka yafikie tutachelewa, kwa sababu makampuni haya yanatu-*charge* pesa nyingi na pesa ambazo kila siku inakuwa tunakopa ili kuyalipa makampuni hayo, nitatoa mfano.

Mhe. Mwenyekiti, karibuni tu hapa naipongeza sana Serikali imejenga barabara ya Fuoni kutoka pale makaburi mpaka kituo cha Polisi Fuoni ni kazi nzuri serikali imefanya. Barabara ile ina ukubwa wa killomita nne kama sikosei lakini pesa iliyolipwa kampuni iliyojenga barabara ile kama sikosei ni karibu bilioni mia tano mpaka mia sita bilioni kwa kipande cha kilomita nne.

Mhe. Mwenyekiti, hizi ni pesa nyingi, pesa hizi kama tungeweza kuzitia pale Hospitali ya Mnazi Mmoja basi ingekuwa ipo sawa sawa na Hospitali ya *Hatom Ccoss* iliyokuwepo nchini Uengereza, lakini tumeweza kujenga barabara. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa naomba nisikitike na naomba nimwambie Mhe. Waziri kutafuta makampuni haya ya nje kuja kutujengea mabarabara yetu, tena yanakwenda mbio sana, nasikia hufikia hadi kuhonga makampuni haya ili yapate *contract* ya kujenga barabara. Hiyo ni peke yake Mhe. Mwenyekiti, inaonesha wazi kwamba makampuni haya yanataka faida kubwa yako tayari kuhonga ili yapate kupata ile *contract* ya kujenga barabara.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri tutumie *UUB* ambayo ni Idara ya Serikali ina jukumu ya kujenga na utunzaji wa barabara katika kutengeza barabara zetu. Mimi naamini kwa watendaji tulionao na baadhi ya vifaa

tulivyonavyo kilomita nne hii ya kutoka Makaburini- Fuoni hadi Kituo cha Polisi, *UUB* walikuwa na uwezo kabisa wa kujenga na bilioni sita hizi tulizozilipa, tungetumia karibu bilioni mbili tu katika kujenga barabara ile lakini kwa kuipa *contract* kampuni ya nje leo hii tumetumia karibu bilioni sita. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni pesa nyingi za wakwenzi na wakulima. Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati wa kutumia taasisi zetu za ndani. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia pesa hizi tulikuwa na uwezo kabisa wa kununua vifaa vilivyokuwa hatuna na pia tukaijenga barabara kwa pesa hizi hizi kwa kutumia Idara yetu ya *UUB*.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana utaratibu huu wa kuyatumia makampuni ya nje kutujengea barabara ufe na bali tutumie kampuni yetu na tuijengee uwezo wa kununua vifaa na uwezo wa mambo mengine. Mimi nakaa Fuoni na sikumuona mtaalamu hata mmoja kutoka nje aliyekuja kushughulikia kujenga barabara ile, wataalamu wote ni wa ndani lakini wa kampuni binafsi, kama tulionao sisi na wengine kutoka Idara yetu hiyo hiyo walikuwa wanatoa utaalamu kwa kusaidia. Mhe. Mwenyekiti, lazima umefika wakati wa kuzitumia taasisi zetu za ndani na si makampuni binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika Idara ya Usimamizi wa Usafiri wa Barabara, Idara ya Leseni na Usafiri. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii jukumu lake ni Leseni na Usafiri. Mhe. Mwenyekiti, tunazo daladala mimi nilivyokuwa mdogo nakumbuka kulikuwa na mabasi Shirika la Mabasi pale Kijangwani. Nakumbuka Mheshimiwa Mtoka, mzee mmoja akiitwa Mtoka alikuwa anakaa Kwahani aliwahi kuwa Meneja wa Shirika la Mabasi.

Mhe. Mwenyekiti, mabasi yale yalikuwa yanatoa *services* kwa wananchi na kulikuwa hakuna ajali kama zilivyo sasa hivi. Ajali zimekuwa nyingi wanaoendesha daladala wanauwa karibu kila siku watu sita mpaka saba kwa mujibu wa takwimu wanawauwa, kwa sababu hawajali wananchi. Mhe. Mwenyekiti, tumechoka kuuliwa na waendesha daladala, tumechoka wananchi wetu kusumbuliwa na waendesha daladla. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana uanzishe Shirika la Mabasi Zanzibar ili litoe *services* kwa wananchi.

Kadhalika Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri atujibu lini ataweka vituo katika barabara kuepusha ajali za kizembe. Mhe. Mwenyekiti, haiwezakini muendesha daladala kamuona abiria kwa shilingi mia tatu anasimama popote bila ya kujali kama atauwa. Hivyo ndivyo ajali nyingi zinavyotokezea, mwenye daladala anasimama popote hajali. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana anijibu Mhe. Waziri atakapokuja lini ataweka vituo vya daladala kama ilivyokuwa zamani Zanzibar. Kituo kiko pale na hatuna gani atazichukua kama muendesha daladala hajasimama katika kituo husika.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika tunawapa vijana wadogo leseni. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Sheria hii ya kuwapa leseni vijana wadogo kuendesha gari za abiria tuitizame upya, kwa sababu ukiangalia ajali nyingi zinazosababishwa na vijana wadogo wenye kuendesha vyombo vya moto hasa wanaoendesha vyombo vya abiria.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika namuomba sana Idara yake hii itizame Bima ambayo ilimlinde mwananchi. Lakini cha kushangza ingawaje Shirika la Bima haliko kwake lakini yeye ndiye mwenye dhamana ya vyombo vya moto. Kwa hivyo kila chombo cha moto Zanzibar hasa cha abiria lazima kiwe kina Bima inayomlinda mwananchi, isiwe ina Bima inayoilinda gari, kama gari imegongwa ilipwe gari lakini mwananchi anafika kufa kwa sababu wazee wake hawana uwezo, watu wake hawana uwezo, mwananchi anakufa lakini gari Shirika la Bima inailipa gari mpya, lakini mwananchi hapelekwi hospitali, kama mtu kamgonga anakuja analetewa soda siku mbili na elfu ishirini halafu basi. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu ufe tuangalie mwananchi anapopata ajali kwanza atizamwe mwanachi, kuwe kuna Bima inayom-*cover* mwananchi hadi kumpeleka nje ya nchi katika kutizama maisha yake, sio ilipwe gari.

Mhe. Mwenyekiti, ni ushahidi ulio wazi kabisa utakuta gari imegongwa Bima inalipa gari mpya milioni thalathini, milioni arubaini, milioni hamsini, lakini mwananchi anaachiwa afe, hakuna wa kumlipa, hakuna wa kumtizama. Sasa inakuwa bora gari, bora uhai wa mtu. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili tunakuomba sana wewe ndio mwenye dhamana Mhe. Waziri atwambie ana mkakati gani wa vyombo hivi vya moto hasa vya abiria kumlinda mwananchi na sio kuilinda gari kulipwa upya.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nakwenda Shirika la Bandari. Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari linafanya kazi nzuri nalipongeza. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na ufinyu wa bandari yetu na udogo wa bandari yetu tumekuwa tuna michoro na tuna maneno mengi ya kutaka kuanzisha bandari mpya ambayo ni bandari ya Mpiga Duri. Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, kama tutaanzisha Bandari ya Mpiga Duri Zanzibar asilimia kubwa ya Wazanzibari hasa vijana watapa ajira.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri huu ujenzi wa bandari ya Mpiga Duri hasa utaanza lini na utakwisha lini. Kwa sababu vijana wengi wamekuwa wanasubiri hii ajira ya bandari ya Mpiga Duri watapata ajira na nchi yetu itapata umaarufu duniani katika kukuza biashara yetu ya utalii. Lakini imekuwa maneno mengi kuhusu bandari ya Mpiga Duri. Sasa tunataka kujua leo alieleze Baraza, lini bandari ya Mpiga Duri itaanza na lini bandari ya Mpiga Duri itakamilika atupe *full program* ya ujenzi wa bandari ya Mpiga Duri

katika mchakato mzima wa kupambana na umaskini katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni wazi kabisa kama tutajenga bandari ya Mpiga Duri kama inavyosemwa na Serikali, umaskini Zanzibar utapungua katika kiwango kikubwa. Lakini isiwe *story*, iwe lini tunajenga bandari ya Mpiga Duri. Hilo nataka kuja kujibiwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda Shirika la Meli. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza serikali kwa kununua meli MV Mapinduzi II. Lakini meli hii Mhe. Mwenyekiti, ina changamoto mlango haufunguki, sijui na kitu gani. Naiomba sana serikali na namuomba Mhe. Waziri changamoto za meli hii aziondoshe ili meli hii iweze kufanya biashara vizuri iweze kuingiza mapato kama serikali inavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, si siri utafiti unaonesha meli ile haifanyi kazi vizuri kutokana na changamoto ilizonazo, mlango haufunguki, sijui wapi haisamami, mambo mengi yapo, najua serikali inayajua. Ningeomba sana yafanyiwe utafiti yaondoshwe mambo yale, yule *contract* aliyejenga meli aje ayaondoshe kwenye meli ile ili iweze kufanya biashara vizuri iingize mapato kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Shirika la Meli ukiangalia kuna kitu kimoja ambacho nimekifanyia utafiti nimekiona hakiko sawa. Shirila la Meli ni Shirika la Serikali, linatakiwa kulipa *tax*, kulipa mapato yote yanatotakiwa kulipwa katika serikali. Lakini cha kushangaza na Shirika lenyewe limeanza juzi na meli mpya imepewa juzi, lakini cha kushangaza hapa Zanzibar tuna utaratibu wa makampuni makubwa makubwa hasa makampuni haya ya mahoteli na mambo mengine yanapokuja kuwekeza Zanzibar wanapewa *tax holiday* na *tax holiday* ile inachukua karibu miaka mitano hayalipi mapato yoyote kwa serikali, wanaita *tax holiday*.

Mhe. Mwenyekiti, na hili Shirika la Meli ili liweze kujiweka vizuri nalo lipewe *tax holiday* kama yanavyopewa makampuni mengine binafsi, kambuni binafsi zinapewa *tax holiday* lakini Shirika la Meli ndio kwanza limeanza upya, linatakiwa kulipa mapato yote ya serikali, inakuwa ni vigumu kwa shirika lile kuweza kujipanga ili kuweza kujiendesha vizuri. Mhe. Mwenyekiti, naliombea sana shirika hili liangaliwe kupewa *tax holiday* kama yanavyopewa makampuni binafsi ya uwekezaji, kwa mfano mahoteli na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja katika ujenzi wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, wizara yako najua ulikuwa Waziri si wewe tarehe nane ya mwaka 2013 ilimpa mtu mkataba wa kujenga barabara, ukarabati wa barabara

Kikwajuni/Wireles, Chukwajuni-Buyu na Fuoni Kibondeni. Mhe. Mwenyekiti, aliyepewa mkataba huu alikuwa anaitwa MC/*Abdalla Contract Company*. Jumla ya fedha milioni mia moja thalathini na mbili na *some thing*. Mhe. Mwenyekiti, mtu huyu inaoneshan wazi hapa Zanzibar Ofisi hana, Ofisi yake iko Dodoma, lakini alipewa kufanya kujenga barabara hizi tatu Zanzibar, lakini ana Ofisi Dodoma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mazingira na tafiti mbali mbali ambazo tumezifanya sisi Wawakilishi tumegundua aliyekuwa Waziri wa wakati huo na waliokuwa watu wa wakati huo, kuna harufu, naomba kusema nifahamike, kuna harufu ya ujanja wa changa la macho katika kufanya kazi hii ya ukarabati wa barabara ya Kikwajuni/Wireles, Chukwani/Buyu na Fuoni Kibondeni, kuna harufu ya ujanja wa watu wachache kujinufaisha pesa za wakwezi na wakulima na kuzitia katika mifuko yao. Mhe. Mwenyekiti, ninajua Mhe. Balozi ulikuwa si Waziri wewe kwa wakati huo lakini bado ni Wizara ya serikali na wizara ipo.

Mhe. Mwenyekiti, nitaomba majibu yaliyokamilika yenye ushahidi kama ifuatavyo. Kwanza nitaomba *copy of registration* ya hii kampuni, *whether so trade* au *Limited Company,* ile kopi kwa sababu kampuni hii ilipoingia mkataba na serikali lazima kuna vitu ipeleke. Kwanza ipeleke kopi kama hii ni kampuni imesajiliwa na ni kampuni hii ni kampuni hii ni *limited company* au s*o trade.* Lakini pa nitaomba kopi ya *tin number* yake ya hii kampuni, *certificate copy* ya *tin number* yake nitaomba. Pia nitaomba *certificate* ya namba vya vyeti kwamba hii kampuni ilikuwa imesajili na inalipa kodi ya serikali. Pia nitaomba kopi ya mkataba iliyoingia na kazi iliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kama nitashindwa kuvipata vitu hivyo kwa ukamilifu kama vilivyo. Naomba sana kutumia Kanuni ya 111 Mhe. Mwenyekiti, katika kunusuru pesa za wakwezi na wakulima kuchukuliwa na wachache.

Kanuni ya 111 inasema:-

"Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani".

Mhe. Mwenyekiti, kama nitashindwa kupata kwa hii kampuni inayoishi Dodoma lakini imepewa *contract* Zanzibar ambayo inaosha wazi kuna ujanja umetumika, nitaomba Baraza lako tukufu liunde Kamati Teule kwa hili jambo fulani, tukalichunguze ili tuje kuleta uhalisia wa jambo hili kwa niaba ya wakwezi na wakulima kwamba pesa zao zisitafunwe kizembe na wajanja wachache kwa kutia mifukoni mwao.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa indhari kwamba naomba sana nipewe hivyo nilivyovitaja kwa ukamilifu kabla Mhe. Waziri hajaanza kujibu ili niweze

kujiridhisha. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, nitawaomba Wajumbe wezangu wote tushirikiane hapa kuunda Kamati Teule tukachunguze, hatuwezi na tunajua serikali yetu ina nia nzuri ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanziabar wana Mapinduzi wakwezi na wakulima. Lakini tunajua kuna wajanja wachache wamo ndani ya serikali ambao hawaitendei mema serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, wanafanya ujanja katika kuihujumu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawaipendi. Sasa hao lazima Mhe. Mwenyekiti, na walikuwemo wengine na baadhi yao wengine wamo lazima tukawafichuwe, tuwaonesha hapa kama hawa ndio wale wapinga Mapinduzi, hawa ndio wale wanapinga Maendeleo Matukufu ya Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena nitatumia Kanuni ya 111 lazima tutoke na Kamati Teule kwa kampuni hii ya *MC Abdalla contractor* ambaye naamini kwa utafiti tulioufanya, kuna ubadhirifu fulani umefanyika kwa kampuni ya Dodoma kuja kufanya kazi Zanzibar.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda ukurasa wa 31 katika kitabu chako cha bajeti ulichokuleta. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 31 Mapato na Matumizi 91. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilijipangia kukusanya jumla ya bilioni tatu milioni, mia sita na *something* kutoka vyanzo vyake mbali mbali na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya shilingi bilioni mbili sitini na nane milioni zimekusanywa, sawa na asilimia 74 ya makusanyo hayo. Makadirio ya bajeti, kwa upande wa matumizi ya Mamlaka ilijipangia kutumia jumla ya fedha bilioni mia tatu arubaini na tisa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, najiuliza kitu kimoja, halafu kwa kazi za kawaida hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya bilioni mbili, milioni mia nne arubani na nne taasisi hii imetumia. Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii imejipangia kukusanya bilioni tatu *point six* na imejipangia kukusanya, lakini ina matumizi ya bilioni tatu *point* tano, yaani kile inachokikusanya chote kinatumika. Sasa Mhe. Mwenyekiti, najiuliza hii taasisi inakusanya shilingi ishirini lakini inatumia shilingi kumi na tisa. Sasa taasisi hii ina manufaa gani kwa serikali wakati inachokikusanya chote kinatumika.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nimepata wasi wasi kilichotumika ni kingi. Nataka *breakdown* ya kile kilichotumika chote ya matumizi yote yaliyotumika mpaka kufikia leo ya hii bilioni 2.4 zimetumikaje. Kama si hivyo nitaomba kutumia kifungu cha 98(4,)(1) cha kuzuia fungu kama sijapata uhalisia wa *breakdown* wa matumizi ya pesa hizi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika Idara ya Leseni na Usafirishaji, narudi tena. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kukagua magari kwamba yale magari yanayotumika Zanzibar yako katika hali nzuri

yanakwenda vizuri na yapo vizuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kule Karakana hivyo wanavyokagua magari imeshapitwa na wakati, wameweka kifusi hivi halafu wameweka mipira ya gari. Kwa hivyo gari yako mpya Mhe. Mwenyekiti, unaipeleka kule anaingia dereva wa kule Karakana halafu anaiwasha, akeshaiwasha anaitoa resi za kweli kweli. Sasa utashangaa gari yako umepeleka upya kuwashwa mule Karakana, basi inatoka inatika yote, imeshakatika *center board*. Sasa utaratibu huu Mhe. Mwenyekiti, dunia nzima haupo. Gari kwenda kutiwa kwenye mashimo, ikiwa serikali inatengeneza barabara ili kunusuru gari na ajali, lakini kule Karakana kuna mashimo ya vifusi na mipira ya gari, gari yako mpya unaipeleka kule wanaiwasha wanaipeleka mbio, halafu ikitoka inatika yote. Aah! Mhe. Mwenyekiti, ule si utaratibu mzuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba sana serikali iweke mashine za kukagua gari, ile kukagua *manual* kwa kuipiga ma-*break* gari kuipeleka mbio, ule mimi sijauona dunia nzima, ule si kukagua gari ni kuia gari. Kwa sababu gari mpya ukaipeleke kule, ikatiwe katika mashimo yale, ikitoka inatika yote Mhe. Mwenyekiti, imeshaharibika. Maana yake hiyo gari yako kama umeipeleka kule Mhe. Mwenyekiti, ikianza kutiwa mle roho inakuuma lakini ndio huna ujanja unasema umeipeleka kukaguliwa. Sasa huku kukaguliwa kubomolewa? Mhe. Mwenyekiti, ule sio utaratibu mzuri. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aje kutwambia vipi ataweka miundo mbinu bora kule Karakana ya kukagua gari, lakini tulionao sasa si utaratibu nzuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo namalizia maana yake nakuona unataka ku-*press* kengele yako hapo, kunako *contractors*. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia Wizara hii inakuwa inaajiri ma- *contractors* wengi hasa katika ujenzi wa barabara. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tunashuhudia pia hao ma-*contractors* wanaopewa *contract* za kujenga barabara wanatuharibia miundo mbinu yetu. Kwa mfano wanatuharibia walipojenga barabara ya Fuoni waliharibu miundo mbinu ya maji yote ya barabara ya Fuoni iliharibika na walikaa karibu miezi sita hawajaijenga na ninaamini katika mikataba yao inasema ukiharibu miundombinu ya wananchi uijenge na hawakuijenga, na kulikuwa hakuna mtu wa kuwaambia, wananchi tumeishi kule Fuoni kwa miezi sita mpaka saba bila ya maji na ma-*contractors* wameshalipwa bilioni za pesa, hizi hapa bilioni tano mpaka sita lakini wamewaachiwa wananchi kuishi bila ya maji, wameharibu miundo mbinu ya umeme. Halikadhalika wanaharibu miundombimu ya mkonga wetu wa Taifa tulioutumia kwa mabilioni chungu nzima kuujenga.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii inapompa mtu *contract* akiharibu miundombinu ya wananchi Jumanne, basi lazima Jumatano waweze kurudisha. Kwa sababu hii ni serikali ya wananchi, wananchi ndio inayowapa kura, sio

waachiwe *contractors* na pesa kishalipwa kama alivyoachiwa kule, pesa kalipwa lakini alikuwa anawasumbua wananchi, na halikadhalika huu mkonga wetu alioukata huyu *contract* aliyejenga barabara ya Fuoni ambayo serikali imetumia pesa nyingi, naomba jibu kwa Mhe. Waziri, huyu *contractor* aliyekata mkonga wa Taifa, ni lini ataujenga na ataurudisha kwa sababu serikali yetu imetumia pesa nyingi.(*Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache namuomba Mhe. Waziri anijibu majibu yangu yote kama siivyo vile vifungu vyangu vyote nilivyotumia Kanuni ya 111 na kifungu kile chengine cha kuzuwia fungu pia nitavitumia atakapokuja kupitisha mafungu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kui-*support* bajeti hii kwa asilimia 50 na asilimia 50 nazibakisha mpaka nitakapokuja kujibiwa majibu yangu hayo ya kimapinduzi.

Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa mchango wako. Sasa kabla ya Mhe. Abdalla Ali Kombo nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed atafuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo, na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa busara na hekma zako na Mwenyezi Mungu akujaalie uendelee kukaa kwenye kiti hicho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu sana lakini nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. Niwapongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri kwa kutujibu majibu yake ya ufasaha kwa muda wote. Lakini pongezi za pekee niwapongeze watendaji, hasa mtendaji mkuu Katibu Mkuu wa wizara hii, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wakurugenzi wote. Najua Mhe. Rais ametumia uwezo wake mkubwa wa kuchagua majembe na yanafanyakazi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze sasa kwenye ukurasa wa 49 Shirika la Nyumba. Nataka nimpongeze sana Mkurugenzi Mtendaji kwa kazi ambazo anazifanya na anavyofuatilia. Lakini kabla ya hapo nataka niseme tu kwenye ukarabati wa nyumba hizi za maendeleo ambapo bwana wetu Rais wa kwanza wa Zanzibar bwana Abeid Amani Karume alizijenga. Naomba kwa heshima kubwa sana nizitaje baadhi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya nyumba hizi ni Kilimani, Michenzani, Bambi, Makunduchi, Mtemani na Kengeja. Mhe. Mwenyekiti, nyumba zimeleta haiba kubwa sana na mtu yeyote atakapokuja kuitembelea Zanzibar, basi mwanzo anaoneshwa kama ni *icon* ya Zanzibar ya Mzee Karume alivyotujengea na Marais wote waliokaa bado hatujathubutu kujenga vitu kama vile. Lakini nyumba hizi zimekuwa zikiachwa katika sehemu ovyo kabisa.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, niseme Majumba ya Maendeleo ya Kilimani. Mhe. Mwenyekiti, tulifanya ziara kubwa mimi na Mhe. Naibu Waziri na Wakurugenzi wake wote, kuangalia matatizo yanazozikabili nyumba zile, lakini athari kubwa zitakazowapata wananchi wa Kilimani. Wananchi wa Shehia ya Kilimani wanaoishi katika majumba yale wanapata kadhia kubwa sana na tumeona ni jinsi gani ubovu uliotokea pale. Kwa hivyo niwaombe sana Wajumbe wenzangu tujitahidi ili basi tuweze kuzitengeneza tufanye marekebisho yale ya *drainage* na mambo mengine. Ingawaje atakaponijibu Waziri sana ataniambia wana nyumba tisa, kuwa na nyumba sio kigezo, mnazo nyumba hamna, kama zipo basi tuzitengeneze kwa pamoja na hii kama nyumba tisa tu anaona yeye ndogo. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri aje pale Kilimani kwenye Shehia yetu aondowe nyumba zake zile tisa, zibaki za wananchi watupu ili basi sisi tuweze kuzitengeneza. Naomba sana kwa jambo hili Mhe. Mwenyekiti, nina nia ya kuzuwia kifungu hiki moja kwa moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema Shirika la Nyumba limetengewa bilioni 5,558,000,000/- kwa ajili ya kazi zote za maendeleo na nyengine, lakini bilioni 3 kwa sababu ya kazi za maendeleo. Lakini ukiangalia na ukubwa wa jambo lenyewe hizi pesa ni kidogo mno. Ningeomba serikali iangalie kwa jicho la huruma sana na kwa sababu ndio tunaanza na shirika hili, liweze basi kuongezewa pesa hizi ili tuone ni jinsi gani mkurugenzi anaweza akafanyakazi kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Bodi ya Usajili wa Wakandarasi hapa, pana ma-*engineers* wetu wengi tumewateuwa kuwepo pale, lakini wanafanya kazi kubwa na tuwashukuru kwa sababu wanafanya kizalendo. Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimwambie tu Mhe. Waziri awatizame wale kwa sababu ni wazalendo hawajakimbia nchi hii, awatizame kwa jicho la huruma ili kuona basi hawa ndio waokozi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika mwelekeo huu wa bajeti katika kifungu kidogo au Programu Ndogo ya Usafirishaji. Wizara inapaswa kuona sio ya nini! ni Programu Ndogo ya Utunzaji wa Barabara. Wizara inapaswa kuona kuhakikisha barabara zote za nchi hii zinakwenda katika hali nzuri sana. Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru Mkurugenzi anafanyakazi kwa bidii sana lakini

tumeona matatizo ambayo yanaweza kutokea. Kuna barabara zote, hata ukiangalia Kwa Mchina Mwanzo pale kwenye mataaa kuna uharibifu mkubwa sana. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua kwa upande wa Unguja, hata kwa Pemba tuna viwango vya barabara ambavyo tumejiwekea ni kiwango kiasi gani ambacho wakandarasi wengine, mbali ya kuwa *UUB*, mkandarasi mwengine anayepewa ukandarasi anaweza akatumia kigezo kile, ni kiwango gani ambacho tunaweza kujiwekea.

Mhe. Mwenekiti, lakini jengine tuweze kuona wakandarasi hawa ambao tunawatumia wana viwango na watapataje. Kwa sababu kuna kampuni nyingi kila ukienda barabara hii mtu mmoja, mtu mmoja, kampuni moja, kampuni moja ndio inayoomba ukandarasi, inaomba peke yake na inashinda peke yake. Nilikuwa nimeanza kupata wasi wasi mkubwa sana. Lakini vile vile bado Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi kuwa hata pesa zilizotengewa ni ndogo sana. Ningeiomba serikali nayo iionee Taasisi hii au Idara hii iione kwa jicho la huruma. Kwa sababu mabarabara mvua imetuathiri vibaya sana. Kama tukiangalia ile barabara ya Mgagadu Kiwani ni barabara ya juzi tu. Mimi nasema labda haikuwa na kiwango ndio maana ikabomoka vile.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwengine kwenye Programu ya Usafirishaji na Leseni. Niwape pongezi sana na nimeona wameongeza pesa nyingi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pesa waliopangiwa ni bilioni 1,188,974,000/- bado pesa hizi hazikidhi, na nina sababu yangu ya kusema hivi. Kwanza akaangalie jengo la Wizara ile inalotumia. Idara ile inatumia jengo ambalo halina haiba hata rangi, unaweza ukasema tu hapa panawashwa moshi, haina haiba hata kidogo, lakini kazi zao ni kubwa sana. Niwashauri tu kwamba tunao uwezo wa kuongeza mapato makubwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi boda boda zimeenea tuwape leseni maalum lakini tuwape vitambulisho maalum ili tuweze kukusanya mapato kwa kupitia boda boda.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 43 kuhusu Shirika la Bandari. Nimpongeze sana Mkurugenzi kwa kazi kubwa ambazo anazifanya na tuliwahi kupiga kelele, na kelele zile serikali imetusikia imewapa vifaa vipya na sasa ninaamini watafanyakazi vizuri sana, tuwapongeze sana na tuwape moyo kwa kazi ambazo wanazozifanya.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka niulize tu Hoteli ya *Mtoni Marine*, tumeona uchimbaji mbali mbali. Je, nataka Mhe. Waziri atakapokuja aniambie imefanyiwa *IAA* kama imefanyiwa nataka nijuwe, na kwenda kufunga zile meli za Bakharesa ni sawa au sio sawa kwenda kufunga kwa sehemu ile. Naomba

hili nipatiwe majibu lakini niwashukuru sana katika sehemu ile ya operesheni Mkurugenzi unanisikia, wape moyo vijana wanafanyakazi kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimeangalia kwa upana wake kwenye Chuo cha Mabaharia Chukwani ambacho kinadhaminiwa na *DANAOS*, kinasomesha vijana wengi sana tukipe pongezi kubwa sana. Lakini Kamati wakati ikisema inasema, bado kuna sheria hazijaridhiwa. Ni sheria nyingi sana hazijaridhiwa na niseme tu ni-*declare interest* Mhe. Mwenyekiti, kuwa hapa nitakuja na hoja binafsi. Sheria nyingi hazijaridhiwa hatujui kwa nini, Bunge linapitisha lakini Baraza halijaridhia. Tunaomba ili tuone basi ni Sheria gani hazijaridhiwa na hapa tuweze kuzifanya ili Sheria hizi ziridhiwe.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Nimpongeze sana Mkurugenzi kwa kazi kubwa na wafanyakazi wa *VIP* kwa kazi kubwa sana wanayoifanya. Lakini jengine tunaona mageuzi ambayo Mkurugenzi anayafanya katika viwanja vyetu, tulikuwa tunasema tu lakini sasa tumeona ni jinsi gani kazi kubwa imefanyika na mtu tumpe moyo kuweza kuutengeneza uwanja huu ukawa na haiba kubwa kama ile, tumpongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende kwenye *Terminal II* ya Uwanja wa Ndege wetu. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba ya Wizara ya Utawala Bora niliwahi kusema mambo ya nyaraka, nikasema sasa hivi hatuna sehemu ya kuweka kumbukumbu zetu na tunapaswa sasa kuziweka pale *Terminal II*. Jengo lile liwe ni makumbusho. Na kwa sababu gani nimesema vile. Nina sababu ambazo nimesema vile. Sababu ambazo nimesema tuweke makumbusho jengo lile, serikali imeshindwa na tumeona jana Kamati imekuja hapa ime-*declare* kabisa kama jengo serikali imeshindwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie kifungu cha 111 kuomba Kamati Teule. Hapa Mhe. Mwenyekiti, naonesha nia ya kuchukua kifungu hiki na kuweza kuomba Kamati Teule, kwa sababu gani nikasema hivi. Mhe. Mwenyekiti, wapo wafanyakazi ambao wa sehemu mbali mbali walioweza kuweka miundombinu ile, lakini hakuna kama hasara kubwa imepatikana, maana yake uwanja ule ndio ambao uliogharimu pesa nyingi duniani au uwanja unaojengwa kwa pesa nyingi duniani. Mpaka sasa umetumia shilingi milioni 128 dola, kitu cha kusikisisha ni pesa za wananchi na ni pesa za wavuja jasho, hili hatutakubaliana nalo, tunataka kusema wazi kwamba hili hatutokubaliana nalo. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu walikuwa wakisema lakini tulikuwa tukiwabeza. Sasa tulifanya utafiti wa kutosha lakini leo serikali inakuja inatuomba pesa nyengine mpya ya kuweza kuzikandamiza pale. Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi na wananisikia. Waheshimiwa Wawakilishi kwa hili Mwenyezi Mungu atatuhukumu tukizipitisha pesa hizi. Nikuombeni sana

muniunge mkono tukichukue kifungu hiki tuunde Kamati Teule ili basi tuone pesa za wavuja jasho zinakwenda katika hali nzuri sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nichangie jambo hili kubwa sana, nilikuwa nasema mambo mawili ambayo nilionesha *concern* yangu na kukerwa kwangu sana na *Airport Terminal II*, lakini nilikerwa sana na nyumba zile kongwe za Kilimani ambazo wizara imeziacha na nimeshapiga kelele sana. Nia yangu hii ninayo na ninasema siungi mkono hoja hii hata asilimia moja.

Kwa hivyo nakushukuru sana ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Dimwa. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Ali Kombo akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Ali Salum Haji ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa ukakamavu wako wa kuendesha vikao vyetu ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia ya wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo kubwa nitakuwa na maombi madogo madogo tu. Naipongeza Wizara kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya katika kipindi ambacho ni kigumu sana. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama sasa hivi wako Unguja Ukuu, kwa wale ambao wanakwenda Nyanda za Kusini wataona hali halisi ikoje. Lakini pia kwa mara ya mwanzo katika mvua kubwa namna hii hatukusikia jumba limeanguka Mji Mkongwe, kwa bahati mbaya zimeanguka kwetu ng'ambu huku. Hii imetegemea sana na juhudi zao. Ahsante sana Wizara, Waziri na Katibu Mkuu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nawashukuru kwa msaada wao wa kifusi katika jimbo langu. Ninawaahidi kwamba nitakwenda kuwaomba tena, wasihamaki. Mhe. Mwenyekiti, katika moja ya maombi yangu ni kipande cha barabara kutoka Mfereji wa Wima mpaka Hospitali ya Mwembeladu, ni kipande kidogo lakini ni kipande ambacho kina vurumai sana ya magari. Sifahamu hapa gari namba 3, 4, 5, 6, 8, na 11 zote wanatumia kipande hiki kwenda kwenye Stendi ya Mwembeladu. Mhe. Mwenyekiti, ombi langu kama kuna uwezekano hii njia iwe ya *one way*, wao ndio wataalamu. Aidha kutokea huu Mfereji wa Wima ama kutokea Kwa Biziredi, lakini tupunguze harakati ambazo zinahatarisha sana wagonjwa wanaokwenda hospitali. Hili ni ombi kama kuna uwezekano.(*Makofi*).

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwauliza Wizara hii pamoja na Tawala za Mikoa ni kitu gani hasa kinawashinda kusimamia vituo vya daladala na

kusababisha vifo vya watu wengi sana. Yaani tume-*manage* kusimamia Kimapunju Jozani kuliko kusimamia watu, hii ni hatari. Kwa hivyo nawaomba sana wizara mbili hizi kwa zikae pamoja angalau kuondosha usumbufu ambao hauna maana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru tena wizara mbili hizi Wizara hii na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kunisaidia kwamba watajenga barabara ya Magogoni/Kinuni na wenzangu wamo humu. Ninachowaomba tuharakishe hali ya njia ya Magogoni sio nzuri hata kidogo. Pia nawajulisha kwamba ni njia ambayo imetusaidia sana kwa kipindi hiki, kwenye kitengo tayari kuna shimo ambalo sio zuri. Kwa hivyo sasa kama ni *UUB* na kama ni Tawala za Mikoa nawaomba waje nikawaoneshe ni hatari muda wowote gari inaweza ikatumbukia.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, hii ndio mada kubwa kwangu mimi, kutoka njia ya Mwanakwerekwe kuja Uwanja wa Amaan, *opposite* na Kituo cha Zimamoto, hapa panajengwa nyumba juu ya barabara. Sasa nataka kuwauliza Mawaziri hawa Komredi Karume na Ndugu yangu Haji Omar Kheir ni nani aliyetoa kibali cha kujengwa ile nyumba juu ya barabara. Mwaka jana na mwaka huu Rais alikuja Mwanakwerekwe na najua kwa uzembe kama huu na mwaka kesho atakuja tena kutizama mafuriko. Bahati nzuri na Mwenyezi Mungu ajaalie hajafa mtu safari hii, lakini kwa sijui lugha gani nitumie, mimi mshamba nikisema upuuzi nimetukana, labda niseme uzembe. Kwa uzembe kama huu Komredi Mohamed Aboud utakwenda kwenye maafa siku zote. Nyumba imejengwa kwenye barabara mtu ukimuuliza atakuambia hatma, Mzee Karume kasema hatma. Mzee Karume alisema hatma uwe mzalendo ufanye kazi, sio hatma ukaharibu mambo useme hatma. Hiyo utatuumiza sisi. Kila kiongozi unamuuliza anakuambia hatma bwana wee!, Mzee Karume kasema bwana. Aaah! Mzee Karume kasema hatma ya uzalendo ujenge nchi yako. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, leo tuna hatma ile ya Mwanakwerekwe kuna Kituo cha petroli. Nina uhakika ukienda yule bwana ana *document* na kuna kiongozi itakuwa katoa pesa anataka hatma. Hatima hiyo sasa unatuuwa. Sasa hivi kuna maradhi, uchumi wa wananchi haupo, mazingira yameharibika. Juzi ana anakuja mtaalam nipo pale mbele ya Rais anamwambia hapa *Velocity, Gravity, Physics* yote kamaliza kabakia *force* na ile *middle principle,* lakini maji yanaongezeka. Sasa ndugu zangu nadhani tufikeni pahala tujionee huruma tuiheshimu nchi yetu, hatma hii haitatufikisha pahala na hawa wengi wanaochukua hatma ukiwakuta barabarani wanakwenda hivi (upande) wote hawajafa, hatma ile aliyoichukua, pesa imekwisha na huku anapepesuka mambo hayakwenda.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi kuna Mwenyezi Mungu unatuumiza, kuna hatma ya Mungu. Kwa hivyo nawaomba hapa Wizara hii initajie nani aliyetoa kibali cha kujenga pale juu ya barabara. Hii nimesema nitapitisha sina tatizo lakini ukitizama huku kulikojengwa na huku kwa sehemu ya Zimamoto tayari kuna shimo, si mtu anataka hatma. Hatma hii itakwenda wapi. Kwa hivyo hapa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri nataka unijuulishe na ikiwezekana twende tukatizame nani aliyetoa kibali cha yule bwana kujenga juu ya barabara. Nadhani dunia nzima vitu kama hivi havipo. Mimi nimetembea tembea kidogo Unguja, Pemba, Bara, Afrika, Ulaya na China lakini uzembe wa namna ile hakuna, hatma hii tuwe macho. Tutamleta Rais na Mhe. Mohammed Aboud kila siku. Kwa hivyo hili naomba sana aliyetoa kibali tuonyeshwa na naiomba Serikali kwa mara ya mwanzo tufike pahala mtu kama hafai aondoshwe, watatuuwa hawa kwa hatma.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwengine kuna malalamiko ya magari ya Chukwani, sikutumwa lakini wananchi wanalalamika kwamba daladala za Chukwani zinachelewa sana kufika kituoni. Sambamba na kwamba tumeunda kituo cha Daladala pale Skuli ya Haile Selassie, lakini kwa kweli Wizara zetu hizi hazijajitayarisha kuwajengea pahala pazuri abiria wetu. Mhe. Mwenyekiti, ukienda sasa hivi wamesambaa chini ya miti mule, wengine wako bondeni huku, wengine wako Skuli ya Ben Bella. Kwa hivyo naiomba Wizara hapa hebu tuwe makini kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jengine limeshasemwa lakini nitaongezea tu utaratibu wa boti zile kwamba zinakuja baadae zinaondoka kituoni zinakwenda Mtoni. Sasa daladala ndio naziombea kituo kizuri, lakini utaratibu ukoje. Hapa naomba Mhe. Waziri ukija unifahamishe, hizi boti zinatakiwa zikae wapi, ziende wapi utaratibu ukoje. Samahani isijekuwa tunatoa abiria huku tunakwenda Mtoni, sisemi kwamba kuna madhara lakini kinachopakiwa kionekane na kinachoingizwa kionekane. Naomba sana Mhe. Waziri ukija utupe utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, najua Serikali yangu haina kitu ni nyepesi kiuchumi lakini naomba wakati mwengine wowote tukijenga barabara sasa tujenge na mitaro. Hali kwa kweli si nzuri. Ninashukuru kupata barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni lakini kuna maeneo ambayo yalikuwa hayaingii maji, sasa hivi yanaingia maji. Naomba pesa hatuna lakini baadae tuombe tupate pesa tuweke mitaro ili kuwa na heshima ya njia zetu. Kwa mfano ukitaka kuijua Ofisi kama nzuri au mbaya, nenda mapokezi au kwenye geti. Mhe. Mwenyekiti, ukitoka Uwanja wa Ndege kama wewe ni mgeni hata kilomita moja haifiki unakumbana na maji yamejaa, mgeni ndio anaingia kwanza nchi hii. Sasa fikra zake atasema hawa jamaa wametoa maji kwenye mashamba ya *irrigation,* ile picha haioneshi nzuri na kwale waliosoma mifugo wanaweza wakasema labda hizi gari zetu zikanyage dawa zikiingia mjini tuwe hatuna

matatizo. Kwa hivyo naiomba Serikali pindipo ikipata pesa safari hii tukijenga barabara tujenge na mitaro ili nchi yetu iwe na heshima, iwe na nidhamu watu wanaopiingia hii ni hatari sana.(*Makofi*).

Jengine Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru, simtetei Makamo Mwenyekiti wa Kamati yangu lakini naiombea barabara ya Msingini Chake Chake itengenezwe, ile barabara ni muhimu sisi ambao tumekaa Pemba imetusaidia sana wakati tunasoma na imekufa vibaya. Kwa hivyo naomba itengenezwe pindipo tukipata fedha. Halikadhalika tumeambiwa Makunduchi nako mji mpya na nini, Mhe. Waziri angalau kutoka Kajengwa mpaka Mzuri kilomita sita jigonge ukienda Mwera basi iwe udongo kidogo umetupungua usije ukatucheka, nakushukuru sana.

Kwa haya machache mimi nasema sina zaidi naunga mkono Wizara hii kwa kazi ngumu inayofuata ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa akifuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, lakini la pili naomba niwapongeze viongozi wote wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba nianze moja kwa moja kwenye program Na.1(a) ya Utunzaji na Matengenezo ya Barabara, aya ya 13 na 14 kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, zimezungumzia umalizaji wa barabara kupitia Idara ya UUB kilomita 23.4 na umalizaji ambao unategemea kumalizika hivi punde kilomita 11.737 ambao umejumuisha na barabara ile ambayo iliachwa na wakandarasi wale *DB Shapria*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana Idara ya UUB kwa kazi nzuri na kazi kubwa ambayo wameifanya kwa kipindi kifupi kwa kazi hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na naiomba Serikali na Wizara hii utakapoangalia huduma wanazozitoa Idara hii ya UUB ni huduma nzuri, lakini wanakwazika sana na vifaa. Kwa hivyo ningeiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kwa mwaka wa fedha ujao angalau tuwaongezee vifaa waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia na ukisoma ripoti zilizopita hasa za matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara katika kitabu cha ripoti ya *CAG*, moja ya tatizo kubwa lililoonekana viwango vile wanajitahidi sana, lakini ule mtambo ambao wanakwenda kuwekea lami umechakaa sana. Kwa hivyo hata kutafuta ile *level* haiwezi ikakaa, unaweza kupima hapa ukapata mapungufu,

ukapima hapa imeongezeka zaidi. Lakini kazi wanafanya vizuri na mtambo ule unaweza ukauchunguza ukaja ukaukuta baadhi ya Wawakilishi wengine hapa umri wao mdogo kuliko mtambo ule. Sasa lazima Serikali ifanye jitihada ili kuboresha Kitengo hichi cha UUB kwa kuwapatia mitambo mipya hasa huu mtambo wa lami ili kazi ziende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika aya ya 23 ambayo inazungumzia Wakala wa Majengo. Katika aya hii ukiipitia vizuri utakuta Wakala huyu ana majukumu ya moja kwa moja ya kusimamia na kufanya matengenezo ya majengo ya Serikali pamoja na kuhakikisha viwango vya ubora vinafuatwa katika ujenzi wa nyumba za Serikali au majengo ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hapa imefanya vizuri sana kuwa na Wakala huyu. Ni wakati muafaka sasa kumtumia Wakala huyu katika majengo makubwa hususan nataka kuyazungumzia majengo ya Wizara ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, yapo majengo ya Wizara ya Elimu ni majengo ya Serikali hii, yanajengwa kwa muda mfupi lakini unakuta nyufa nyingi zimetokea, wako Wawakilishi wanakuja kuleta ripoti zao hapa na malalamiko kuona kuna skuli zinavuja. Sasa nimuulize tu Mhe. Waziri kupitia Wakala huyu, Serikali inawashirikishaje hasa haya majengo mapya ambayo yanataka kujengwa na Wizara ya Elimu katika hatua ya kwenye kutengeneza zabuni, hatua pia ile ya kutengeneza michoro, hatua ya *evaluation* na hatua ya *board meeting*, kwa maana ya *decision* ya kuwatafuta wakandarasi ukiacha ile hatua ya kumpata *consultant*. Sasa niseme Wakala huyu kwa sababu kazi kubwa nimeshaitaja, dhamira kubwa ya Serikali na kazi zao imeenda sambamba na ndio maana nikapongeza.

Sasa nataka kujua tu na kuuliza hapa ushirikishwaji wa majengo haya ya Serikali na nasema hususan yale majengo ya Wizara ya Elimu, maana yaliyopita yamelalamikiwa. Juzi tu Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetangaza skuli karibu tisa au kumi na moja sina uhakika wa katika eneo hilo, lakini zipo *tender* ambazo zimetangazwa karibuni. Sasa Wakala huyu katika kutimiza ile kazi yake na nadhamira nzuri ya Serikali ya kusimamia na kupata ubora wa majengo ya Serikali, kunako eneo hili wameshirikishwa kwa kiasi gani. Sasa akija Mhe. Waziri aje anijibu kunako eneo hili.

Vile vile naomba niende aya ya 57 "Uimarishaji wa Huduma za Viwanja vya Ndege vya Zanzibar". Katika Program hii Ndogo imeeleza namna ya kumpata Mshauri Elekezi na maelezo yamejitosheleza hapa walikuwa 56, tumewapata 3 lakini kazi kubwa ya *Consultant* huyu ni kufanya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study)* katika kuandaa michoro na kutayarisha zabuni kwenye Kiwanja cha Ndege Pemba. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tu katika eneo hili na mwisho kuna kipengele ambacho kimeelezea kuwa tayari Wizara inaandika

barua kwenda katika maendeleo ya Africa (*AfBB).* Sasa nilikuwa niulize kitaalamu kwa sababu katika maelezo ya humu, katika kuyapitia tumeyaona kuwa kimoja ambacho kinakwenda kuangaliwa ni ile *financial evaluation* ya hawa watatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Wizara isifike hatua ya kuwafanyia *financial evaluation* yenyewe kabla ya kuwapeleka katika Benki ya Maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu ukiacha hayo masharti tunayokwenda nayo, tumeona mara nyingi tunazipitisha kampuni na zinapitishwa na hawa wafadhili wanaotupa fedha tunaridhia kila kitu kwa sababu ya masharti wanayotuwekea baadae wanakuja kushindwa kazi huku. Sifikirii kama hawa Benki ya Maendeleo kama wanaweza wakawafanyia ile *Due Diligence* nzuri ambayo inaweza ikaja kutusaidia sisi kuangalia ile *cash flow* ya hawa *consultants* ambao wameainishwa hapa. Sasa niiombe tu Wizara katika hatua ya kuangalia hili, wangefanya wao kwanza wakapeleka ripoti nzima baadae benki hii ikapata kumchangua mmoja katika wale watatu kama *performance* yao inaonekana kuwa nzuri. Kwa hivyo na hapa tu niishauri Serikali ifanye utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nirudi tu kidogo kuna aya hapa imenipita ya 55 ambayo inazungumzia "Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria Kiwanja cha Ndege (*AKIA) Terminal 11"*. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana niipongeze Serikali katika hatua nzuri ya upatikanaji wa fedha, lazima tukiri tulifika pahala katika eneo hili jengo limekwama kwa muda mrefu. Kwa hivyo Serikali imehangaika imepata fedha zimeainishwa, fedha kutoka *Exim Bank* ya China. Kwa hivyo kwanza ni hatua ya kuipongeza Serikali lakini kuipongeza Wizara katika hatua njema ya mafanikio ya umalizaji wa lile jengo, tusingependa libakie vile. Tunapenda limalize na mimi sitaki kwenda huko nyuma nataka kuanza hapa na kuishauri Serikali. Katika utaratibu huo kiukweli mimi naomba niishauri Serikali katika maeneo ninayoyataja.

Kwanza naiomba Wizara washirikiane na Wizara ya Fedha na Mipango kwa sababu unajua miradi hii husimamiwa kule na Wizara ya Fedha, lakini Wizara ina sehemu ya uwakilishi wa kuendeleza ujenzi huu. Hivyo naiomba Wizara kwanza kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tuzipitie changamoto zilizojitokeza katika hatua zile za mwanzoni mpaka tukasita, ili tupate hatua nzuri ya ujenzi ule huko tunakokwenda la mwanzo.

Lakini la pili, kuwe na ushirikishwaji wa ma-*engineers* wa Mamlaka au wa Wizara kwa mkandarasi ambaye atapewa sasa kama ni ile *counter party* ya *staff* wa ile Wizara kupitia ile timu ya ma-*engineers*, kupitia ile timu ya watalaamu ambao wanatokana na Mamlaka husika ili siku ukimaliza ujenzi ule, wale wajenzi wanaondoka basi kuwe kuna watu ambao wamepata taaluma ya

miundombinu ya jengo zima. Sasa tusije tukafika pahala tunampa mkandarasi anajenga lakini watu wetu hawapo, ikitokezea hitlafu ndogo maana yake mpaka tuwaite wao waje waturekebishie. Mhe. Mwenyekiti, sasa niseme tu katika eneo hili tuone ushirikishwaji wa watu wetu unakuwemo kwa sababu miundombinu mingi itapatikana mle maji, umeme na vitu vyengine vidogo vidogo ambavyo ni vitu vya muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna michoro mule *exhibiting drawing* ambayo inaonesha ujenzi mzima wa lile jengo. Sasa baada ya ujenzi tuwaambie wenzetu wale basi waikabidhishe Wizara ili kuona hatua zote ambazo za ujenzi zilizopitiwa na kila kitu kipo wapi ili kuona tunapata uwezo mzuri wa kuja kufanya marekebisho pale inapotokezea hitilafu, kwa sababu mara nyingi *drawing* hizi zinaonesha kila kitu ambacho kimefanyika pale.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nishauri tufanye *review* tena ya lile jengo katika hatua ile ya vifaa sababu pale tulipofikia na muda tuliosita, kuna vifaa vinawezekana ikawa vimeshaanza kuharibika. Kwanza lile jengo lipo karibu na bahari. Hivyo tuone tukifanya *review* tutaona kuna vitu maana yake ile *life time* yake haiwezi kuhimili kukaa wazi kama nondo na vitu vyengine, inawezekana pale tulipofikia basi kuna vitu vikawa vimeharibika. Kwa hivyo tufanye *review* ili tusijekuwa kuna *contingence* kubwa sana huko kila tukiende baada ya ile bajeti tuliyoiwekea kuna *variation* zinakuja tu, kiasi kwamba zinaweza zikaja zikapindukia hata ile *contract price* ambayo tulianza nayo mapema. Kwa hivyo nishauri hili ili tuende vizuri.

Lakini jengine ambalo hili namuomba sana na Mwanasheria Mkuu anisikilize katika utaratibu mpya ambao tunakwenda nao, tufanye *review* mpya ya *mode of payment.* Tulijifunza sana katika eneo la jengo lile na malipo yalivyokwenda, kuna wengine sasa hivi wanaanza kuuliza figure, basi tuone hapa tulipo katika sura nzuri ambayo sisi itatuweka salama, tunazungumzia Mhe. Waziri twende katika mfumo mzuri wa *mode of payment* ili tuweke ile *security wise* kuonekana sasa tunamuambia mjenzi unatakiwa ujenge kwa asilimia 50 lakini malipo tutakulipa kwa asilimia 30 ili yeye atangulie mbele kuliko sisi katika kumlipa, mwisho huko unatengeneza *clause* ya kumalizia hakuna tatizo. Lakini sio ile kuonekana sasa hivi kuna wakandarasi tunawalipa asilimia 70 hawaikamilishi wanakuja kuondoka na fedha tunaingia katika matatizo tena.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mara hii tubadilishe ile *mode of payment,* tuwatangulize mbele wao, maana watengeneze kwa asilimia 70 wewe baadae unamwambia unatengeneza *clause* ya kumlipa asilimia 50, alau tuone tunaweza tukamalizaje tumejifunza sana. Lakini katika pia eneo nyengine ambalo nalo tulizingatie sana, katika utaratibu wa kutengeneza *performance security* ya

huyu mkandarasi ambaye tutakwenda naye, mimi ninaishauri Serikali tuiangalie kwa umakini mkubwa, mara sasa hivi tunaweza kuziandikia benki zikatuangalia baadae zikaleta ripoti benki na huku zishapangana na hawa wakandarasi. Mimi naomba hapa tutengeneze timu za kwenda kufanya ile *Due Diligence*, kuangalia wakija huku watupe ushauri ambao tukiingia naye mkataba basi tunaona tunakuja kwenda vizuri kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu *performance security* hii itakuja kutusaidia kudhibiti fedha ambazo yeye akishindwa kazi tutakwenda kuona tunazipata. Lakini kunako eneo hili Mhe. Mwenyekiti, niombe tu katika kipengele pia chengine cha *security* kile, tuizingatie sana hii *performance security* ili iweze kulinda fedha zetu ambao tunawapa hawa wazabuni. Lakini niende katika eneo ambalo la *retention money*. Kila mikataba yetu mikubwa ina maeneo haya na pesa hizi lazima Mhe. Waziri uangalie.

Sheria hii ipo na *interval* lazima isipindukie asilimia kumi, maana huwezi kuja asilimia kumi na moja. Lakini tusichuke pia kwa mazingira haya tuliyonayo lazima tubakishe pesa kwa kiwango kikubwa ambacho kitakuja kutusaidia yale marekebisho mawili, matatu ambayo huko mbele katika utaratibu wa kutengeneza *guarantee* na *guarantee* yake nitaisemea huko mbele. Lakini tusije tukashuka asilimia kumi, maana ndio *interval* yake huwezi kwenda juu, lakini kushuka unaweza ukashuka. Lakini tuiweke ile kumi yeyewe ili tuzuwie fungu kubwa, tuone tunapokuja kulinda ile *guarantee* ya muda ambao tutakubaliana, fedha hizi ziweze kuja kukidhi katika eneo hilo. Lakini naomba nipendekeze pia katika eneo hili pia ile *guarantee* isipungue miaka mitano. Mhe. Mwenyekiti, tumejifunza sana kwenye maeneo mengi. Serikali ilinunua tu juzi meli kwa jambo zuri tu ambalo azma ya Serikali imetimia, tumeweka *guarantee* sijui ya mwaka mmoja.

Sasa hivi kuna kitu kinaambiwa kikanunuliwe Ujerumani, tungeweka mitatu si angenunua yeye. Sasa hapa nilikuwa nipendekeze tu kwenye eneo hili basi tuweke *guarentee* ya miaka mitano, tuone tunajilinda vipi katika ujenzi ule.(*Makofi*). Lakini Mhe. Mwenyekiti naomba nihamie katika C.2 "Shirika la Bandari". Leo kitabu hichi kimewazungumza na wao katika kuwapitishia bajeti yao. Lakini katika kufuatilia miaka ya fedha karibu miwili hatujaona ule uhalisia wa utekelezaji wa mapato na matumizi ambayo yanakuja kupitishwa na Baraza, kupitia Ripoti za Ukaguzi hawajakaguliwa, ripoti zinakuja karibu miaka miwili ya fedha iliyopita hawajakaguliwa.

Ni sababu zipi ambazo zinapelekea taasisi hii haijakaguliwa. Ninamaanisha haijakagulia na *CAG* akaleta ripoti ambayo wakati fulani ikeshakabidhiwa Barazani Kamati ya *PAC* inakwenda kuifanyia kazi. Ni sababu zipi, tukija tupate ili tuone kile kipimo cha *implementation* ya taasisi hii. Maana tusiwe

tunakwenda tunawapitishia lakini hawakaguliwi kama wanatumia vibaya tuwashauri, kama wanatumia vizuri tuwapongeze eneo lipi tutaona. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja aniambie ni sababu zipi.*(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika kipengele cha C.4 ya Mamlaka ya Usafiri Baharini. Wenzangu wameichangia lakini na hapa Mhe. Waziri toka kuanzishwa kwa Mamlaka hii haijawahi kukaguliwa na kuletwa ripoti yake kwa mujibu wa Sheria tulizotunga wenyewe. Nikuombe Mhe. Waziri utakapokuja uniambie sababu zipi tumetengeneza Mamlaka hii inakusanya fedha na inatumia fedha za Serikali lakini hazijakaguliwa, sababu zipi. Sasa eneo jengine ambao Mhe. Mwenyekiti, nilichangia katika hotuba iliyopita ni eneo la Bodi ya Wakandarasi, na nikapata majibu na nikasema katika utekelezaji wa bajeti 2016/2017 nitapata utekelezaji wake. Lakini suala hili naomba nikuulize tena Mhe. Waziri moja kati ya mambo ambayo niliyachangia nilisema hata ile akaunti kipindi kile ilikuwa haijulikani anaiendesha nani, kwa maana ilikuwa haipo.

Kwa hivyo mara hii nione katika suala la akaunti limefikia wapi na limefunguliwa, lakini pia naomba kupata hesabu za makushano kwa mwaka wa fedha mzima 2016/2017 wamekusanya kiasi gani, lakini hayo makusanyo yenyewe unichambulie kwenye *civil* tumekusanya kiasi gani kwenye *construction* tumekusanya kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki kuchangia sana kwa sababu bajeti hii wamechangia wenzangu wengi na wameyasema mengi, lakini niwaombe tu wenzangu tuipitie kwa umakini bajeti hii basi wenzetu tuwapitishie wende wakafanye kazi ili mambo yaendele vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 98, asilimia 2 tu nimezibakisha si kwa nia ya boti, kwa nia tu Waziri atakapofika hapala hakunipa majawabu kwenye maeneo fulani, nimuulize na anipe niridhike ili twende mbele. Lakini nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Salum Haji naye ameomba dakika 10 ninampa dakika 10, lakini pia Mhe. Shehe Hamad Mattar nampa dakika 5 atafuatiwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu na baadae atafuatia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais na Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano ajitayarishe.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujaalia afya njema na uhai lakini pia nimshukuru Waziri husika wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, nina michango mingi lakini nitajaribu kuchangia kwa ufupi kabisa kidogo kidogo lakini nataka kutoa *data* leo kidogo mwisho kabisa wakati wa michango yangu. Naomba unistahamilie kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Mchango wangu wa kwanza Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni kutoa pongezi, baada ya kuipongeza Wizara basi pia nizipongeze baadhi ya taasisi zao katika maeneo mbali mbali kwa namna ambavyo wameweza kujitahidi katika kusaidia katika taasisi hizi katika hatua iliyokuwepo na pale ambapo tunaelekea. Nataka nitoe pongezi kwa Mkurugenzi wa Bandari kwa namna anavyojitahidi katika utendaji wake wa kazi, mabadiliko mengi tumeyaona katika bandari yetu. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tuna mashaka mengi, mambo ya makontena ilikuwa balaa tukahamia sehemu ya uwanjwa Hoteli ya Bwawani na maeneo mengine, lakini hali sasa hivi alhamdulillahi, tumejenga utaratibu uliokuwa mzuri na mambo yanaenda vizuri. Lakini tulipiga makelele mengi sana hapa, tulikuwa tunapata tabu. Waheshimiwa mambo ya kupekuliwa pekuliwa ovyo pasipo na utaratibu mzuri.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, taasisi imejitahidi mashine zimefika pale na vijana wetu sasa hivi wamefika kupata taaluma kwa kutumia mashine zile katika hali iliyokuwa nzuri, ni jitihada ambazo tunapaswa tuzipongeze. Lakini pia nataka tumpongeze Mkurugenzi wa *airport* namna ambavyo tumeona makelele mengi yalikuwemo, tumepiga makelele kwa muda mrefu hapa, namna ya ubora wa *airpport*, masuala ya *parking*, masuala ya kukaa wageni pamoja na maeneo mengine, hali halisi ya mandhari yenyewe, mambo mengi yamebadilika lazima tujitahidi kupongeza katika hatua ambazo zimechukuliwa pamoja kuwa tunakiri kwamba kuna baadhi ya kasoro ambazo bado zinaonekana zinahitaji kufanyiwa ukarabati wa haraka ambapo wenzangu wamejaribu kuzungumza, suala zima la eneo lile la kusubiria abiria ambao wanataka kusafiri na hususan hali ya hewa inapokuwa ya joto hali mazingira inakuwa si mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini lazma tupongeze kwa jitihada ambazo umezichukua. Lakini naomba pia nipongeze Mkurugenzi wa Shirika la Meli, jitihada tunaziona mambo yanabadilika lakini ndio tunasema kwamba panapo mazuri na kasoro haziachi. Niwaombe kwa yale maeneo ambapo muna kasoro nyingi basi wajaribu kuyafanyia kazi. Ninataka kutoa pongezi hizi kwa kumalizia kwa kumpongeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe naye kwa utendaji wake mzuri wa kazi na hali halisi ambayo inaonekana katika mji wetu katika

kuutunza ili kupata sifa katika Shirika la *UNESCO,* ili mji wetu usije ukapoteza haiba katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi kwa ufupi kabisa nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja tu kwamba katika bajeti ambazo tulikuwa tukipita tulikuwa tukizungumzia sana suala la vituo vya daladala na zaidi tulikuwa tukizungumzia kituo cha daladala cha Michenzani kile, tukafika pahala tukaambiwa Serikali inafanya jitihada ina mipango mizuri cha kuanzisha kituo cha daladala japo cha dharura, watu wengine wakahamia Baraza la Wawakilishi la zamani hivi karibuni tukaambiwa kwamba kituo cha daladala kitahamia Kijangwani pale. Nataka nijue kituo kile kitaanza ujenzi lini ili kuweza kuondosha kero katika mji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia kuna tatizo limejitokeza katika ndugu zetu hawa wanaoanzisha daladala wanapohitaji ruti za magari. Kumekuwa na utaratibu wa ndugu zetu mabaguwani hawa kwamba unapotaka ruti, lazima upitie kwa mabaguwani kwenda kuchukua fomu. Na ile fomu watu wanalipia lakini ubaya wenyewe inasemekana kwamba unapolipia unapewa fomu ambayo ina nembo za Serikali. Sasa najua sijajua taratibu zao zikoje na mimi ninavyofahamu kwa mujibu wa taratibu wa sheria za Serikali kwamba mwenye mamlaka na uwezo wa kukusanya kodi basi ni Taasisi ya Serikali. Hawa mamlaka waliyokuwa nayo ni yepi, kwa sababu kwanza unapewa barua hiyo unalipia, lakini ukishakwenda katika Idara ya Leseni pia unapopata hiyo ruti yenyewe nako pia unalipia. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie sasa hizi nguvu ambazo unawapa mabaguwani wa kuweza kuwatoza watu kodi kabla hata kupata hizo ruti zenyewe katika Taasisi husika.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambao nilikuwa ninataka kulizungumzia kwamba lazima tukiri kwamba nchi yetu sasa hivi imekuwa na mfumko wa watu kupata kuwa na uwezo wa kutumia vyombo vya moto. Sasa *traffic* ya nchi yetu imekuwa kubwa na *jam* zimekuwa zinaongezeka. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, hebu mimi aje anambie tu mipango ya Serikali katika kuhakikisha kwamba wanaweka taa katika maeneo mbali mbali ya *round about* ambazo zimekuwa na matatizo, kuanzia muda wa watu kutoka kazini, zina matatizo nyakati za jioni watu wanapokwenda kufanya mapumziko. Kama maeneo ya Mwanakwerekwe, Amani, yaani watu wanakaa kwenye msongamano muda mrefu, pasipokuwa na sababu. Kwa sababu mtu hajijui nani anakwenda, halafu pia wanasababisha maajali. Nimwambie tu mpango ya Wizara katika kuhakikisha kwamba kuweka *traffic light* katika maeneo yale kwa kipindi hichi kifupi na kwa haraka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mafupi mafupi mimi nataka niwapongeze *back benchers* wenzangu sana wamechangia kwa hamasa kubwa, wameibua mambo mengi na wengine wametangaza mambo makubwa sana ya kutaka Kamati Teule kama matano, sita. Mhe. Mwenyekiti, yote hayo yametokana na uchungu wa Serikali yao. Baada ya kuona kadhia ya maeneo mengi kwamba hayaendi kwamba hajendi vizuri, hiyo ni haki yao wana haki ya kuisemea Serikali hii. Lakini nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati ya nafsi yangu kwamba lazima tukae na kutizama tunatoka wapi, wapi tuko na tunakwenda wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi ambayo tunayapigia kelele sasa hivi, Baraza lililopita tulipiga kelele mpaka vifua vikadata na kasoro hizi huku ndiko zilikotokezea, wenzetu hawa wamerithi ingawa Serikali ni haki yake kurithi yaliyotokea huko nyuma. Lakini tunapaswa tujiulize sababu za msingi, za kusikia suala haya au mambo haya leo hii kuwa tunayapigia kelele kwa kishindo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii ya CCM ina dhamira kubwa sana na ina nia njema na wananchi wake, lakini lazima tukubali kwamba tulifikia wakati Katiba zilitubana. Katiba zilitubana kwa sababu tulifikia pahala tukaingia katika mtego wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na maeneo mengi ambayo yaliharibika na yaliharibiwa kwa makusudi ili kuipaka Serikali yetu matope, ni maeneo ambayo yalishikiliwa na Mawaziri wa upinzani Chama cha CUF. Hayo maeneo ambayo tunapigia kelele Mhe. Mwenyekiti, miundo mbinu ilikuwa na Hamad Masoud, akaja Seif Rashid, tukija Afya kulikuwa na Juma Duni. Sasa ilikuwa hatuwezi kwa mujibu wa Katiba hawa watu kuwaondosha, kazi kubwa ilikuwa inatupata, unaondosha zimwi unaweka shetani. *(Makofi)*

Sasa haya ndio matatizo ambayo Mhe. Mwenyekiti, yaliyotupata kwa sababu kwa akili ya kawaida, kuna baadhi ya mambo unapoyaona wala huwezi kuyafikiria kwamba haya kweli yamekuja mshauri elekezi au haya kweli yamesimamiwa na injinia mwenye akili timamu wenye usomi, hakuna vitu havielekei. Leo tufikie hapa maana yake watu wanataka kuunda Kamati Teule, tulipiga kelele sana *airport* tuliambiwa njia ya ndege iko juu, jengo liko chini, sijui jengo limefika mpaka kwenye barabara. Lakini ni mambo ambayo yalifanywa kwa makusudi, watu walishindwa kuisimamia Serikali hii ili baadae turudi hapa tuilaumu Serikali, na ndio hivi limetokea sasa hivi kwamba watu walituharibia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini hawakutuharibia huko tu mpaka katika masuala ya mikataba kwenye masuala ya kisheria. Ndugu yangu Othman Masoud alifanya mikataba mibovu na sio kama sababu alikuwa hana uwezo, alifanya makusudi kwamba afunge mikataba mibovu Serikali iharibikiwe, ikisha haribikiwa sisi

turudi tuilaumu Serikali yetu. Lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu watu walikuwa hawana dhamira njema ameleta ya kuleta wale watu sasa hivi wako nje. Sasa hivi Serikali hii ya CCM tunayo wenyewe. Ni vyema Mhe. Mwenyekiti, naomba sana wenzangu mapungufu na kasoro zilizojitokeza, tuipitisheni bajeti, tukishaipitisha bajeti tuwaachieni wenzetu wakaondoshe kasoro zilizokuwepo, ili tuisimamishe Serikali hii ifanye matendo yanayostahiki na kumpa imani Mhe. Rais kumaliza zile kero za wananchi wetu katika maeneo mbali mbali. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi na wenzangu naomba waangalie kwa undani kabisa, hawa watu walitengeneza mazingira makubwa. Maeneo nyeti kabisa ya kuisaida Serikali na kuishauri Serikali waliyakamata na wakawa wanatuharibu. Sasa niwaombe Waheshimiwa Mawaziri tuwe makini, sisi saivi CCM ni watawala, hakuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tunapo ushauri, tunapoelekeza, tunapokuambieni, mtusikie mkaondoshe maoza-oza yalikuwepo yaliyobakia. Hawa watu walitengeneza katika maeneo tofauti, kama katika maeneo ya Vitengo vya Sheria, katika maeneo ya manunuzi, katika maeneo ya mainjia ili kutengeneza mazingira ya kugharibu nchi, na ndio matokeo yake sasa hivi tunaamua kuilamu Serikali, kumbe tuliharibiwa yaani tulipigwa kwa bakora yetu. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe wenzangu, najua sana mapungufu yote yaliyojitokeza, sote tunajua lakini aliharibu nani, kwa misingi gani. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba ninawaomba Mawaziri tutajenga imani ya kupitisha bajeti, lakini tutakuja kuwahoji mwakani kwa yale mapungufu ambayo sisi tunahitaji tuwape fedha wakayamalize. Si vyema leo tukafika pahala kwamba tuzuie majengo, ushajenga hatua iliyokuwepo ukiacha ndio tunaharibikiwa. Mhe. Mwenyekiti, tuwape imani wamalize ili wakimaliza baadae tuje tuhoji kumekwama nini. Mhe. Mwnyekiti, hapa viroja vilikuwa vikubwa kipindi kilichopita, watu waliajiri wafanyakazi hapa zikaundwa kamati zikenda taasisi husika mtu kuandika jina lake hajui, lakini walifanya wao kwa makusudi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Mwenyekiti, namalizia na namalizia kwa uchungu na kuwaomba wenzangu kabisa, na namwambia Mhe. Waziri kwamba bado makando kando, makobe waliojipaka rangi wamebakia katika Mawiza yetu na wanatuharibikia Serikali na tunazungumza kwa uchungu tuondosheni watu wasioitakia mema Serikali ya CCM tufanye kazi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na wewe bado una mtu ambaye aliletwa pale kwa misingi ya kuchunguza Wizara. Msaidizi wako siye. Hawa watu

hawatufai, hawa watu hawaitakii mema serikali hii. Tunakupitishieni bajeti na nina imani mabuti hayotokuwepo na kama yatakuwepo ya wastani. Lakini tunakupeni bajeti mkaisaidi Serikali yetu ya CCM na kama kuna makando kando, kuna makobe yalipaka rangi tuondosheeni ili serikali yetu iweze kusimama. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii watu wameteseka, watu wamepata tabu na hiyo ndio misingi ya serikali yetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakusikia na ninakufahamu na najali muda wako, lakini haya ninayoyazungumza nakisaidia kiti chako. Namwaga jasho jingi wakati wa amani ili tuje tumwage jasho dogo, wakati vita utakapokuja kama Kamati kuisaidia serikali yetu, kuisaidia bajeti hii ipite kwa wepesi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja kwa asilimia 100, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani nakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji (Kirova) Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani pia ni Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Baraza hili.

Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa dakika tano, ziwe dakika tano za kweli kweli kama ulivyoziomba na nitampisha Mhe. Mwanasheria Mkuu akifuatiwa na Mhe. Waziri Mohamed Aboud.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya dakika tano nitazitumia.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii na kwa kitabu chake hichi, lakini kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii. Naiunga mkono hotuba hii na bajeti hii asilimia mia juu ya mia, kwanza natanguliza hilo ili nisije nikasahau.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia atakapokuja kwanza naomba aniwekee sawa na atuwewekee sawa sote pamoja na wenzangu. Katika kitabu hichi cha hotuba ameomba jumla ya shilingi bilioni mia mbili na kumi na nane, milioni mia nane na ishirini, mia mbili na mbili elfu (218,820,202,000). Lakini katika kitabu hichi cha vifungu kinaonesha tofauti, kinaomba bilioni mia mbili kumi na sita, mia nane na ishirini mia mbili na mbili elfu (216,820,202,000), ni ipi iliyo sahihi atakapokuja naomba atuwekee sawa hapa.

Baada ya hapo naomba niende moja kwa moja, niwapongeze Wizara hii na taasisi zake mbali mbali ambazo zimeonesha jinsi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016 ilivyofanywa. Kwa kweli imetumia busara nyingi sana katika Idara zake mbali mbali ikiwemo Shirika la Bandari, Shirika la Meli na nyenginezo, wizara imajitahidi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli imeweza kushughuulikia usalama wa meli zetu, wa barabarani na kuona kwamba wananchi huduma zilizo bora. Vile vile niwapongeze pale walipokuwa wamejitahidi katika ukusanyaji wa mapato kwa kufikia asilimia 70 kwa Shirika la Bandari. Humu ni mwahali ambamo tunategemea kwamba ni pato la nchi katika sehemu ya bandari. Kwa hivyo kama mwezi wa Machi wamefikia asilimia 70, nadhani hata ikifikia Juni watakuwa wamefika ama asilimia 100 au 90.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee kuwapongeza Shirika la Bandari kwa kazi ya utanuzi wa bandari ya Wete. Nilifika mwenyewe nikaona hali inayoendelea na wanaendelea na juhudi hiyo kuona kwamba vyombo vinavyofika pale vinaendelea kupata huduma vizuri na kwa wakati wowote. Lakini ninalishauri Shirika la Bandari kwa mambo mawili. Pale Wete waendelee sasa kama walivyoonesha kwenye kitabu chake cha hotuba kwamba wataweza kujenga, lakini sasa wafanye kwa vitendo, badala ya kila siku kuona kwamba kitabu hichi kinaonesha kama watajenga gati ya Wete. Tunaomba kwanza tuiyone. Mkoa wa Kaskazini ndio Mkoa ambao unaidadi kubwa ya watu kwa kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nalishauri Shirika la Bandari, tuna meli yetu ya MV. Mapinduzi ambayo kuwa ni vitu ambavyo vinategemeana hawa. Bandari ya Unguja panahitaji sehemu ambayo meli yetu itaweza kuteremsha mizigo na kupakia mizigo ili meli yetu iweze kufanya biashara vizuri , kwani wamepanga sana katika kuona kwamba meli inaingiza mapato, lakini kwa sasa inashindikana. Kwa upande wa Pemba afadhali, inapofika kule maji kama ni mazuri inafungua lango lile na kuweza kuteremsha na kupakia mizigo kwa vizuri sana. Kwa hivyo nashauri sana kama vile mwenzetu Said Bakharesa alivyoweza kujenga eneo la kushushia meli zake na sisi tuone namna gani badala ya kuikata meli hiyo, basi tutengeneze sehemu ambayo itakayoweza kufungua na kufunga, kupakia mizigo meli ya MV. Mapinduzi II bila usumbufu wowote ulivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nilipongeze Shirika la Meli kwa juhudi zake ambazo zinaendelea kuitunza meli yetu, lakini kuna matatizo kwenye meli yetu ya MV. Mapinduzi ni meli kubwa na ya kisasa, lakini inahitaji huduma za usafi. Mara nyingi sana mimi ni meli ambayo huwa nasafiria na nimeona changamoto wakati wa usafi meli inapofika na kurudi, wafanyakazi waliyokuwemo ni kidogo sana kiasi ambacho kuwa wanalazimika kubeba mzigo mkubwa wale

wafanyakazi waliyokuwemo ndani ya meli. Nawaomba sana Shirika la Meli kupitia Mkurugenzi wake waone jinsi gani wataweza kuwafuatilia wafanyakazi hawa meli inapofika Pemba iweze kufanyiwa usafi kwa watu maalum, hata kama ni kuwaajiri watu wa muda na inapofika Unguja pia vile vile iweze kufanyiwa usafi. Kwa sababu abiria hawawezi kuingia melini kama meli haijafanyiwa usafi, hilo naliomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilipongeze Shirika la Meli pale ambapo tuliposhirikiana katika kuondoa ile kero ya tiketi za ulanguzi pale bandari. Nimpongeze Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Shirika la Meli baada ya kumpelekea tatizo hili, kuona kwamba wanachi wanateseka kufika pale bandarini tiketi ya bei nafuu zimekwisha na zote zimo mikononi na wao nikawafika nikawaeleza tatizo hili, wakaweza kulisimamia na baadae hadi meli inasafiri unaweza ukaikuta tiketi za bei zile za serikali ambazo imezipanga za chini na ukaweza kupata, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika "Programu ya Usimamizi wa Usafirishaji". Katika kikao kama hichi mwaka jana nilieleza juu ya suala la usalama barabarani. Barabara zetu ni kubwa sasa hivi lakini tunazitumia ovyo. Nilishauri kwamba na sisi tuweke katika ni siku maalum ya usalama barabarani, kama vile wenzetu wa Tanzania Bara kwa Jeshi la Polisi inavyofanya. Bado sijakiona kitendo kama hicho ni muhimu sana, watu wanakwenda ovyo, ajali nyengine zinatokea kizembe sana. Kwa hivyo tunaweza kukinga badala ya kutibu. Naomba sana na nalishauri hili jambo liendelee.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia vile vile suala la ukarabati wa ujenzi wa barabara. Mwaka jana katika hotuba kama hii nilichangia na kueleza kwamba Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein aliweka ahadi katika Baraza ya Finya Kicha, na tukakumbushia katika Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka uliopita haikutekelezwa na mwaka huu haijatekelezwa wala sijaiona katika kipaumbele ambacho kuwa kimejieleza. Nawashauri sana na naomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni vipi njia hii itaweza kutekelezwa. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wana hamu kuona kwamba nao wanapita katika sehemu ambazo kuwa zinapitika na vyombo vyao na kuweza kupeleka mazao katika sehemu zinazohusika bila ya usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, niliende katika suala zima kuona kwamba mwaka jana nilikumbushia na mwaka huu nakumbushia tena, kuwa wananchi wangu ambao wameharibiwa vipando vyao katika ujenzi wa barabara ya Wete/Konde na Mzambarau/Karim na Mapopwe. Wananchi hawa bado mpaka leo wana malalamiko na sisi tunaendelea kufanya shughuli za barabara na huko yatakuja

mengine. Kwa hivyo ni mzigo kwa serikali. Hebu tuone basi kwamba jinsi gani tutaweza kulitatua tatizo hili la kulipa fidia, isiwe kila siku linarejewa rejewa.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali hapo kwa kupitia hotuba hii basi ipunguze sehemu ya fungu ambalo kuwa litaweza kuwasaidia ijapokuwa shilingi milioni mia mbili ziwekwe pembeni kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi hawa ambao wameathirika na ujenzi ule wa barabara. Bado ni kilio cha wananchi wananituma na wao wanataka kujua ni lini fedha zao watazipata kwa mazao na baadhi ya mali zao zilizoathirika. Fedha hiyo naiombe sana itoke katika mkopo wa maendeleo uliombwa hapa au kwenye fungu la Shirika. Mchango huu ambao utaweza kusaidia kuona kwamba wanaweza kupata fidia hii bila ya usumbufu wowote. Ni vyema sana na naomba sana Mhe. Mwenyekiti, fedha hii ipatikane kwa sababu katika kitabu hichi sijaona namna gani fidia ilivyopewa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisiupoteze muda wako niliouchukua, yangu ni hayo machache Mhe. Waziri atakapokuja atusaidia ili wananchi wapate kujua barabara ya Finya/Kicha itajengwa lini na hii hesabu nayo pia tuwaekee sawa na usalama barabarani vipi utaweza kuutekeleza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijampisha Mwanasheria Mkuu naomba niwatangazie kuwa Mheshimiwa yeyote ambaye amechukua funguo pale mlangoni kimakosa, labda amechukua mbili tunaomba aji-*search*, kuna mwenyewe hapo nje anazisubiri funguo zake.

Mhe. Mwanasheria Mkuu tuendelee.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii angalau kusema machache sana kwenye hoja hii ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Wizara hii Balozi Ali Abeid Karume pamoja na Naibu Waziri, pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya kwa kipindi hichi kifupi tokea wakabidhiwe Wizara hii.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ni kubwa na imeongezewa majukumu mengine, lakini niwahakikishie kuwa kazi zao wanazozifanya ni nzuri sana na tunawaomba waendelee na kasi hiyo hiyo ambayo wameanza nayo, ili wazidi kuwawekea matumaini wananchi wetu. Maana sekta hii ndio sekta muhimu, ujenzi upo hapa, mawasiliano yapo hapa na usafirishaji upo hapo. Hayo ndio

mambo matatu makubwa na muhimu ya nchi na yote haya yapo mikononi mwao. Kwa hivyo kwa dhati kabisa niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili nichukue fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia dhamira yake ya kuwahakikishia wananchi wa Zanzibar kuwa wanapata usafiri wa uhakika, wenye usalama wao pamoja na mizigo yao. Pamoja na yote ambayo tumeyasema kuhusiana na Meli ya MV. Mapinduzi II, lakini Mhe. Rais hakuvunjika moyo na kwenye bajeti hii ameahidi meli nyengine mpya. Ni wajibu wetu sote kuungana mkono na Mhe. Rais katika kumpongeza na kumuhakikishia kuwa bajeti hii tutaipitisha ili ile dhamira ambayo anayo ya kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanapata usafiri wa uhakika basi itimie. Sitaki kusema mengi kuhusiana na ununuzi wa meli, lakini wengi tunajua yaliyotokea na ndio sababu ambayo imepelekea Mhe. Rais kuamua kwamba sasa umefika wakati tuwe na meli mpya.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mara ya mwisho kuwa na meli mpya nchi hii ilikuwa ni miaka ya mwisho ya sabini, lakini viongozi wengi wamepita mpaka alipokuja yeye ndio akaamua sasa kununua meli hiyo mpya. Kwa dhati kabisa Mhe. Rais amefanya hivyo kwa sababu wale ambao waliokabidhiwa sekta hii, miongoni mwetu wafanyabiashara wachache waliokabidhiwa sekta hii baada ya kuwatumikia wananchi, wao waliweka faida na kipato mbele kuliko usalama wa raia na mizigo yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa yaliyotokea mengi sina haja ya kuyataja pamoja na yote ambayo yametokea, lakini tumpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Rais kama amekomboa wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba, kama leo wanaweza wakasafiri wakawa wametulia ndani ya chombo ambacho kinawahakikishia usalama wao. Kwa hivyo ninampongeza sana kwa dhati kabisa Mhe. Rais na nimuombe sana Mhe. Waziri kama asimamie vizuri ununuzi wa meli hizi mbili mpya ambazo serikali imeahidi kuzinunua na ninaamini kama atasimamia vizuri yeye pamoja na watendaji wake wote tutafanikiwa katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, pili nichukue fursa hii kuzungumzia suala ambalo Wajumbe wengi wamelizungumzia juu ya usimamizi wa mikataba *(contract management),* limekuwa ni suala ambalo Wajumbe wanalizungumzia na limekuwa linajirudia kila baada ya muda. Nilizungumza wakati wakati tunachangia hoja ya hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na nikasema kwamba nchi yetu kwenye mambo ya manunuzi inaongozwa na Sheria ya Ununuzi Nam. 9 ya mwaka 2005, ndio Sheria ambayo inaongoza ununuzi wote

wa serikali na ndio Sheria ambayo inayoongoza uondoshaji wote wa mali za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Sheria ile zimetungwa Kanuni za mwaka 2006. Kanuni hizi kimsingi ndio zimeweka masharti yote yanayotakiwa kuwemo ndani ya mikataba. Hakuna mkataba wowote unaotengenezwa wa serikali unaotakiwa kwenda kinyume na masharti ambayo yameelezwa ndani ya Sheria Nam. 9 ya mwaka 2005 na ndani ya Kanuni zake zinazotokana na Sheria hiyo. Lakini pia tukisoma Kanuni hiyo imeeleza aina tatu za mikataba ambayo serikali inatakiwa kuingia. Moja nilisema juzi na naomba nirudie tena kama hivi:-

1) Mikataba ya ujenzi ambayo serikali inatakiwa iingie na mikataba hii ya ujenzi pia imegawika kwenye sehemu tatu.

- Sehemu moja ni *(lump sum contract)*, ni ile mikataba ambayo mnakubaliana kwa kima maalum cha fedha kama tujengee na kima hichi ndio utatumalizia ujenzi wetu.
- Sehemu ya Pili *(schedule of rate contract*), hii ni mikataba ambayo inakwendana na ile *bill of quantity* ambayo tunakubaliana.
- Kuna mikataba ambayo inaingia ina *special feature* kama kuna maeneo maalum tunakubaliana na tunalipana kutokana na maeneo hayo.

2) Mhe. Mwenyekiti, pia kuna mikataba mengine nayo ni Mikataba ya bidhaa na huduma, sote tunanunua magari, tunanunua makompyuta, tunanunua meli, yote hayo ni mikataba ambayo inaingia katika sehemu hii.

3) Kuna Mikataba ya Ushauri (*consultancy)*, tunapotaka watu waje watushauri kwenye maeneo maalum ambayo utaalamu wetu siyo mkubwa kwenye maeneo hayo, basi tunaingia kwenye mikataba ya *consultancy* na tunawaajiri washauri ili waje watushauri kwenye maeneo hayo muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria hiyo haikuacha tu bila ya kuzungumzia masharti ambayo na mkandarasi anatakiwa awe nayo.

1) Masharti ambayo anatakiwa awe nayo ni lazima awe na ujuzi wa fani ambayo anayoiombea. Huwezi ukaingia mkataba na mtu ambaye hana fani, unataka kuingia kwenye mkataba wa ujenzi unakwenda kumchukua mtu mshona viatu, Sheria inakataza. Sheria inasema unapotaka kuingia mkataba wa ujenzi basi yule mkandarasi awe ana sifa za ukandarasi, hayo ndio masharti ya Sheria.

2) Sheria inasema mkandarasi mwenyewe awe anazo sifa za kuingia kwenye mkataba. Sifa hizi za mkataba zimetajwa na Sheria ya Mkataba Sura ya 149, anatakiwa mtu awe na sifa ambazo zimetajwa ndani ya Sheria ile.

3) Jengine ambalo nalo hili ni muhimu mkandarasi anatakiwa kwanza awe ana uwezo wa kifedha wa kuifanya ile kazi.

4) Lakini pia awe ana vitendea kazi vya kazi ambayo anataka kuifanyia kazi basi ahakikishe kama anavyo vitendea kazi vya kazi ile.

5) Pia ahakikishe kuwa anapofanya kazi ile basi analinda zile *facilities* ambazo zimo katika lile eneo ambalo analifanyia kazi.

Nimesikia wengi wa Waheshimiwa Wajumbe hapa wanasema wakandarasi wetu wengi wanaposimamia mikataba hii wanaharibu miundombinu ambayo ipo. Sheria na Kanuni inamtaka mkandarasi ahifadhi yale maeneo ambayo yupo na akiharibu Sheria inamtaka yeye mwenyewe atengeneze na kwa gharama zake. Sasa yote haya Mhe. Mwenyekiti, yameelezwa lakini zaidi mkandarasi anatakiwa atowe *performance guarantee,* atowe dhamana ya asilimia kumi mpaka ishirini ya bei ya ule mkataba ambao anatakiwa aingie nao, atowe *performance guarantee* ya asilimia kumi hadi ishirini.

Lakini pia anatakiwa pia aweke *insurance* ya ile kazi ambayo anatakiwa aifanye. Mhe. Mwenyekiti, yote haya yameandikwa ndani ya Sheria zetu. Tatizo letu si sheria wala si mikataba. Tatizo linalotusibu ni usimamizi wa dhati. Hilo ndio tatizo ambalo linatusibu kama miongoni mwetu hatuna udhati wa kusimamia hii mikataba ambayo tunaingia. Sote tuna haraka ya kutika saini mikataba. Mimi pale nipo Ofisini ni shahidi. Mhe. Mwenyekiti, utapigiwa simu si chini ya kumi, mkataba huo muhimu, mkandarasi anataka kusafiri, tumechelewa, *AG* unatucheleweshe yote hayo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini unapotia saini tu ule mkataba basi ule udhati wa usimamizi haupo na hilo lazima tukubaliane kama baadhi yetu hawana udhati wa kusimamia shughuli hizi za Serikali, na ndio maana matatizo haya mengi yanatukuta. Mkataba umeingia na mkandarasi yuko Kibuteni, wewe unakaa mjini, hupiti, humuulizi, huwendi, humuulizi *contract manager*, humuuzi *project manager,* sote tunakaa maofisini tukidhani kama mkandarasi atafanya shughuli zake. Hawezi kufanya hata siku moja lakini baada ya yote hayo analeta gharama anasema nishafika kozi ya pili, sasa nilipe na wewe unamlipa bila ya kwenda kutizama kumbe ndio kwanza hata huo msingi hakumaliza, yote haya yametokea na yote haya yamefanyika ni udhati wa usimamizi wa shughuli zetu hizi ambazo tumepewa wala mikataba haina tatizo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mikataba yenyewe hakuna jipya ambalo tunatengeneza, wote Waheshimiwa Wajumbe wanajua kama mikataba ya ujenzi inaongozwa na mikataba maalum, kuna *standard format* ya mikataba hii, unapotaka kununua mikataba ya ununuzi kuna *format* yake ya mikataba yote hayo yapo. Lakini kama hatujakubaliana kwa dhati sote humu ndani maana na sisi nimesema juzi na narudia na sisi humu ndani Mhe. Mwenyekiti, tuna *role* kubwa ya kusimamia yote haya yana yanayotendeka Serikalini, kwa sababu sisi ndio tunayoidhinisha fedha kwa Wizara na kila miezi mitatu tunapita kwenye Wizara zote.(*Makofi*).

Sasa *over site role* ile inaanza kwetu sisi, sisi ndio wasimamizi wa kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, wa kuhakikisha kama tunahoji. Wewe umesema unataka kujenga barabara kilomita ishirini, umeshalipa bilioni 10 mbona haikufika kilomita 5 imekuaje. Lazima haya tuhoji kwa sababu sisi ndio tunaoidhinisha hizi fedha lakini kama hatuhoji tukasubiri tuje kupiga mabuti kwenye bajeti, hatutokuwa tumeisaida Serikali, hatutokuwa tumeisaidia Wizara wala hatutokuwa tumewasaidia wananchi ambao ndio wametuleta humu ndani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa niwaomba kabisa Waheshimiwa Wajumbe kama tushirikiane na tuzinduwane katika kuhakikisha kama tuna udhati na umakini katika kusimamia majukumu haya ambayo tumepewa. Kinyume na hivyo Mhe. Mwenyekiti, tutazungumza hapa kila siku haya lakini sisi ambao ndio wasimamizi wa watendaji wetu hawa, niwaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wote kama tushirikiane kwa dhati katika kuhakikisha tunawasimamia watendaji wetu wote kwenye kazi zote ambazo wanazozifanya na hasa kwenye kazi hizi kubwa ambazo ndizo fedha nyingi za Serikali zinatumika kwenye usimamizi wa mikataba. Maana ndio Serikali inatumia fedha nyingi kwenye maeneo hayo. Sasa kwa dhati kabisa lazima tuwakumbushe na tuwasimamie watendaji wetu, tusikubali watuletee taarifa bila ya sisi wenyewe ku-*verify*, bila ya sisi wenyewe kuhakikisha kama tumefuatilia na tumejiridhisha na kujitosheleza na taarifa zilizomo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba niungane na wote ambao wameunga mkono hoja hii na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud na Mhe. Naibu Waziri Mohamed Ahmada ajitayarishe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Aidha

nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpomgeza sana Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Balozi Ali Karume kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake lakini yeye akishirikiana na Naibu Waziri na watendaji wote kwa kufanya kazi nzuri katika Wizara hii kubwa nzito na ngumu, ni wajibu wetu kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mimi nizungumzie kidogo kuhusu suala la meli kwa nini tumenunua meli serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kijografia Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba tumezungukwa na bahari kutokana na kuzungukwa huko na kihistoria kwa miaka mingi hata kabla ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, Serikali kulikuwa na utaratibu wa kuwa na meli kwa ajili ya kutoa huduma kati ya visiwa vyetu viwili hivi pamoja na Tanzania Bara na nchi jirani. Kwa hivyo ni jambo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu, limefanyika hivyo kwa dhamira njema ya kuhakikisha wananchi wetu wanaondokana na usumbufu wa usafiri katika sekta hii ya bahari.

Lakini pia katika siku za karibuni kutokana na sekta binafsi kuwa na meli zilizokuwa chakavu na ukongwe kwa baadhi ya makampuni, yakasababisha majanga ya kuzama kwa meli hizo, likatokea tatizo kubwa la kupoteza maisha ya watu na mali zao. Hivyo Serikali ikaona ichukue hatua katika hali ngumu ya kununua meli ya MV Mapinduzi II. Na ilifanya vile kwa kusikiliza kilio cha Wajumbe wakati huo waliokuwa katika Baraza hili tukufu pamoja na wananchi waliomba Serikali ili tupate meli mpya ya kisasa, na ndio maana Serikali ikanunua meli mpya ya kisasa.

Baada ya matukio mbali mbali sote tunakumbuka katika mwezi wa tano mwaka 2009 *MV Fatihi* ilizama pale bandarini, ilisababisha kupoteza maisha ya watu pamoja na mali na mizigo, *MV Spice Islanders* mwezi wa Novemba mwaka 2011 nayo ilizama katika bahari ya Nungwi na ilisababisha upotevu mkubwa wa maisha ya watu wetu, zaidi ya watu 183 walipoteza maisha katika ajali, mizigo na vitu mbali mbali vya wananchi.

Vile vile katika Julai 2012, *MV Skagit* kwenye kisiwa cha Chumbe ilizama, zaidi ya watu 12 walipoteza maisha na mali zao. Aidha meli ya *New Happy* na vyombo vyengine vidogo vidogo vilipata matatizo. Kutokana na hali hiyo ambayo wananchi wetu walipoteza maisha, walipoteza mali zao, Serikali kwa makusudi iliamua kutafuta ukombozi kwa kununua meli mpya ya kisasa, meli nzuri inayo sifa zote kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu lakini kwa ajili pia ya kurahisisha usafiri kati ya Unguja na Pemba na Unguja na Dar es Salaam.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe meli ile ni ya kisasa ni tofauti kabisa na maneno mengi ambayo watu wanasema, wako waliosema mtumba, wako waliosema imechakaa na kadhalika. Lakini ile meli ni mpya ya kisasa na ilifuata taratibu zote za *tender*. Kwa maana ilikuwa ni *Internationa Tender* ile iliyotangazwa na vigezo vyote viliwekwa na ndio maana ikanunuliwa kwa utaratibu wa *tender* ya wazi, kwa dhamira ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata usafiri mwema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Serikali ilifanya vile kwa imani na kwa usikivu wa mahitaji ya wananchi na ina nia ya kuimarisha Shirika letu la Meli kuwa na meli zaidi za mizigo, meli za abiria, meli ya mafuta ili kujirudishia sifa ya Zanzibar katika kutoa huduma hizo, na tutaendelea kufanya hivyo kwa kujiimarisha kiuchumi kupitia sekta hiyo, lakini kwa kuzidi kutoa huduma kwa wananchi wetu ili kuepuka na matatizo ambayo yanaweza kujitokeza hasa kama nilivyokwishayaeleza.

Lakini pia Serikali ilichukua hatua ya ziada ya kuimarisha *ZMA* ili kudhibiti usalama wa baharini na sisi sote hapa ndani tuliokuwepo katika mwaka 2013 tulipitisha Sheria ili kudhibiti meli chakavu, meli mbovu ambazo haziwezi kutoa huduma bora kwa wananchi wetu. Katika kufanya hivyo ilibidi Serikali ijitolee kuwa na meli ya mfano katika kufanya shughuli hizi. Kwa hivyo ninawahakikishia wananchi hiyo ndio iliyokuwa dhamira ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli meli ile tumenunua kwa milioni 33 pesa za Kimarekani. Lakini lazima tuelewe kwamba meli ile inabeba abiria 1,200, inabeba zaidi ya tani 200 za mizigo na meli ina sifa zote za kisasa zikiwemo *out of drive*, ile meli ni kama ndege ikiwashwa ile ikiwekwa inaondoka. Haiyumbi katika mkondo wala hailali ubavu ubavu kama meli nyengine, ina eneo inapotokea wakati wa dharura, *helicopter* inaweze kutua mule ili kutoa msaada. Ni meli iliyoundwa kwa kuzingatia sifa zote. Kwa msingi huu, "Ukitaka vya mvunguni lazima uiname", ndio maana ikawa na thamani kubwa na mtu yeyote anayo haki ya kuangalia kwa kuifanyia tathmini meli iko pale na ulizieni kwa mitandao yote mtaona kwamba meli imekwenda kwa thamani yake (*value for money)*. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hizi meli nyengine za binafsi mnazoziona zinazo *operate* hapa hazitoki moja kwa moja zinakotoka huko, zinabebwa na meli nyengine mpaka kufika hapa. Hii imetoka kutoka Korea mpaka Zanzibar ili kuonesha mkondo wowote meli ile inaweza kupita na kwa usalama zaidi na humo ilimokuwa ikipita na ikisimama kwa mujibu wa manahodha wetu wakisema inaposimama wanapokuja wale wataalamu wa mambo ya meli, waliona umahiri na ubingwa uliotengezewa meli ile na usasa wake. Kwa hivyo ni sisi

wenyewe sasa tubadilike tukenda kisasa kutokana na hali halisi ya meli ile. Kwa hivyo ilinunuliwa kwa utaratibu wa *tender* ya wazi na kufuata taratibu zote bila ya kuwa na shaka yoyote, Serikali ilifanya hivyo kwa nia njema.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na dhamira ya Serikali ni kuendeleza kuwa na meli zaidi. Mwanasheria Mkuu ameeleza hapa lakini mpango wetu ni kuwa na Shirika kubwa zaidi la meli, kuwa na meli nyingi zitowe huduma bora, tuwe na meli za mizigo na meli za abiria na kadhalika, na huko mbele hata watu wakenda Hijja itakuwa hatuna haja sana ya kutafuta sana ndege, meli yetu inakwenda ile na viti vya kisasa na kila kitu unachokitaka. Kwa hivyo mimi naamini uamuzi ule wa Serikali ulikuwa mzuri sana na unatusaidia sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vile ilikuwa suala moja naomba nilisemee na nina hakika Mhe. Waziri alilisemea zaidi ni suala la barabara hii ya Mwanakwerekwe/Fuoni. Moja katika barabara nzuri za Zanzibar ni barabara hii ya Mwanakwerekwe/Fuoni. Barabara hii ni kweli ya kilomita nne lakini ni ya pande mbili (*double current)* na ina upana wa mita 14, kwa maana upande mmoja mita saba na upande mwengine mita saba. Kwa msingi huo ni sawa na barabara yenye upana wa mita saba ya kilomita nane, maana ni nne mara mbili. Kwa msingi huo thamani iliyojengewa barabara ile ni Bilioni 8, siyo bilioni 600 kama inavyosemwa *(Makofi)*

Kwa hivyo ukilinganisha thamani halisi ya ujenzi ule wa barabara na *standard* ile ya barabara, utaona Wizara imesimamia vizuri, imefanya kazi vizuri na pia *contractor* naye amefanya kazi nzuri. Hivyo waliofanya mazuri lazima tuwapongeze, kazi imefanyika vizuri pale na hali imekwenda vizuri. Ninaamini barabara ile inatusaidia sana na naamini Mhe. Mjumbe ataelewa kwamba sion Bilioni 600 ni Bilioni 8 ndio zilizojenga barabara ile.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na suala la kuimarisha kiwanja chetu cha ndege. Mhe. Mwenyekiti, hatukandamizi fedha pale, pale tunawekeza kwa maslahi ya Zanzibar. *Terminal II* inayojengwa ni kioo cha nchi yetu. Tunapojenga *airport* ile ya kisasa na Zanzibar inategemea utalii ni jambo muhimu kufanya kitu hicho. Kwa hivyo uamuzi wa Wizara kufikiria na kuomba fedha kwa ajili ya kuendeleza suala zima la kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege ni jambo la msingi sana. Maana Kiwanja cha Ndege kile, ndicho chanzo cha kuvutia utalii na sisi Zanzibar tunategemea sana utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naamini Mhe. Waziri atatoa ufafanuzi wa kina kuhusu suala la ujenzi wa *Airport Terminal II*, lakini Serikali yetu ilifanya makusudii kuchukua hatua muafaka ili kuimarisha Kiwanja cha Ndege kitakachokidhi haja yetu ya ndani na kwa miaka mingi mbele ijayo kiweze

kutumika, na kiweze kuwa na sifa katika dunia watu wapokuja waone upo uwanja wa ndege mzuri. Sote tunasafiri tunaona viwanja vya ndege vya wenzetu. Kwa hivyo hatuna budi katika dunia hii na sisi tukawa na Kiwanja cha Ndege kizuri. Na ndio imani ya Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein tuwe na kiwanja cha ndege kizuri, cha kisasa, bora kitakachotoa huduma bora na jambo hili analisimamia kwa dhati ili liwezekane na likamilike. Mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi kwamba kiwanja chetu cha ndege kitamalizika, tutakuwa kiwanja cha ndege bora na huduma bora zitapatikana kutoka hapa.(*Makofi*).

Kwa hivyo ningewaomba Wahesimiwa Wajumbe tumuunge mkono Mhe. Waziri kwa kumuwezesha bajeti yake ipite ili aweze kusimamia majukumu yake ipasavyo, ameonesha mfano mzuri sana wakutekeleza wajibu wake, yeye na Naibu Waziri na watendaji tuwaombee dua wazidi kuwa na imani ya kufanya kazi ya kuwahudumia nchi yetu na sisi mfano mzuri ni kuwaunga mkono kupitisha bajeti hii vizuri na bila kuwapigia buti ipite kwa salama na amani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na namshukuru sana na mimi naendelea tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana leo katika kuipitisha bajeti ya Wizara muhimu na nyeti sana katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar, na Mwenyezi Mungu akitujaalia tunaipitisha bajeti hii katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. (*Makofi*).

Nina imani kubwa sana kwa nia ghalisi zinazotoka ndani ya sakafu ya mioyo yetu, sisi Wizara kupitia Waziri wetu wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na mimi nikiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na watendaji wetu wote wakuu tunajua dhima kubwa aliyotupa Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein katika kusimamia Wizara hii. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wangu, amekuwa amenifunza mambo mengi, kisiasa, kidiplomasia na kuweza kunifundisha kitu uvumilivu na kufanya kazi kwa uwajibikaji mkubwa sana.(*Makofi*).

Pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye amekuwa muhimili mkubwa sana katika Wizara yetu kwa kutupa miongozo, ushauri, nasaha na maelekezo kila wakati kwa kuwa anajua umuhimu wa wizara yetu hii katika sekta ya maendeleo na uchumi wa nchi yetu. Vile vile nimshukuru Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa ushauri wake na maelekezo yake anayokuwa anatupa kila wakati katika kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa uaminifu, na uzalendo wa hali ya juu sana na uwajibikaji mkubwa sana katika kuitumikia Wizara hii ambayo nyote mnajua ndio Wizara yenye bajeti kubwa kuliko wizara zote. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nichukue nafasi hii kuanza kujibu baadhi ya hoja za Wajumbe ambao wamechangia katika bajeti yetu hii kwa kipindi cha tokea jana mpaka hii leo, na wakati nakuja huku kulikuwa kunaendelea kutolewa michango. Kwa hivyo mimi niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameonesha namna gani walivyokuwa na moyo wa kuwahudumia wananchi na vile vile kuipenda serikali yao na nchi yao ya Zanzibar, kwa kutushauri, kutuelekeza na baadhi ya wakati kutuhadharisha na vile vile kutugomba pale ambapo wanaona kwamba tunahitaji kugombeka.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na hoja ambazo nitachangia mimi ni kuhusu Idara ya Leseni. Waheshimiwa wengi tu waliulizia mambo tofauti katika Idara hii ya Leseni na Usafirishaji. Mhe. Mwenyekiti, wapo waliotaka kujua vituo vya daladala, wapo waliotaka kujua kuhusu madereva wetu, wapo waliotaka kujua umri wa vijana ambao wanaendesha vyombo hivi vya moto.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua katika Idara ya Usafiri na Leseni wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya 2003. Sheria ile imeanisha kila kitu, imeanisha miongozo nani anatakiwa apewe leseni, nani anatakiwa aendeshe gari aina gani, na nani anatakiwa vile vile apewe adhabu gani wakati ambapo atafanya makosa. Kwa ufupi tu nataka kuwaarifu Baraza lako tukufu ili kwamba katika Idara ya Leseni umri hasa niliozungumza suala la vijana wale wadogo. Vijana wa miaka 16 sisi tunapowapa leseni, tunawapa leseni "M", kwa mujibu wa Sheria Nam.7 ya 2003 kwa kuendesha chombo cha aina ya "*moped"* tu peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wapo baadhi ya vijana ambao wanakiuka taratibu zetu na mimi hupenda sana kuwaambia kwamba wana hatarisha usalama wao na wana hatarisha usalama wa wananchi. Kwa hivyo naliomba sana Jeshi la Polisi wa Usalama Barabarani kuhakikisha kwamba wanachukua hatua kali kwa wale vijana ambao wamekuwa wakikiuka taratibu zetu hizi za sheria, wala wasimuonee muhali kwani baadhi ya wakati hata sisi Wawakilishi huwaombea wale vijana wanapofanya makosa. Naomba sana kupitia Baraza lako tukufu

vijana hawa wanapokiuka taratibu hizi basi ni lazima tuwachukulie hatua kwani kutii sheria bila ya shuruti ni jambo ambalo tunalihimiza sana, ili kuokoa vifo vingi ambavyo vinatokana na ajali ambazo visiwa vyetu vinakabaliana nazo hivi sasa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanataka kujua kile kituo cha daladala pale Kijangwani kitajengwa lini. Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Wizara ya Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambao pia wanashughulikia mambo ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba kile kituo tunakijenga ili kuwaondoshea wananchi adha na bughudha wanayoipata hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tumechukua ushauri tuliopewa kuhusu kujenga vituo vya kupumzikia abiria wakati wanasubiri usafiri katika sehemu tofauti za barabara zetu tulizojenga. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaarifu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba sisi kazi yetu kama wizara ni kuonesha kwa Wizara ambayo inashughulikia kazi hizo za kujenga vituo ili baadae wavijenge vile vituo. Sote tunajua mfano barabara ya Mwanakwerekwe tumeonesha sehemu za kuwepo vituo vitano upande mmoja na vituo vitano upande wa pili. Nina imani kubwa sana Wizara hii husika iko tayari kuifanya hiyo kazi pale ambapo bajeti itaruhusu na sisi tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha kwamba vile vituo vinawekwa ili baadae sasa kunapotokea tatizo lolote watu wasipate sababu ya kusema kwamba au wale wenye daladala kwamba kuna sehemu hamna kituo kile.

Mhe. Mwenyekiti, pia limezungumziwa suala la alama za barabarani. Kusema hili suala pia linatugusa sana, tunajua watu wetu wanavyopata tabu baadhi ya wakati wanapopita sehemu na kukutana na *traffic* hasa pale ambapo wanaambiwa wakwenda kinyume na *speed* iliyowekwa katika barabara zile. Kuna baadhi ya alama zimeondoshwa lakini sisi tutahakikisha kwamba zile alama zinarejeshwa ili baadae sheria zichukuliwe kwa wale wote watakaokiuka sheria zilizowekwa katika mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi kuna watu wametaka kujua kuhusu leseni za *PSU* na *FU* kwa magari ya abiria na magari ya mizigo. Mmoja wapo aliyeuliza suala hili ni Mhe. Ali Khamis Bakari. Kama nilivyosema mwanzo leseni za madaraja ya C na D zinatolewa Unguja kwa sababu Pemba hakuna Chuo chenye sifa ya kufundishia madereva wa gari hizo. Hivyo tunaendelea kuwashawishi watu mbali mbali wawekeze Pemba kuanzisha Chuo gari kubwa, yaani daraja C na D. Kwa hivyo mimi naomba kama Mhe. Ali Khamis Bakar anawajua watu hao basi tunawahimiza wafanye hiyo kazi na tuko tayari kushirikiana nao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Zaina Abdalla Salum ameuliza kuhusu kigezo kinachotumika katika utoaji wa leseni nimejibu kwamba daraja zinatofautiana, wanaanza umri wa miaka 16 mpaka kwenda juu na daraja ya juu kabisa ni ile daraja tunaita *general*. Kwa hivyo nina imani kubwa sana *concern* zao kuhusu umri wa hao wanaoendesha hivi vyombo ile ni sheria, kama wamehisi kwamba imefika wakati ile sheria ifanyiwe mabadiliko, basi sisi tupo tayari kushirikiana na wadau tofauti pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba ile Sheria Nam.7 ya 2003 tunaifanyia marekebisho kwa maslahi ya wananchi wetu na ili kupunguza hizi ajali za barabarani ambazo sisi hatupendi zitokee.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nina imani kubwa sana Waheshimiwa Wajumbe tumechukua matarajio yao na vile vile ushauri wao na yuko Mhe. Masoud Abrahman Masoud amezungumzia kuhusu wale ambao wanachukua gari na kwenda kuziunguza maeneo yale aliyoyasema. Kusema kweli tunasikitishwa sana na kama kuna watu wanafanya kitendo hicho basi naomba sana Jeshi la Polisi waendelee kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kwamba wale wote wanaofanya vitendo hivyo, ili baadae wajipatie Bima isivyo halali wanachukuliwa sheria ili kuhakikisha kwamba sisi sote tunajali utu na vile vile sheria zetu hizi za usalama barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha katika Idara hii ya Leseni ningeomba kidogo kuchangia hoja za Wajumbe wengine katika sehemu tofauti. Kuna Wajumbe wamechangia kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kuna Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mhe. Miraji Khamis Mussa….

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Naibu Waziri naomba nimpishe Mhe. Spika aendelee.

(Hapa Mhe. Spika alikalia kiti)

Mhe. Spika: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kuchangia katika hoja zilizotolewa na Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi. Sasa hivi nachangia kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, wapo Wajumbe wameulizia kuhusu ulipaji wa fidia kwa waathirika wale waliopo sehemu ya Uwanja wa Ndege ambapo hivi sasa tunaendelea na upanuzi wa Uwanja wa Ndege. Mmoja wapo aliyeuliza suala hili ni Mhe. Mwanaasha Khamis Juma. Napenda kumuhakikishia kwamba ni jana tu tumekutana na wale waathirika na tumekubaliana nao namna gani ya

kuwalipa fidia iliyobakia na wao wameridhika na majibu yetu. Vile vile kuna viwanja vyengine 13 ambavyo tutawalipa wale walioathirika ambavyo tayari tumekubaliana nao.

Kwa hivyo kusema la kweli nakushukuru sana Mhe. Mwanaasha tumekutana na wale watu na wameridhika na tunajua kwamba hili jambo liko muda mrefu tokea 2004. Lakini mimi niwapongeze sana wananchi wale kwa kuweza kusubiri kwa muda wote huu mpaka hapo ambapoi tutawalipa fidia kutokana na zile athari walizozipata baada ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na Waheshimiwa wengine pia walitushauri kuhusu kuwashirikisha wataalamu wetu wazalendo katika awamu hii itakayoendelea kwa ujenzi ule wa *Terminal II*. Ushauri wao tumeukubali na tunauchukua na ninamuhakikishia kwamba tutaufanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu ili baadae yale matatizo au changamoto zilizokuwepo hapo kabla zisitokezee tena.

Vile vile wengine waliulizia kuhusu *airport* maeneo ya *VIP* kuhusu kutokuwepo na watu wa kuchukua mizigo, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alichangia hilo. Napenda kumwambia tu kwamba kiutaratibu sehemu ya *VIP* unapofika pale mzigo wako unaonesha ile tiketi yako pamoja na kile kikadi chako cha kuonesha aina gani ya mzigo, na wafanyakazi wetu wanakuwa wanakwenda kule, kwenda kuutambua mzigo wako na wanauchukua wanauingiza mpaka ndani ya gari yako. Hiyo ndio sifa moja wapo ya *VIP*.

Kwa upande wa maegesho ya kawaida, wapo waliochangia na kutushauri kuhusu aina gani ya kuwasaidia walemavu. Kama tulivyosema pale vile vile wapo vijana ambao wamewekwa na vitambulisho maalum. Kazi yao sasa unawalipa cho chote ili baadae wauchukue ule mzigo na wa kupelekee katika gari yako. Ipo *concern* imezungumziwa kuhusu walemavu, hilo pia tumelichukua na tutalifanyia utaratibu lakini tunawashauri sana abiria wetu kwamba wasione tabu kuwalipa wale vijana pesa ambayo itasaidia wao kurahisisha kupeleka mizigo yao sehemu husika.

Mhe. Spika, lipo suala ambalo wajumbe wengi wamelizungumzia kuhusu *Terminal II* na wapo ambao wameomba mpaka kuundwe kwa Kamati Teule. Mhe. Spika, nasema kwa ukweli kabisa mimi nilibahatika kusafiri na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango kwenda China kuhusu kufuatilia suala hili la *Terminal II*. Tumetumwa ujumbe maalum mahsusi na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kujua umuhimu wa *Terminal II*. Yale ni makubaliano ambayo yalifikiwa baina ya Rais wetu mpendwa wa Zanzibar na Rais wa China kipindi kile alipokuja kufanya ziara Tanzania.

Mhe. Spika, tumekwenda kule wenzetu walikuwa wakati wa kipindi cha Krismas wameweza kuvunja safari zao za nje ili kuja kuonana na sisi kwa kuthamini mchango ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeitoa kwa China, katika maendeleo yao na vile vile katika maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Spika, wameacha kwenda katika shughuli zao za Krismas wakatupokea sisi, tukazungumza nao kwa ukweli kabisa na uhalisia kabisa na wakakubali kabisa kwa dhati ya moyo wao kwamba huu mradi hauna budi uendelezwe na kama kuna changamoto zote zilizokuwepo hapo kabla, zile changamoto tuziache kwa ajili ya maslahi ya nchi zetu mbili na kudumisha urafiki wa muda mrefu baina ya Tanzania na China. Naomba sana Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wajue hisia zetu katika mradi huu, tunajua kwamba mradi huu umechelewa, tunajua mradi huu kuna gharama mpaka sasa hivi zishatumika na vile vile kuna gharama ambazo zitatumika ili kukamilisha mradi huu ambao hadi kumalizika kwake zitatumika takriban Dola milioni 120.

Mhe. Spika, wako waliosema kwamba hizi ni pesa nyingi lakini namshukuru Mhe. Mohammed Aboud Mohammed amesema wazi sana katika kitega uchumi kama kile na kwa Serikali yetu ikiwa tumeweza kununua meli ya MV. Mapinduzi II ili kuokoa maisha ya wananchi wetu, basi na ujenzi ule ni ujenzi ambao utakuwa na faida kubwa sana, zipo gharama zimeongezeka kweli. Mwanzo ule uwanja ulikuwa umekadiriwa kuchukua abiria milioni 1,200,000 lakini baadae ikaonekana wazi kwamba kwa kukua kwa uchumi wetu hivi sasa na kuongezeka kwa watalii, hivi sasa tushafikia kwa mwaka abiria zaidi ya 800,000 wanatumia uwanja ule, huu wa sasa hivi tuliokuwa nao na tunategemea mwaka huu watafika mpaka milioni moja na zaidi. Nina imani kubwa sana kwa abiria 1,600,000 uwanja ule utakuwa umekidhi kwa miaka mingi ijayo. Kwa hivyo kwa serikali tunaomba sana mtuamini, zile gharama zilizotumika pale ni gharama ambazo zitakuja kuleta faida kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi tu tunatarajia ukimalizika ule mradi kuajiri wafanyakazi wengine pale zaidi ya 350, ni ajira nyingi sana, ni ajira ambazo zitawasaidia sana vijana wetu, vile vile zitasaidia katika kuongeza pato letu la uchumi. Kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakubaliana baadhi ya wakati mikataba inapowekwa ni mikataba ambayo inatakiwa ufuatiliaji na mimi nina imani kubwa sana katika mikataba hii chini ya uongozi wa Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wangu, tutakuwa tunafuatilia hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba mikataba yote tunayoingia katika Wizara yetu na Serikali kwa jumla, inakuwa mikataba ambayo ina maslahi kwa taifa letu. Nimuombe sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Mohammed Said Mohammed na wengine wote jana nilisikia msemo wa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba

tusiangalie tulipoanguka bali tuangalie tunapojikwaa. Na mimi nina imani kubwa sana yote haya yaliyofanyika tunajenga ukurasa mpya kwa ajili ya maslahi ya watu wetu na vile vile kwa ajili ya maslahi ya Chama chetu cha Mapinduzi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe. Ali Salum Haji alisema mengi. Nina imani kubwa sana na Wawakilishi na nyinyi mmesema mengi na nina imani kubwa sana yale yote yaliyosemwa mwisho wa siku tutahakikisha tunayatekeleza kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu na vile vile kwa Chama chetu cha Mapinduzi ambacho sisi kupitia Ilani yetu ambayo tulipita kwa wananchi kwenda kuinadi, basi yale yote tuliyoyaahidi mle tunayatekeleza ipasavyo na jengo hili ni moja wapo ya mambo ambayo yamepewa kipaumbele katika Ilani ile na tumesema kwamba tutaikamilisha katika kipindi cha Ilani hii. Waheshimiwa Wawakilishi tuungeni mkono, tupeni nguvu zaidi muipitishe bajeti yetu hasa katika jengo la *Terminal II* na ninakuombeni sana Kamati Teule tusiunde, kwa sababu haina haja ya kufukua makaburi sisi kilichokuwepo hivi sasa kuangalia wapi tunakwenda ili kuwapa moyo Waheshimiwa zaidi wenzetu wa China.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kama nilivyosema tulikwenda sisi kule na baadae akaja mjumbe mzito sana, Mjumbe wa Kamati Kuu kutoka China kafunga safari kuja maalum kuja kuliangalia lile jengo. Yule mjumbe ni mtu mkubwa sana, Mjumbe wa Kamati Kuu wa Chama cha China na ikiwa ni Naibu Meya wa Jiji la Beijing. Mhe. Spika, ametuhakikishia pamoja na wakandarasi wa ule mradi kwamba huu mradi utakamilika kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu na Balozi Mdogo wa China katuhakikishia ule mradi utakamilika iwapo tutauanza mwezi wa Julai, basi ndani ya miezi 24 ule mradi utakuwa tayari ushakamilika. Namuomba sana Mhe. Mohammed Said Mohammed ombi lake la kwenda kuweka nyaraka pale aliondoshe na nina imani kubwa sana kwa uongozi huu lile jengo tutalimaliza ili wananchi wetu waendelee kufaidika nalo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kutoka *Terminal II* naomba kidogo nizungumzie katika sekta ya usafiri baharini. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameulizia kuhusu meli zilizosajiliwa ambazo ni 186. Ni kweli meli zilizosajiliwa ni 186, kwa ujumla meli zile zina uzito wa *GRT* 439,312. Mapato ya jumla yaliyopatikana pale ni zaidi ya TZS.1,400,075,000. Kwa hivyo ni pesa nyingi kweli zilizopatikana na hii yote inatokana na kazi kubwa sana wanayoifanya watu wa *ZMA*. Mimi shuhuda nilikwenda Dubai katika kufungua ile Ofisi na Makamu wa Pili alikuja kututembelea, vijana kule wanafanya kazi kubwa sana. Ni vijana wachache lakini wanafanya kazi kwa uzalendo wa hali ya juu sana katika kuhakikisha kwamba zile meli zinazosajiliwa pale zinaingiza mapato kwa nchi yetu.

Kwa hivyo sisi tunaendelea kujipanga na tutahakikisha kwamba yale mapato yanaongezeka na kusema kweli Zanzibar inasifiwa sana. Kwa sababu kila

mmoja anataka kusajili meli zake kupitia usajili wa Zanzibar. Zanzibar ina sifa kubwa duniani, makampuni mengi yanataka kuja kujisajili lakini kama walivyotupa tahadhari Waheshimiwa Wawakilishi tunaangalia sana kuhakikisha kwamba kampuni tunazozisajili zisilete athari katika kulitangaza jina letu kama zile kampuni ambazo zinachukua labda madawa ya kulevya. Kwa hivyo tunachukua tahadhari hii ndio maana tunakuta tunafanya usajili wa uhakika kabisa ili athari hizo zisiikute nchi yetu ya Zanzibar kwani inasifika sana duniani.

Mhe Spika, kama nilivyosema suala la usajili ni suala la kimataifa pia ni suala la kibiashara ambalo linafanywa nchi nyingi sana kama Sierra Leone, Togo, Panama na Comoro pia hivi sasa baada ya kuona na sisi tunafanya hii biashara tena vizuri sana na wao wanataka kufungua Ofisi zao Dubai. Kwa hivyo ni mashindano makubwa sana lakini kama nilivyosema bado jina la Zanzibar ni *brand* linahitajika sana na makampuni mengi wanaendelea kuomba kufanya usajili kupitia ile kampuni yetu iliyokuwepo pale Dubai.

Kuhusu *ZMA* Mhe. Suleiman Sarahan ameuliza je, italeta boti za uokozi. Mhe. Spika, tunaendelea kufanya mazungumzo ili katika kipindi cha 2017/2018 kutafuta angalau boti nne za kufanya wenyewe wanasema ukaguzi, vile vile kufuatilia zaidi mambo ya uokozi na tunategemea boti hizo iwapo zitapatikana basi itawekwa katika bandari ya Malindi, bandari ya Mkokotoni na nyengine itawekwa katika bandari ya Mkoani na boti moja itawekwa kule Wete. Kwa hivyo tupo katika mpango huo na nina imani kubwa sana tutafanikiwa katika kufanya hii kazi ili baadae kunapotokea tatizo la kuzama kwa vyombo, mabaharia au kwa abiria basi tunaweza kufika sehemu ile kwa haraka zaidi na kuokoa maisha ya watu pamoja na mali zao.

Mhe. Mohamed Said Mohamed aliulizia kuhusu suala la kuridhia mikataba. Nataka kumuarifu kwamba kuna baadhi ya mikataba tayari tushaanza kuiridhia na imeshapelekwa katika Bunge letu na tunategemea wakati wote kuja kuridhiwa ili baadae sasa, yale masuala tofauti ambayo ni changamoto kwetu katika kuhakikisha kwamba tunapata mambo mengine ambayo yamezungumzwa kupitia *IMO* basi yanafanikiwa kwa haraka. Tumeendelea kuwashauri na kuwahimiza wenzetu wa Tanzania Bara katika kuhakikisha kwamba ile mikataba ambayo iko katika *IMO* inaridhiwa ili baadae na sisi tupate fursa. Kama tunavyosema Zanzibar inasifika sana tunataka kuanzisha Chuo cha Ubaharia kinachotambulika.

Vile vile tunataka kuhakikisha mabaharia wetu wanapata kazi katika zile meli na wanapofika kule hawapati tabu katika baadhi ya nchi wakashushwa. Kwa hivyo mimi namwambia Mhe. Mohamed Said Mohamed tunaendelea sana kulifuatilia hili na vile vile tunawaomba sana wenzetu hasa *SUMATRA*

waendelee kutuunga mkono, kwani kufanikiwa kwa Zanzibar ni kufanikiwa Tanzania na sifa yote inarudi kwetu na baadae wananchi wetu kuweza kupata ajira. Mhe. Spika, nina imani kubwa sana nimeweza kumtosheleza Mhe. Jaku Hashim na vile vile Mhe. Mohamed Said Mohamed kuhusu suala hilo la *ZMA* na sisi tumekuwa tunalifuatilia kwa karibu sana na nina imani baada ya muda mfupi tutapata ufumbuzi wa changamoto zilizokuwepo hapo mbele yetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hapo napenda kuzungumzia sekta ambayo vile vile inagusa nyoyo za watu wengi nayo ni sekta ya barabara. Mhe. Spika, tumeanza kazi vizuri sana na mimi niwapongeze watendaji wetu wa UUB na vile vile watendaji wengine wa wizara ambao tumekuwa bega kwa bega katika kuhakikisha kwamba zile ahadi tulizozitoa kupitia Ilani ya Uchaguzi wa CCM basi tunazitekeleza kwa ukamilifu. Kuna barabara nyingi tu ambazo sisi Wizara kupitia kitabu chetu cha Ilani tumetakiwa tuzitengeneze kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ambazo hivi sasa tumeshaanza chengine kuzitengeneza na nyengine tunaendelea kuzitengeneza, na nyengine nina imani kubwa sana tutazitengeneza. Kitabu chetu cha bajeti kimeelezea barabara ambazo hivi sasa tumezitengeneza na vile vile barabara ambazo zipo katika mpango wa kuzitengeneza mwaka 2017/2018. Nia yetu hasa ni kuhakikisha kwamba zile ahadi tulizotoa kwa wananchi kupitia Ilani yetu basi tunatekeleza kwa ukamilifu na zile barabara nyengine tunaendelea kuzitengeneza.

Mhe. Spika, ni karibuni tu tulikuwa Pemba na nilikuwa Unguja, kuangalia uharibifu wa mvua ambao kusema kweli hata sisi umetugusa na kama walivyotupongeza Waheshimiwa wengi na mimi vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote. Mhe. Spika, wako Wawakilishi tulipokuwa Pema tumeshirikiana nao kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunakwenda kuzikagua hizo barabara zao na vile vile kuzifanyia matengenezo kwa zile barabara ambazo tunao uwezo wa kuzitengeneza kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, zipo barabara ambazo tulikuwa hatuna budi tuzitengeneze kwa haraka. Kwa mfano barabara ambayo wengi tunaijua ya Mkoani/Chake Chake. Mhe. Spika, wakati inaharibika barabara hiyo tulikuwa katika ziara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenda kuwakagua wenzetu waliopata athari za mafuriko pamoja na maafa mengine, wamejionea wenyewe kuhusu namna mvua zile zilivyokuwa kubwa mpaka zile barabara zinakatika mtu wewe mwenyewe huwezi kuamini. Barabara nyingi zimejengwa kwa kiwango na kuna barabara nyengine zimeshakuwa chakavu. Kama hii barabara ya Mkoani/Chake Chake ambayo sisi vile vile katika bajeti yetu ya safari hii pamoja na barabara ya kutoka Tunguu mpaka Makunduchi tumetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya uchambuzi yakinifu, ili baadae sasa

barabara zile tuziombee fedha kwa wafadhili wetu ili tuzijenge katika kiwango kizuri na zipitike bila ya wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, tumeona athari barabara nyingi zimeharibika lakini mimi nichukue nafasi hii kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye wakati akitoa hotuba ya kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ameeleza kuguswa kwake na maafa yale na akatoa ahadi kwamba hizi barabara tutazijenga awamu kwa awamu na kadri hali ya uwezo wa nchi yetu utakavyoruhusu. Lakini tutahakikisha kwamba barabara zile zinapitika ima kwa matengenezo ya dharura au kwa kuitia kifusi au kwa baadae kuja kuzijenga kwa lami, lakini tunahakikisha kwamba barabara zile zinapitika.(*Makofi*).

Mhe. Spika, wako Waheshimiwa waliosema kwa nini tusubiri hizi barabara mpaka viongozi wapite wazione baadae ndio tuzitengeneze. Hatuwezi kusubiri viongozi, viongozi wametupa hii dhamana kwa kutuamini na wanajua tunaposema kwamba barabara hii imeharibika basi ile barabara imeharibika na inataka matengenezo. Barabara nyingi zimeharibika tumeziona zimeathirika sana lakini nina imani kubwa sana kwa mipango mizuri tuliyoipanga zile barabara tutazijenga hatua kwa hatua ili zirejee katika hali yake ya kawaida.

Mhe. Spika, maji yalikuwa makubwa sana na barabara hizi zimeathirika zaidi katika maeneo ya madaraja na zaidi Pemba. Mhe. Spika, udongo wa Pemba ni wa aina tofauti. Tumeona barabara zilizojengwa na Kampuni ya H. Young za kwenda Mtambwe, sehemu ambazo zilikuwa zikipasuka wenyewe mpaka baadae zikaja kujengwa kwa kutumia utaratibu wa *gabions* au *stone pitch.* Hiyo ni kutokana na kwamba nia na madhumuni ya barabara zile zilipojengwa ni kuhakikisha kwamba zinadumu kwa muda mrefu. Tumejifunza katika sehemu zilizoharibika, tuna imani sana tutazitengeneza ili baadae zisilete athari kwa wananchi wetu na ziendelee kuwa barabara za kudumu. Mhe. Spika, ziko sababu tofauti zilizofanya barabara hizi nyengine ziharibike kwa haraka ikiwemo magari ya uzito mkubwa, ikiwemo baadhi ya wakati kama nilivyosema kutuama maji na vile vile baadhi ya wakati kutokuwa na mitaro. Changamoto zote hizi tumezichukua na nina imani kubwa sana tutazifanyia kazi ili baadae hizi barabara ziendelee kupitika kwa wakati wote.

Mhe. Spika, wako ambao wamezungumzia ni kwa nini *tender* zote anapewa *MECCO*. Mimi napenda kusema wazi kwamba sio kama *tender* zote anapewa *MECCO*, lakini kuna utaratibu maalumu ambao unatumika katika kutoa *tender*. Kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa ile Sheria ya Manunuzi hizi *tender* zote inabidi zitangazwe, wako watu au makampuni yale ambayo yanaleta zabuni zao na baada ya kuleta zabuni, basi tunaangalia vigezo vyote ili baadae zile kampuni zinakabidhiwa zile *tender*. Kwa hivyo mimi

napenda kumtoa wasi wasi Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf hatua tofauti zimetumika katika kutangaza hizo *tender* na baadae kumpata mzabuni na baadae kuja kujenga barabara.

Mhe. Spika, barabara nyingi *MECCO* amejenga ikiwemo ya Mwanakwerekwe mpaka pale Fuoni, barabara hii nyengine ambayo *PRISMO* walianza ya kwetu kule Fumba baadae *MECCO* ndiye aliyekuja kumaliza, barabara ya Bumbwini, kuna barabara Pemba ya Gando - Wete, vile vile Konde - Wete ni barabara ambazo kusema kweli hata Waziri Mkuu alipokuja kufungua barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni aliona vile viwango na akatusifu sana.

Mimi niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kwamba sisi tutakuwa waangalifu sana katika kuhakikisha kwamba mzabuni yeyote anayepewa hii kandarasi basi anatekeleza kwa mujibu wa matakwa yale ya viwango vinavyotakiwa. Mhe. Spika, wapo waliosema labda hatuna viwango vya kuweza kuwapa wakandarasi. Sisi kwa mujibu wa taratibu zetu tunafuata viwango kutoka wenzetu wa Tanzania Bara lakini ushauri wa Waheshimiwa Wawakilishi tunauchukua na tutaufanyia kazi, ili kuhakikisha kwamba na sisi basi tunakuwa na viwango vyetu ili kuhakikisha kwamba hizi barabara zinakuwa zinadumu kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, lakini napenda kuwahakikishia Wawakilishi kwamba barabara zote vile vile zina muda wake, *life span* yake inaanzia miaka kumi mpaka kumi na tano na vile vile inategemea na matunzaji ya barabara. Sasa sisi tutachukua nafasi hii kuhakikisha kwamba hizi barabara tunazitunza ili ziendelee kudumu kwa muda mrefu zaidi.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba sana Wajumbe waamini kwamba mikataba hii inakwenda kwa taratibu zinazotakiwa na mimi karibuni tu nilikuwa nipo katika semina ya Bodi ya Wakandarasi, alikuja mkufunzi kutoka Bara, aliwafundisha wakandarasi wetu namna gani ya usimamizi wa mikataba hii. Mhe. Spika, walikiri wenyewe wakandarasi wetu kwamba yale masomo waliyopewa pale kwa muda wa siku tano ilikuwa ni darasa tosha kwao, kwa sababu mambo mengi walikuwa hawajui kuhusu huu usimamizi wa mikataba. Nikiri kwamba tuna upungufu huo lakini tunaendelea kila wakati tunapopata uwezo kuwasomesha wakandarasi wetu semina au mafunzo ili wajue hii mikataba inapofungwa wanaifunga namna gani. Vile vile wajue haki na wajibu wao wakati wanapofanya kazi zao na pale mkandarasi atakaposhindwa kufuata masharti basi ndani ya kipindi cha mwaka mmoja sisi tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba anafanya marekebisho kwa zile sehemu ambazo zimekuwa zina matatizo.

Kwa hivyo barabara zetu hizi zinakuwa na muda wa mwaka mmoja, kipindi cha kumuangalia mkandarasi na hiyo mikataba ambayo iko sehemu zote duniani. Sasa iwapo mtatwambia au mtatushauri namna gani ya kuongeza mikataba yao basi ushauri tutauchukua, iwapo itawezekana ikawa kwa mazingira maalumu ya Zanzibar basi sisi tuko tayari kuhakikisha kwamba tunafanyia utaratibu huo na baadae unakubalika. Lakini hiyo ni mikataba ambayo inafungwa na wengine wakandarasi kutoka nje ya nchi, kwa hivyo inabidi twende kwa mujibu wa mikataba ile ya kimataifa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa naye vile vile amezungumzia mambo mengi kuhusu barabara na matumizi ya barabara. Vile vile barabara yake wenyewe wanaita Pangeni mpaka Kitope au kwa jina jengine inaitwa Kichwele. Mhe. Spika, ziko barabara nyingi ambazo tumezielezea katika Ilani, zipo barabara za Bwejuu bado hatujaanza kuzitengeneza, ipo barabara ya Finya - Chika mote humo bado hazijatengenezwa, lakini kama nilivyosema tunakwenda kwa mujibu wa bajeti yetu na kwa mujibu wa fedha, lakini tuna imani kubwa sana katika kipindi cha miaka mitano ahadi tulizotoa kwa wananchi kupitia Ilani hii hasa katika ujenzi wa barabara basi tutaitekeleza ipasavyo.

Mhe. Spika, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi wawe na subra, nimeweza kuzitembelea barabara nyingi, zikiwemo barabara za ndani, barabara za Ndagoni, Birikau, Tironi mpaka za Micheweni, Fukuchani, Kajengwa kule za *MIVARF* na barabara nyengine zote ambazo bado haziko katika kiwango ambacho kinatakiwa. Mimi nina imani kubwa sana, zile ambazo tutaona zina umuhimu basi tutachukua hatua za kuzipa kipaumbele na kuanza kuzitengeneza. Juzi tu Mhe. Rais alikwenda kutembelea waathirika wa maafa ya mvua akatoa agizo la kwamba barabara ile inayotoka Fuoni mpaka kuja kwa Chimbeni ambayo imejengwa na *MIVARF*, basi tuangalie utaratibu wa kuijenga kwa lami na sisi agizo hilo tumelichukua ili kurahisisha usafiri wakati ambapo barabara ya Mwanakwerekwe inakuwa inajaa maji. Kwa hivyo yapo maombi, ushauri wa aina tofauti katika barabara.(*Makofi*).

Mhe. Ali Suleiman Shihata ametushauri pia katika kupunguza msongamano basi twende mpaka huku Kisauni. Ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Mhe. Spika, wako waliosema Ndagoni kule kuna miundombinu, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ alisema hapa kwamba wanaendelea kufanya uchambuzi yakinifu, lakini na sisi tutaangalia namna gani ijapo kwa kuanza basi tufanyie ukarabati maeneo yale ya dharura. Mhe. Spika, zipo barabara nyengine za Msingini zimezungumzwa zote hizo tutazifanyia utaratibu kuhakikisha kwamba tunazitengeneza.

Mhe. Spika, barabara nyingi zimeuliziwa lakini kama nilivyosema mwanzo zimenigusa sana na mimi niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi nilipokuwa Pemba kule nimeona namna gani wananchi wameacha hasa kuangalia itikadi zao za kisiasa, lakini zaidi wakitaka maendeleo ya hizo barabara. Nilikuwa Chambani kwa Mhe. Bahati Khamis Kombo niliona jinsi siku niliyopata bahati mbaya gari yangu kukwama wametoka mpaka watu wazee kuja kuikwamua gari yangu katika matope, wameacha kuangalia itikadi zao za kichama, wengine wazee nimewaonea huruma tunapigwa na mvua. Nikauliza nyinyi kwa nini mnafanya kazi hiyo? Wakasema sisi tunafanya kazi hii kwa sababu tunataka tuone barabara zetu tunatengenezewa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nimekwenda Kipapo Mgelema nikakutana na matatizo hayo hayo, nikasaidiwa na watu ambao hata wale watendaji wangu walikuwa wananiambia Mheshimiwa usijitambulishe. Nikawaambia hata haiwezekani, nitajitambulisha kama mimi Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba mnisaidie katika kukwamua gari yangu na wakaniahidi na kweli wazee wakaitumia kamba wakaikwamua gari ile. Kwa hivyo wanaonesha wameguswa sana.

Mimi niwapongeze Wawakilishi wote...

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Haya. Mimi niwapongeze Wawakilishi na niwaombe sana waendelee kutuunga mkono katika hili.

Mhe. Spika, mwisho kabla ya kumaliza nizungumzie suala la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Mhe. Nadir alitaka kujua wale wafanyakazi wawili hatua tulizozichukua. Kusema la kweli wale wafanyakazi mimi nimeguswa nao sana ni kama ndugu zangu, nimewaomba sana wafanye kazi waache kutumia majina ya wazee wao katika kufanya kazi. Nimeitwa na wazee nikawashauri na nikawaelekeza, imefika wakati unashindwa hujui uwasaidie vipi.

Mhe. Spika, mimi nitamuomba sana Mhe. Nadir Abdul-latif kama walivyokuomba wakakuletea maombi yao basi ukae na wale vijana uwaombe sana waangalie kwamba katika kufanya kazi mtu hupimwa kwa uwajibikaji wake, si chengine chochote na nidhamu kazini. Nina imani utanisaidia vile vile kuhusu wale watu waliouziwa ile nyumba baadae ikaja kuchukuliwa vyengine, nitamuomba sana Mhe. Nadir tusiunde Kamati Teule bali tuwaombe wale watu waendelee kukaa na watu wangu na mimi na yeye baadae tukae ili tulizungumze zaidi na nina imani tutalimaliza bila ya kulileta huku Barazani.(*Makofi*).

Mhe. Spika, pia ninamuomba sana Mhe. Mohamed Said Mohamed kuhusu nyumba zile za Kilimani, Ninajua tulikwenda pamoja na ninamuomba sana asizuwie shilingi wala asitake kufanya lolote jengine, tunatoa ahadi kwamba Bodi ya *Condominium* ambayo tumeiingizia ruzuku safari hii, itapokuja basi tutashirikiana na wananchi wake kama alivyosema mwenyewe tufanye harambee, ili kuhakikisha yale majengo tunayanusuru hasa katika kipindi hiki ambacho kuna maradhi ya kipindupindu na nina imani kubwa sana kama alivyo yeye na wananchi wake watajitolea kufanikisha hayo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nina imani kubwa sana Mhe. Waziri atakuja kutoa ufafanuzi mwengine katika yale ambayo nimeyaacha, kwa sababu yako mengi sana kuhusu wizara hii. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi na vile vile ninawaomba sana Wawakilishi wenzangu nao vile vile waiunge mkono bajeti yetu hii asilimia mia kwa mia, ili sasa watupe fursa na moyo zaidi wa kwenda kufanyakazi na nina imani hatutowaangusha, tuna deni kubwa sana kwao na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia deni hilo tutalilipa *inshaallah* kwa insafu.

Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri karibu sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa leo sote tuhai na wazima wa afya. Pili nataka nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Rais wangu aliyeniteuwa kunileta hapa na kunipa majukumu haya, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. (*Makofi*)

Kupitia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, nataka niwatangazie wananchi wote kwamba jukumu hili nililopewa na Mhe. Rais akishirikina na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nitalitekeleza kwa uwezo wangu wote na kwa kushirikiana na watendaji wa wizara.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jana nilipokuwa natoa *summation* ya *submission* yangu ya kuomba fedha za matumizi nilikuwa sikupata muda wa kutosha. Kwa hivyo kuna sehemu ya kuomba zile fedha za matumizi nilikuwa sijawahi kuziomba. Kwa hivyo nataka kutumia fursa hii Mhe. Spika, kukuomba kwamba maelezo yangu yote niliyotoa kwenye hotuba ambayo yamo katika vile ambavyo vimesambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, maelezo yale yatiwe kwenye *hansard*.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hayo nikata kuchukua fursa hii kuwashukuru sana, kwanza Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Ninawashukuru Wawakilishi wote waliochangia:

1 Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
2 Mhe. Jaku Hashim Ayoub
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
6. Mhe. Ali Suleiman Ali
7. Mhe. Omar Seif Abeid
8. Mhe. Bahati Khamis Kombo
9. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
10. Mhe. Mussa Foum Mussa
11. Mhe. Suleiman Sarahan Said
12. Mhe. Nassor Salim Ali
13. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
14. Mhe. Maryam Thani Juma
15. Mhe. Mussa Ali Mussa
16. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
17. Mhe. Mohammed Said Mohammed
18. Mhe. Miraji Khamis Mussa
19 Mhe. Ali Salum Haji
20. Mhe. Abdalla Ali Kombo
21. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Nakushukuru sana hasa kwa muongozo wako wa kisheria ambao nataka kuwahakikishia Mhe. Spika, Baraza lako tukufu kwamba utendaji wetu wote katika Wizara hii tunafuata Katiba ya nchi, Sheria na Kanuni.(*Makofi*).

Pia nataka kumshukuru:

22. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
23. Mhe. Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji- Namshukuru alivyonisaidia sana katika kazi zetu huko wizarani
24. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
25. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais
26. Mhe. Simai Mohammed Said.

Ningependa kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kuelezea shughuli ambazo tunazozifanya na nyote mnajua na wananchi wanajua kwamba Wizara hii inawagusa kwa ukaribu sana katika shughuli zao za maisha za kila siku. Lakini

wito ninaotaka kuutoa ni kwamba wakati serikali inafanya shughuli za kuweza kutatua matatizo yanayohusu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Tegemeo letu kubwa ni kwamba wananchi wenyewe nao wachangie katika kuhakikisha kwamba huduma ambazo tunazitoa katika shughuli hizo na wao wanahakikisha kuwa utumiaji wa barabara, wawe wanatumia vizuri na shughuli nyengine kutokana sheria kama tulivyoeleza mapema wawe ni wafuataji wa sheria ili shughuli zetu hizi ziende kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kulikuwa masuala mengine ambayo nilihisi ningeyajibu mwenyewe. Kwanza tuanze na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, sakata la ujenzi wa *Terminal II* kwenye uwanja wa *Abeid Amani Karume International Airport* karibuni nyote mnalijua na namshukuru Naibu Waziri wangu kwa kulielezea kwa undani kabisa. Hilo sitaki kuligusia isipokuwa nataka nieleze tu kwamba katika kuboresha uwanja wa ndege na huduma zake zinazotolewa kimataifa, kuna huu mtambo ambao tulikuwa tunaombwa tuuweke hapo unaitwa *ILS*.

Nakupenda kukuhakikishia Mhe. Spika, pamoja na Baraza lako tukufu kwamba suala hilo linafanyiwa kazi. Kabla sijaendelea nataka niwakumbushe tu Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba leo nimefarajika sana ya kuona kwamba Mhe. Spika, umekaa mwenyewe hapo na utanisadia kwa sababu naamini kwamba wakati fulani katika maisha yako na utendaji wako uliwahi pia kusimamia Wizara hii na ulisimamia vizuri sana. Kwa hivyo nategemea kwamba ninapokuwa najibu masuala hapa na wewe utanitetea kwa baadhi ya kadhia. (*Makofi*)

Kuhusu mashine za upekuzi katika eneo la mizigo. Mhe. Spika, ninataka kuhakikisha tu kwamba katika kutatua changamoto hiyo Mamlaka imo katika mchakato wa kufanya manunuzi wa mashine hiyo katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018. Mhe. Spika, kijana wangu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kalizungumzia sana suala la Kikosi cha Zimamoto kule katika uwanja wa ndege na alizungumzia kwa hisia kubwa sana suala la upatikanaji wa gari za Zimamoto.

Napenda kukuhakikishia Mhe. Spika, na Baraza lako tukufu pamoja na kumuhakikishia Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf kwamba katika kutafuta au katika ununuzi wa magari hayo tulifanya uadilifu na tulifuata utaratibu wa manunuzi yanayoagizwa na Benki ya Dunia na kuhusu vigezo vya hayo magari yote tulifuata kikamilifu, na pia kulitayarishwa zabuni ambayo kampuni tano ziliingia katika zabuni hizo na wahusika ndio wakachagua hiyo kampuni ambayo ilifanya kazi hiyo inaitwa *Kilman Industrial Automation Limited*. Ninapenda uhakika kama hakuna mbinu chafu uliyopita hapo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, suala la wafanyakazi wawili ambalo liliulizwa hapa, Mhe. Naibu Waziri wangu kalieleza vizuri sana na sina la kuongeza isipokuwa niseme tu kwenye suala la ndugu Sadala Abdalla Juma, yeye bado nilivyoambiwa kuwa bado ni mfanyakazi wa Mamlaka ambaye amesimamishwa kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Lakini yeye anaweza kwenda kuchukua hatua za kwenda kuomba zaidi suala lake liangaliwe tena, yaani anawweza ku-*appeal* ule uamuzi wa kusimamishwa kazi kwa muda.

Mhe. Spika, nimeambiwa kuwa huko *airport* kuna mashine ambayo inaweka plastiki katika mabegi ili kugharamia na gharama yake ni kubwa, hii wenyewe wanaita *wrapping machine* na kwamba gharama zake ni ghali ni shilingi elfu kumi na saba. Ni kweli shilingi elfu kumi na saba ukizibadili elfu kumi na saba Mhe. Spika, ni pesa nyingi sana na tunasafiri sana huko nchi za nje, hakuna mtu mzigo wake unakuwa w*rapped* na plastiki ikawa gharama zake zinafikia elfu kumi na saba.

Mhe. Spika, lakini kwenye hili tulikuwa tunasema kwamba anayefanya huduma hiyo ni kampuni binafsi na pengine niongeze tu jibu la kwangu mimi mwenyewe kwamba tumeruhusu wajasiriamali wafanye shughuli hizi na kama kuna mtu anamuhisi kwamba huyu jamaa anapata faida basi na yeye akampeleked, tunaita ushindani wa kibiashara. Vyenginevyo naona hili jambo la kawaida na pengine niwaulize tu hawa wahusika kwamba je, wanahitaji kwamba kila begi ambalo linasafirishwa lazima lifanyiwe *wrapping*. Jibu nililojibiwa ni kwamba ni wale tu ambao wanataka kuhakikisha usalama wa mabegi yao ndio wanafanya hivyo. Kwa hivyo mimi nasema ni uamuzi wa kwao na siishauri kwamba Wizara iingilie suala hilo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliulizia suala la kuweka miundo mbinu ya walemavu. Mimi kwenye suala hilo napenda kumjibu kwamba ni kweli kimataifa duniani watu wanakubali wazi kwamba kuna wenzetu kidogo wana matatizo ya ulemavu na sisi pia tusibweteke kuona kwamba kuwa ni wazima tunaweza kupanda ngazi, tunafanya shughuli nyengine tukasema kwamba hawa tuwadharau, hapana. Kuna msemo unaosema kwamba, "Kabla hujafa hujaumbika", tunaweza na sisi wenyewe pia tukaja kupata matatizo hayo. Kwa hivyo nashauri kwamba hili suala tutalifanyia kazi na kuhakikisha kwamba hawa watu ambao wana ulemavu pia tutawasaidia kuwahakikishia kwamba wanaweza wakatumia majengo haya kikamilifu.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar kauliza swala la kuvuja kwa jengo la abiria huko Pemba. Ni kweli kabisa Mhe. Spika, jengo hilo lilipata matatizo ya kuvuja na mimi mwenyewe nilipata kwenda huko Pemba na nikapanda kule kwenye kile chumba cha wageni mashuhuri na kwa bahati nikakuta wameweka ndoo pale za

kukinga maji na viti vimeondolewa. Sasa nilipoona suala lile nikasema nitalifuatilia na napenda kutoa uhakika kwenye Baraza lako tukufu kwamba kazi hiyo inafanywa na njia ambayo tunaitumia ni kwamba tutamfuatilia yule ambaye aliwahi kupata kazi ya kufanya matengenezo katika lile jengo na akalipwa vizuri tu. Lakini hiyo kazi hakuifanya zile ambavyo tuliitegemea, tunategemea kumfautilia ili tuangalie namna ya kutafuta suluhu ya tatizo hili.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa nataka kwa ruhusa yako niende kidogo kwenye suala la Mamlaka ya Mji Kongwe. Suala hili la Mamlaka ya Mji Mkongwe Mhe. Spika, Wajumbe wengi wameuliza maswali mengi sana. Imani yangu ni kwamba majibu mengine mnayajua isipokuwa mnataka mpate uhakika. Ni kweli kwamba tumeingia katika makubaliano ya *UNESCO* kwamba mji Mkongwe tuuhifadhi uwe kama vile ulivyokuwa. Huu ni uamuzi wa kisiasa na mimi niliposhauriwa, nikasema kwamba afadhali Mji Mkongwe wa Zanzibar tuendelee kuuhifadhi ili watoto wetu, wajukuu zetu na hao watakaokuja baadae watalii wakija hapa waje wauone Mji Mkongwe wa Zanzibar vile ulivyokuwa. Na nimehakikishiwa kwamba kuna baadhi ya watalii wanakuja hapa Zanzibar, kuja kutembelea Mji Mkongwe tu kuja kuona hali ilivyo. Kwa hivyo kwenye hili nilitaka Mhe. Spika, Wajumbe wako Wajumbe wa Baraza hili tukufu wakubali kwamba tuna haja ya kutunza Mji Mkongwe na katika kuutunza Mji Mkongwe kuna gharama zake na gharama zenyewe ni hizo kwamba huwezi ukajenga jengo lililokuwa limepaa zaidi kuliko *Bait el Ajaib* la *shooting* ile ambayo tumeelekezewa.

Kwa hivyo, kwenye hilo jibu kubwa ni hilo tu kwamba jukumu kubwa la Mamlaka ni kusimamia ujenzi wa haya wa haya majengo na kuyafanya yarejee katika hali yake ya zamani, lakini gharama zake za kujengea, hizo inabidi atoe mwekezaji au tutoe sisi upande wa Serikali na tunalo Shirika la Nyumba ambalo linashughulikia ukodishwaji wa nyumba, baadhi ya hizo ziko katika maeneo ya Mji Mkongwe na uhakika ninaotaka kuutoa ni kwamba tunafanyia kazi zoezi hilo la kutafuta fedha ili nyumba zetu ambazo tunazikodisha kwa upande wa Mji Kongwe ziwe kwanza kabla ya kusema kwamba tunazitunza tuhakikishe kwamba hazianguki, tuzihifadhi ziwe kwanza hazianguki, baadae tuhakikishe kwamba zinafanyiwa matengenezo stahiki.

Katika suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye ameulizia na amezungumzia suala la kwamba haafiki wazo la kuzivunja Skuli ya Darajani na Vikokotoni na kumshauri Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mji Kongwe kuishauri serikali kuhusu suala hilo.

Ningependa kumjibu Mheshimiwa kwamba wizara imelipokea wazo hilo na kufikiria kutozivunja skuli hizo kutokana na malalamiko ya wananchi na

kutaka serikali kulifikiria jambo hilo. Kwa hivyo ninachotaka kusema hapa Mhe. Spika, ni kwamba tutakwenda kushauri kwamba katika kujenga upya hiyo *Darajani corridor*, basi skuli hizo za kihstoria hazitavunjwa. Lakini pia nataka niongezee tu kwamba Wizara yetu hii inashirikiana na Wizara nyengine katika shughuli hizi na tutakwenda tukaendeleze mashauriano hayo kwa lengo na nia ya kwamba tuweze pia kuzihifadhi hizi skuli zisivunjwe.

Mhe. Spika, pia Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia alimetoa ushauri hapa kwamba tupungeze eneo la Uhifadhi wa Mji Mkongwe lipunguzwe mpaka lifikie *Greek Road*, yaani pale Darajani eneo hili tutoke *station* ya Polisi ya Malindi moja kwa moja mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja huku iwe njia ile ndio mpaka. Kwenye hilo Mhe. Spika, ningependa kujibu tu kwamba mipaka ya eneo la urithi wa dunia linapindukia upande wa barabara ya *Greek road* Darajani, hii ndio inayotambulika kwenye Kamati ya Urithi wa Dunia na kulipunguza inaweza kusababisha kuondoshwa kwenye orodha hiyo.

Hapa ili tuelewane zaidi kwamba nilisema pale awali Mhe. Spika, kwamba ilibidi tufanye uamuzi na tunabakia katika himaya ya urithi wa dunia ya *UNESCO* au tunatoka. Uamuzi wetu ni kwamba tunabaki na kwa kuwa tunabaki basi inabidi tuendelee tuwe na eneo la uhifadhi lile ambalo tumekubaliana nao wale wahusika na kulipunguza hilo kama nilivyosema itakuwa kuna hatari ya sisi kufukuzwa huko na hatutaki kufukuzwa.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Seif Abeid na yeye anaulizia sababu iliyopelekea jengo la *Bait El Ajaib* kutofanyiwa mategenezo ni kitu gani. Kwa ufupi tu Mhe. Spika, naweza kusema kwamba tayari mpango huu wa kitaalamu umeshatayarishwa na kupata baraka za Kamati ya Urithi wa Dunia kwa ajili ya uendeleaji wa kazi ya matengenezo ambayo tayari mfadhili ni Serikali ya *Sultanate of Oman* imeshajuilishwa juu ya hilo na wameahidi kutupatia fedha za matengenezo, na nataka kusema tu kwamba iwapo itashindikana kabisa kupata mfadhili wa kuifanya kazi hii basi serikali yetu itabeba jukumu hilo la kutengeneza jengo hilo sisi wenyewe.

Mhe. Spika, kumeulizwa suala juu ya kuwekwa mashine ya kupekulia abiria na mizigo katika bandari ya Malindi. Mhe. Spika, Shirika la Bandari tayari limeshanunua mashine mbili za kupekulia abiria na mizigo, yaani *X-ray machines* na milango yake na pamoja na tayari zimeshafungwa na zinafanyakazi hivi sasa katika gati ya abiria Malindi. Aidha Shirika la Bandari limepanga kuongeza mashime nyengine mbili ndani ya mwaka ujao wa fedha 2017/2018. Moja kwa Gati kuu ya Malindi na nyengine kwa gati ya Mkoani Pemba.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Maulidi Diwani yeye ameulizia suala la wingi wa vitengo katika bandari ya Malindi na vinasababisha usumbufu kwa wateja. Hilo ni kweli kabisa kuna vitengo mbali mbali katika bandari ya Malindi. Vitengo hivyo vipo bandarini kwa mujibu wa sheria na vinafanyakazi kwa niaba ya serikali ili kusimamia taratibu za nchi na ukusanyaji wa mapato ya serikali. Mhe. Spika, hivi sasa serikali inafanya tathmini ya umuhimu wa kuendelea kuwepo kwa taasisi hizo zote au baadhi ya vitengo hivyo kuviunganisha na kuvipunguza, au kuviweka sehemu moja kutokana na mahitaji ya sheria na kanuni zao, zoezi hilo linaendelea.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuweka *charges* kwa makontena yanayokuja Zanzibar. Wizara kwa kushirikiana na Bandari imeshauriana suala hilo na tunaahidi kulifanyia kazi na hasa wakati huu ambapo msongamano wa meli umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Bahati Khamis Kombo yeye ameulizia kuhusu msongamano wa magari katika eneo la bandari ya Mkoani. Mhe. Spika, Shirika la Bandari limeamua kulitumia eneo hilo kwa muda ili kuondoa msongamano mkubwa uliokuwepo mbele ya lango la kuingilia bandarini, hali hiyo imesaidia kuondoa msongamano hapo mlangoni. Hata hivyo, shirika limeanza kuwasiliana na Baraza la Mji la Mkoani ili kuwatafutia eneo jengine maalum la kuegesha magari.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Bahati Khamis Kombo, suala lao ni kwamba kuweka kipaa kwenye njia ya kupitia abiria kwenye gati ya bandari ya Mkoani au kuweka utaratibu wa mabasi kuchukulia abiria. Mhe. Spika, Shirika la Bandari limeangalia uwezekano wa kujenga kipaa sehemu hiyo na kuona kuwa ujenzi huo utaweza kuleta usumbufu katika kuitumia gati hiyo ipasavyo. Hata hivyo, Shirika la Bandari linaangalia uwezekano wa kutumia mabasi maalum kuwasafirisha abiria kuwapeleka gatini kama inavyoshauriwa.

Mhe. Maryam Thani Juma aliulizia kuhusu matengenezo ya bandari ya Wete na hatua iliyofikiwa. Mhe. Spika, matengenezo ya Gati ya Wete yanaendelea kwa kuifanyia ukarabati mkubwa gati hiyo, kwa kuongeza upana hadi kufikia mita tisa za ziada pamoja na kuweka sawa eneo lililodidimia. Kazi hiyo inategemea kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha 2016/2017. Aidha, serikali imo katika hatua za mwisho za majadiliano na mwekezaji binafsi ambaye ameonesha nia ya kujenga gati mpya ya abiria katika bandari hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Makame Ali aliulizia suala la kuhusu eneo la kuwekea makontena katika bandari ya Mkoani. Ni kweli kuwa eneo hilo limetengenezwa kwa ajili ya kuweka makontena, eneo hilo halijaanza kutumika kama ilivyokusudiwa kwa sababu wafanyabiashara wenyewe hawajawa tayari

kutumia bandari ya Mkoani kushusha makontena, pamoja na kuwa shirika limeanza kupeleka vifaa kwa ajili hiyo. Shirika linaendelea kuwashawishi wafanyabiashara waanze kupeleka mizigo yao huko. Mhe. Spika, napenda kulitangazia Baraza lako tukufu kwamba wapo wafanyabiashara tayari wameshaleta maombi yao wizarani, kuomba waitumie bandari hiyo kwa kushusha na kupakia makontena.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani aliulizia kuhusu mikato mingi kwa vyama vya ushirika wa bandarini. Mhe. Spika, ni kweli kuwa kuna mikato katika malipo ya vyama vya ushirika bandarini yanayotokana na Sheria za Kodi. Mikato hiyo ni pamoja na *withholding tax* na *custom duty*, kodi hizo zinakatwa na *ZRB* pamoja na *TRA* kulingana na sheria zilizowekwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Abdalla Maulidi Diwani, Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Nassor Salim Ali wametoa pongezi kwa wizara kwa kupitia Shirika la Bandari. Pongezi hizo tunazipokea na tunawashukuru sana na pia kuwahakikishia kuwa tutaendeleza jitihada za kutoa huduma bora kwenye bandari zetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nilikuwa nataka niende kwenye Shirika la Meli la Uwakala na huko kuna masuala yaliulizwa na Mhe. Shamata Shaame Khamis, yeye alikuwa anatoa ushauri kwa wizara kuangalia uwezekano wa kuanzisha huduma za usafiri wa meli kati ya kisiwa cha Pemba na Tanga, ili kuwaongezea ajira wananchi na kuepuka maafa ya baharini. Hilo ni shauri zuri sana. Tukumbuke Mhe. Spika, hivi karibuni tu tulileletewa habari hapa kwamba meli moja ambayo ilikuwa inachukua mizigo kutoka Tanga kuelekea Pemba ilichukua na abiria pia na wakapata maafa makubwa wakatutia majonzi makubwa. Kwa hivyo ushauri huu tutaushughulikia. Wizara yetu imepokea ushauri huu na inaahidi kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Aidha, kwa muda huu nawaomba wananchi wa Pemba waendelee kutumia huduma zinazotolewa na sekta binafsi, kupitia kampuni zenye vyombo vya uhakika vinavyoruhusiwa rasmi kisheria kusafirisha abiria. Kwa vile meli za serikali haziwezi kuingia bandari ya Tanga kwa ufanisi kutokana na kuhitaji kina kirefu cha maji, tofauti na ilivyo katika bandari hiyo.

Mhe. Asha Abdalla Juma alizungumzia kuhusu fedha zilizotengwa kwa ununuzi wa boti ndogo ndogo kama zinatosha kutatua changamoto iliyopo kwenye visiwa vyetu ni vingi. Kweli Mhe. Spika, kama alivyouliza swali lake kuwa visiwa vidogo vidogo ni vingi, hivyo mradi huu utakuwa endelevu na fedha zilizotengwa ni za kuanzia tu mradi huo. Kwa mwaka huu wa fedha jumla ya boti nne zinatarajiwa kununuliwa kwa kuhudumia maeneo yafuatayo:-

1. Wete/Fundo,
2. Makoongwe/Kisiwa Panza Mkoani,
3. Mkokotoni/Tumbatu
4. Likoni/Kojani.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliulizia Shirika la Meli kuna tatizo la kulipishwa kodi za serikali tofauti na wawekezaji wa fani hii ambapo kuwa huwa wanapatiwa msamaha, yaani *tax holiday*, iweje fursa hii wasipewe nao Shirika la Meli. Suala zuri sana Mhe. Spika, lakini suala hili ni la kisheria na jibu lake ni kwamba kodi zote zinazolipwa na Shirika la Meli ni tozo za kisheria ambazo mashirika yote ya serikali yanawajibika na yanalipa kodi hizo kikamilifu.

Mhe. Spika, Mhe. Hamida Abdalla Issa aliulizia wizara iharakishe matengenezo ya meli ya MV. Mapinduzi kwa vile wananchi wameanza kuilaumu serikali kutokana na kukosekana huduma hiyo. Kama nilivyotangulia kujibu Mhe. Spika, michango mbali mbali kuhusiana na maharibiko ya meli ya MV Mapinduzi II. Wizara yetu kwa kupitia Shirika la Meli imechukua hatua za dharura kuangalia kifaa kilichoharibika na tunatarajia kukipokea leo na matengenezo yataanza mara moja, ili kuona huduma zinarejea katika hali ya kawaida hivi karibuni. Kwa hivyo nawaomba wananchi wawe wastahamilivu na wizara yetu inaelewa tabu wanayoipata na inaahidi kurejesha huduma hiyo hivi karibuni.

Mhe. Spika,....

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani kidogo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 96(5) una muda usiozidi saa moja wa kufanya majumuisho lakini Mhe. Naibu Waziri tulimpa dakika 20 katika muda wako. Kwa hivyo utakuwa una dakika 40. Kwa maana hiyo utakuwa umebakiwa na dakika 10 tu za kumaliza ili tuweze kwenda kwenye shughuli nyengine.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kuna swali muhimu sana liliulizwa kuhusu habari ya gharama za kufungua ofisi ya *ZMA* kule Dubai. Gharama hizo zote ni gharama ya usajili wa ofisi ni Dola 20,000 gharama za kazi na *resident permit* ni Dola 6,000, gharama za kodi ya jengo Dola 20,000, gharama za ukataji wa partition, kuleta mawasiliano na ununuzi wa vifaa na ufunguzi wa ofisi Dola 34,000 na Dola 4,000 ni kwa ajili ya gharama za mafunzo kwa wafanyakazi. Jumla yote ni Dola 84,000.

Mhe. Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla aliulizia kuwa jengo la Wizara ya Fedha kule Pemba katika hali yake lilivyo. Jibu lake Mhe. Spika, ni kwamba jengo

hili linamilikiwa na Wizara ya Fedha, wizara hiyo ilitoa zabuni ya kulivunja kwa kupitia Idara ya Ujenzi iliyokuwa zamani na kutayarisha makisio ya kulivunja jengo hilo kitaalamu na kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Hivyo, tunasubiri majibu kutoka Wizara ya Fedha kwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, kuhusu swali la Mhe. Zaina Abdalla Salum la kuhusu jengo la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, utanisaidia kwenye jibu hilo, lakini jibu la wizara yetu ni kwamba tutashirikiana na wahusika kwenye Baraza la Wawakilishi tuangalie namna ya kujengewa hizo huduma ambazo watazihitaji watu waliokuwa wana ulemavu.

Ahsante Mhe. Spika, ningependa tu kujibu kwa haraka masuala mengine yaliyoulizwa ya Shirika la Meli. Kuna suala tumeulizwa hapa kuhusu mchakato wa ujenzi wa meli mpya ya mafuta, abiria na mizigo uharakishwe. Kwenye hilo naamini wazi Mhe. Naibu Waziri amelijibu vizuri, mimi sina jibu la ziada. Isipokuwa napenda tu kuwahakikishia kwamba kazi hiyo ya kununua meli mpya kwa sasa hivi iko katika hatua kubwa sana na tunategemea hivi karibuni kupeleka ujumbe nchini Uholanzi ili kwenda kufanya mazungumzo ya mwisho na ile kampuni ambayo itakuwa inafanya shughuli hizo.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala liliulizwa kuhusu habari ya utatuzi wa uuzwaji tiketi kiholela bandarini. Jibu lake kwa ufupi ni kwamba hatua zimechukuliwa za kuhakikisha kwamba tiketi zitakuwa zinauzwa moja kwa moja bila ya kupitia kwa wakala, na pia kutumia teknolojia ya kisasa ya *barcode readers* ambayo sasa hivi imeshaanza kufanyakazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuwa na hoja tatu kuhusiana na safari ya Meli ya MV Mapinduzi II nchini Comoro. Jibu lake Mhe. Spika, ni kwamba meli hiyo kweli haikuweza kufunga gati katika safari ya Comoro, lakini hiyo ilitokana na kwamba watu wa *port* ya Comoro walishauri kwamba meli mpya kama ile na kubwa ni afadhali ikae kwenye *router bridge outer in credge* kuliko kuchukua dhamana ya kuipekeka kwenye gati. Wafanyakazi melini *crews* walikuwa wengi kuliko abiria katika safari hiyo. Hiyo Mheshimiwa imetegemea kwamba matangazo yaliyotangazwa hayakutangazwa vya kutosheleza. Kwa hivyo hatukupata abiria wa kutosha lakini tunategemea kwamba safari nyengine tutapata abiria wa kutosha. Meli hiyo napenda kutoa uhakika Mhe. Spika, kwamba inaendeshwa kitaalamu na inaedeshwa na wataalamu hakuna tatizo kwenye hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Nassor Salim Ali walitaka kujua tatizo lililoikabili Meli ya MV Mapinduzi II tena, iliyopelekea kusita kufanya safari zake na wameshauri hatua za haraka zichukuliwe kurudisha huduma hizo. Tatizo lililoikabili Meli ya MV

Mapinduzi II hivi sasa ni maharibiko na hayo nimeshayaelezea, kuwa yanatokana na *generator* kwa kupeleka umeme katika *engine* na kushindwa kupeleka umeme huo, kwa sababu ya kifaa ambacho kimeharibika na hivi sasa tumeshakiagiza na kama nilivyosema tunategemea kwamba meli hiyo itaanza shughuli zake haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Abdalla Mussa alitaka kujua katika mchakato wa ujenzi wa meli mpya za serikali wataalamu wazalendo wameshirikishwa vipi. Nataka kumuhakikishia kama nilivyosema kwamba mchakato uko katika hali ya juu na wataalamu wawili kutoka Shirika la Meli wameshirikishwa kikamilifu katika suala hilo.

Mhe. Mussa Foum Mussa aliulizia katika mchango wake alitaka kujua mambo yafuatayo, ongezeko la safari kutoka abiria 85 kwa mwaka mpaka kufikia abiria 168 kwa mwaka. Mhe. Spika, safari zilizokuwa mwaka uliopita 85 na sasa 168, hii imetokana na ongezeko hilo la safari ya abiria pamoja na mizigo kwa matarajio ya kuongezeka idadi ya safari za ndani kutoka nje hadi sita kwa wiki.

Aidha, safari za Mombasa na Comoro ambazo zitakuwa endelevu pia zinatarajiwa kuongezewa ufanisi. Kiufupi safari zitakuwa zimeongezwa. Wizara yetu ilikuwa inakamilisha taratibu za kisheria kuhusiana na kuiuza Meli ya MV Maendeleo ambayo hivi sasa zimekamilika, na kuanzia sasa matangazo kuhusiana na uuzaji wa meli hiyo wakati wowote yatatoka kupitia vyombo vya habari. Mhe. Spika, nataka kuwatangazia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba kama kuna mtu au watu wanataka kuinunua meli hiyo waje Ofisini. Meli ya MV Ukombozi nayo inatarajiwa kuuzwa kutokana na uchakavu na kutokana na kupoteza sifa za kufanya biashara kulingana na matakwa ya Shirika linalosimamia usafiri wa baharini ulimwenguni.

Mhe. Spika, kwa hayo machache natumai kwamba nimeweza kujibu karibuni masuala mengi ambayo nimeulizwa hapa. Kwa kumalizia tu nataka Mhe. Hassan Khamis Hafidh aliuliza suala kuhusu ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Ningependa tu kumjibu, ujenzi utaanza mara tu baada ya kusainiwa mkataba wa mkopo, (*Loan Agreement)* baina ya Serikali ya Muungano ya Tanzania na Benki ya Exim ya China. Rasimu ya mkataba huo tayari imeshapitiwa na kuridhiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini bado rasimu hiyo inaendelea kufanyiwa kazi na Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ujenzi huo unatarajiwa kuchukua miezi 36 na kama nilivyosema inatarajiwa kuanza haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kuhusu uchimbaji uliofanywa katika Hoteli ya *Mtoni Marine*, kama uliyofanyiwa uchunguzi wa kimazingira. Jibu lake Mhe. Spika, ni kwamba uchimbaji huo ulifuata taratibu zote, ikiwemo uchunguzi wa kimazingira kwa mujibu wa sheria.

Suala la hoja kuhusu Kampuni ya Azam kupeleka boti yake eneo la Hoteli ya *Mtoni Marine* kama ni kinyume na sheria au inafuata sheria. Jibu lake ni kwamba ni kweli kuwa Kampuni ya Azam iliwahi kupeleka vyombo vyake kulaza hapo Mtoni. Hata hivyo, hivi sasa utaratibu huo umezuiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bandari na hivi sasa hazipelekwi tena huko Mtoni.

Mhe. Spika, Mhe. Hassan Khamis Hafidh na yeye aliulizia kampuni ambazo zinapewa kazi na Idara ya *UUB* kama zimesajiliwa. Jibu lake ni kwamba kampuni hiyo iliyotajwa ya *Abdalla Contract Company Limited* ilipewa kazi za ujenzi wa barabara ya Wirelesi/Chukwani na pia Buyu/Fuoni Kibondeni. Kampuni hii Makao Makuu yake yapo Dodoma na ilifanya kazi ya ujenzi wa barabara hizi na kukamilika. Hawa ni miongoni mwa wakandarasi wa mwanzo wazalendo kuanza kufanya kazi za matengenezo ya barabara. Kampuni hiyo ilikidhi vigezo vyote vinavyohitajika kufanyakazi.

Mhe. Spika, kwenye Idara ya *UUB* kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa mmoja kwamba ameona katika programu ya uratibu Pemba kuwa Tanzania shilingi bilioni 2,142,580,000 zitatumika kwa shughuli mbali mbali ikiwemo matengenezo ya barabara mbali mbali Pemba. Barabara inayotoka Pandani kwenda Miwani kupitia Kivungo kwenda Wingwi itakuja na hiyo iingizwe kwenye bajeti. Jibu Mhe. Spika, ni kwamba kwa ufupi fedha zilizotajwa ni kwa ajili ya shughuli za ulipwaji wa mishahara na matumizi ya kawaida ya Ofisi. Hata hivyo, ombi lako limepokelewa na litafanyiwa kazi pindi fedha zitakapotosha.

Mhe. Spika, nimefikia hapo ningependa kukushukuru sana kwa kunipa muda huu kuelezea kuhusu maombi haya ambayo tunayafanya kwa Baraza lako tukufu tupatiwe fedha na uwezo wa kuweza kufanya hizi kazi ambazo wananchi wanatutegemea kwamba tutazikamilisha.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama kamati lisikilize ombi.

Mhe. Spika: Bado kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, Bado. Kwa hivyo, baada ya maelezo haya Mhe. Spika, napenda kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wale wote ambao wanaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya maelezo haya yote na kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yetu.

KAMATI YA MATUMIZI

UTARATIBU

Mhe. Mwenyekiti: Naam Mhe. Jaku Hashim Ayoub vipi tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nataka kidogo nataka kuelimishwa tu Kanuni ya 98(5) lazima nikupongeze. Juzi katika kuendesha kikao umetumia hekma na busara za hali ya juu kwenye hoja moja kwa Wajumbe watatu, nilikuwa nataka kujua tutaendelea na utaratibu ule ule kama uliotuendesha juzi au mwengine.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tutaendelea na ule utaratibu ambao nimeuanzisha, tutataja fungu lile la program halafu utanyanyukia kifungu chochote kidogo ambacho kimo. Lakini kifungu hicho kidogo hakitohojiwa na zaidi ya watu watatu, tutakwenda kwa utaratibu huo na jielekezeni zaidi kwenye vifungu vya fedha au mambo yanayohusu sera.

Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kukumbusha hilo, tunaendelea Waheshimiwa.

FUNGU P 01 - WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Kifungu P0101 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Khamis Bakari samahani haya ni mapato.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Mwenyekiti, ulisema tuangalie kwenye vifungu ambavyo...

Mhe. Mwenyekiti: Huko unakotaka bado Mheshimiwa imetajwa Pemba tu lakini hatujafika tuendele.

Kifungu P0101 Ofisi Kuu Pemba 387,000,000
Kifungu P0104 Idara ya Ujenzi 35,000,000
Kifungu P0106 Idara ya Usafiri na Leseni

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa haya ni makusanyo tu, hizo hoja zenu hazipo hapa tuendelee.

Kifungu P0106 Idara ya Usafiri na Leseni 2,421,970,000
Kifungu P0109 Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba uendelee kukaa kwanza bado, tuendelee.

Kifungu P0109 Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe40,000,000
Jumla Kuu ya Makusanyo **2,883,970,000**

(Vijifugu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu P01

Mhe. Mwenyekiti: Haya ahsante Waheshimiwa sasa nitaaza kutaja hiyo *list* kwanza niorodheshe hapa, nikikutaja unakaa kitako Mhe. Ali Khamis Bakari nikishakutaja ukae kitako lakini utachangia wewe mwanzo.

Mhe. Ali Khamis Bakar, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Suleiman, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na mapacha wangu hawa nitaanza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani halafu Mhe. Hassan Khamis Hafidh atakuwa mwisho na Mhe. Mohammed Said Mohammed nimekuona pia ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakai anza. Naomba lakini utaje hicho kifungu.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Sawa sawa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nimechangia kwa maandishi Mhe. Waziri nimemuuliza

hapa kuhusiana na utaratibu ambao sasa hivi Kitengo cha Leseni kule Pemba cha magari makubwa kimeondolewa, hatujui ni kwa sababu gani na sasa hivi wananchi wanahangaika, yaani leseni sasa hivi kupasisha mpaka uje Unguja. Sasa nilitaka muongozo wake yeye Mhe. Waziri anifahamishe. Je kuna sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mheshimiwa ulionesha nia ya kuuliza.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Nilichangia eeh! ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, natumai Mhe. Ali Khamis Bakar nilipokuwa nikitoa ufafanuzi hakunisikia vizuri lakini kama nilivyosema sasa hivi kutokana na zile *class* ambazo amesema kwa hivi sasa imebidi kweli tunajua hilo tatizo kwamba linawakuta usumbufu watu wetu. Lakini kama ulivyosema sisi tunaendelea na juhudi za kuonesha kwamba basi na Pemba wanapata leseni ili kuondosha adha ya kutoka Pemba kuja Unguja kufuata zile huduma. Kwa hivyo namuomba sana atustahamilie tunaangalia namna gani ya kutatua.

Lakini nataka kumfahamisha tu kwamba hivi sasa tupo katika hatua ya kutaka kuimarisha huduma zetu pale na tunaelekea katika kufanya Wakala wa mambo haya ya Usafiri. Kwa hivyo atustahamilie sana kwa hilo.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia kwa majibu yake mazuri lakini mimi nilitaka huu muda. Maana kustahamilia ni kweli na leo tunaipitisha hii bajeti yao.

Sasa ni muda gani kwa sababu muda mwingi kusema kweli mimi tokea sijaingia humu Barazani basi kule kitengo hichi hakipo wananchi wanahangaika. Sasa nataka kujua ni muda gani.

Mhe. Mwenyekiti: Ushafahamika Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomjibu hapo mwanzo basi pale tu ambapo taratibu zitakamilika basi ile huduma tutairejesha kule Pemba.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi pia…

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kipi, naomba ukitaje hicho kifungu ulichochangia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ndio naendelea kukitaja ni SP010101, lakini ukenda na chengine cha pili huku SP 010103. Nitazungumzia kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye program mahsusi ndogo H, program zenye H.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: HP 010101 halafu HP010103

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo hiyo moja tu Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya lakini si naweza kuelezea mambo mawili ambayo tofauti niliyozungumza.

Mhe. Mwenyekiti: Moja tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Moja tu. Mimi nilitaka kujua kwa sababu nilichangia kwamba barabara tunaziona kwamba mbovu karibu zote, isipokuwa zilizojengwa tu na baadhi ya watu misaada ya nje kama ya Nungwi na sehemu nyenginezo lakini zilizobakia karibu zote mbovu, zina mashimo ukichunguza hazina kiwango, nikaja nikaulize nije nijibiwe katika kuwapa *contract* hasa huyu *MECCO* anayepewa karibu njia zote za Zanzibar kama mtu wa Tanzania, anaweka *security* ya shilingi ngapi pindipo itapotokea ile *damage* katika barabara sijajibiwa.

Pili ameweka *guarantee* miaka mingapi katika serikali pindipo itatokezea *any problem* na barabara ile ataweza kutengeneza kama zilivyotengenezwa nyengine.

Lakini la tatu nikazungumza kwamba kampuni ngapi zimekuja kwenye suala la barabara matokeo yake anashinda yeye kila siku.

Lakini la nne …

Mhe. Mwenyekiti: Basi Mheshimiwa Mhe. Waziri mjibu.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nimeona suala hili bora nilijibu mwenyewe kwa sababu lina siasa kubwa, kwanza nitaanza na hilo suala kusema kwamba baraba zote Zanzibar zilizojengwa anapewa *MECCO* hiyo sio kweli, kuna *H. Yang* wamejenga njia nyingi tu kule Pemba na kwengineko, lakini ni kweli kuna rekodi inaonyesha kwamba kampuni ya *MECCO* huwa inashinda shinda zabuni zakujenga njia hili

linatokana na kwamba hii kampuni ya *MECCO* mwenyewe ni mtu wa hapa hapa anaijua kampuni ya *MECCO* vizuri *MECCO* ilikuwa kampuni ya Serikali zamani ya wananchi *Engineering Company* huyu anafahamu hii *Market* ya nchi yetu viuri na wakija watu wengine kuja kuingia katika hizi *Tender* kwa uzoefu nilioupata kwa muda mfupi tu nimekuta kwamba anawashinda wale wengine kwa sababu yeye anajua hali halisi ya gharama zile za ujenzi na nyenginezo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie na niihakikishie Kamati hii na Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba hakuna mchezo mchafu wowote unaofanywa wa kuhakikisha kwamba kampuni moja tu itakuwa inashinda dhabuni hizi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa nafikiri itakuwa inatosha hiyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: La pili Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako suala la viwango vya barabara unapotoa hizi dhabuni kuwapa wakandarasi wajenge njia tunakuwa tunakubaliana kwamba wanaweka *Performance Bond* ya *10 percent* wanaweka, halafu kuhusu habari ya viwango vile kwamba tunapata *warrant* wa muda gani tumesema tunapata *Warrant* wa mwaka mmoja tu wengi hawakubali kutoa *Warrant* wa zaidi ya mwaka mmoja, kwa hivyo kwnye hilo niliwahi kusema Mhe. Mwenyekiti kwenye baraza lako tukufu kwamba tunafanyia kazi kwamba tutapotoa zabuni miaka ijayo tutajaribu kuongeza huu *Warrant*.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa nafikiri itakuwa inatosha kwa sababu Kanuni inatutaka tuwe *Brief* kidogo mwenye kuuliza na mwenye kujibu vile vile Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba leo kwa sababu ramadhani tutaenda mpaka saa 12 tusifanye haraka…..

Mhe. Mwenyekiti: Hatutafika huko Mheshimiwa hatutaki hivyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina nia njema safi kabisa na Mheshimiwa Waziri alikuwa yuko Itali wala hii Wizara alikuwa hayupo, mimi simlaumu lakini ninachotaka kujua mimi nchi zote *International* wanaojenga barabara na mijenzi mikubwa wanakuwa na *Guarantee* ya *Bank* au ya Wizara husika, sasa *MECCO* au kampuni nyengine yoyote iliiyojenga hapa kwa nini tunawapa mwaka mmoja wakati barabara dunia nzima watu wanapewa miaka mitano, sita mpaka kumi halafu kuna *Security* inakuwepo wanaambiwa waiweke kwa muda fulani itapokuwa kitu kipo *okey* anarejeshewa mwenyewe kwa nini hapa hakufanyiki matokeo yake njia zinafanya matuta zinachimbuka.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi tu nasema utaratibu huo tunao na kwamba akija mkandarasi kujenga njia akishamaliza ile njia tukishapokea ile njia anaweka asilimia 5 gharama za kujenga njia anaweka benki kule muda wa mwaka mzima tunaangalia kama kuna matatizo, yakitokezea tunatumia pesa zile kufanya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Nadir tutakuwa tumemaliza nadhani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Naomba aendelee Kamanda nimemruhusu bwana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia fungu lakini nilitaka ufafanuzi wakati nachangia kuhusiana na fungu la SP 010104 Huduma za Usafirishaji, nilitaka kujua kwamba thamani ya bei ya Meli hizi ambazo zinataka kununuliwa yaani kuna Shilingi bilioni 18 hili fungu lina bilioni 18 na milioni 800 meli hizi nilitaka kujua thamani yake.

Lakini pia nilitaka kujua hii meli ya abiria itakuwa na uwezo wa kuchukua abiria wangapi pamoja na tani zile za mizigo, lakini pili nilisema kwamba meli ya mafuta itakuwa na uwezo gani wa kitaalam wa kupokea na kutoa mafuta bila ya matatizo yoyote Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sisi tupo katika hatua za awali za ku-*design* na baadae kupeleka michoro baada ya kutangaza *Tender* kwa wahusika kwa hivyo mpaka sasa hivi tumetenga hichi kiasi kwa kukisia, kwa sababu tukichukua zile *Experience* tuliyoipata kutokana na MV Mapinduzi, kwa hivyo mpaka sasa hivi hatujajua kiasi gani za meli zozote lakini hichi ni kiwango ambacho tumekiweka ili baadae, kwa sababu hii meli tutakapotengeneza zote mbili tutalipa kwa njia ya mkopo, kwa hivyo tuaanza kutengeneza kabisa hizo pesa ili baadae tukianza utengenezaji basi na hizi pesa tumeshaziweka kabisa Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bi Panya Mhe. Asha ulisema kwamba hukuwa na nia ya kuzuia fungu sasa hukupaswa kunyanyuka, Mhe. Bi Panya.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nichuku fursa hii kwanza kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri anajitahidi kutoa majibu kwa ufafanuzi lakini na mimi nilitaka kujua kitabu kile cha mwaka jana kilikuwa kinaonyesha vipaumbele vya barabara ikiwemo barabara ya

Matemwe, sasa kitabu hichi cha mara hii kinaonyesha tu barabra mbali mbali na hii barabara ilikuwa ni miongoni mwa ahadi za Mhe. Rais wakati wa mwaka 2010/2015 na mpaka muda huu bado barabara hii nilitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwapa matumaini wananchi wale wa Matwemwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi tu katika barabara zetu za kilimota 52 barabara mojawapo ni hiyo barabara tunayoiita Matemwe/Muyuni, barabara ya kuanzia Bububu kwa Nyanya mpaka Mkokotoni, Pale Kiongele na huku Fuoni Kisakasaka.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mheshimiwa nashukuru na kwa majibu haya mazuri ambayo yanawapa wananchi wetu matumaini makubwa Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niungane na wenzangu wote kwamba sina nia ya kuzuia fungu lolote isipokuwa nataka ufafanuzi tu kwenye hapa HP…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Makame Ali huna nia ya kuzuia fungu unatupotezea wakati kwa sababu majibu aliyojibu Waziri najua ulikuwa unauliza kuhusu wapi hapo alikuwa anapataja sana Mheshimiwa kajibu hapa nilikuwa nasikiliza, sasa kama huna nia ya kuzuia fungu waachie wale wanaotaka kuzuia kwa sababu hapa unyanyuke kama ulitia nia ya kuzuia fungu tu, nilimruhusu Asha lakini baadae nikajilaumu tunajaribu ku-*save* wakati waheshimiwa, wengine wanasema tutaondoka Saa. 12.00 hatutaki tuondoke saa 12.00 sasa msitake kunyanyuka hapa ili Waziri ajibu yale ambayo kesha yajibu pale tusipoteze huo wakati Waheshimiwa tujihurumie sisi wenyewe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nikitaka nipate ufafanuzi tu kwenye hili suala nililomuuliza kwamba kuna Shilingi bilioni 2 kwenye utengenezaji wa barabara ile ya Madenjani/Mzambarauni, sasa nataka kujua kwamba ile barabara imeombewa pesa hivi hapa lakin imeshafikia hatua ya kumalizika barabara ile sasa nataka nipate ufafanuzi tu kwamba kuna nini hata imebidi pesa hizo ziombewe tena kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Suleiman Makame ni kweli ile barabara tumeijenga kwa mkopo na hivi sasa tunategemea katika bajeti ijayo mkandarasi kakubali tumlipe, kwa hivyo ndio maana ukaona tumetenga bilioni 2 katika kipindi hichi, lakini tumejenga kwa mkopo hatukumlipa chochote mkandarasi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri pale aliponiambia kwamba skuli zile zitabaki Vikokotoni na Darajani nikupongeze sana na ile nia aliyokuwa nayo kwa upande wa Mji Mkongwe niachie mimi….

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kidogo kipi unakihoji Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu katika kifungu PP0101 SP 010104 Huduma za usafirishaji Usimamizi wa Shughuli za Meli na Uwakala, ahsante Mhe. Mwenyekiti hapa nataka nizungumze kidogo kidogo ili nieleweke maana yake hapa ni pahali pazito sana hapa Mheshimiwa, Mheshimiwa kipindi kilichopita mwaka 2013 tulipitisha sheria na nitaomba niinukuu Mhe.Mwenyekiti na waliosoma Kiingereza watanisaidia maana yake nilisema mimi elimu yangu ni dogo *Every ship of a Tanzania Zanzibar shipping will provide and a minimum of two buck for purpose of practical sea training of Tanzania Zanzibar trams sea there of which register vessels* nini maana yake. Mheshimiwa maana yake ni hii nilifikiria nitapata mtu atanisaidia lakini sikupata.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa ufupi Mheshimiwa nenda kwenye hoja hiyo hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Maana yake kwanza tuje kuona hoja Mheshimiwa hapa pazito sana kila meli wapatiwe nafasi mabaharia wa kazi Wazanzibari wasiopungua wawili kwa ajili ya mafunzo ajira, ndio ajira zenyewe tunatafuta ajira tumesajili zaidi ya meli 300 au 400 mwaka jana tu 186 sasa hivi tuna karibu 360 na hii ni sheria, huku tunalalamika wapiga kura wetu hawana kazi. Naomba muongozo wa kiti chako vyenginevyo sitoeleweka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti kama tulivyojibu mwanzo kwamba kuna baadhi ya mikataba ambayo sisi tunataka wenzetu wabunge waridhie ili baadae sisi fursa kama hizi wanazozisema tuzipate, kwa hiyo mimi namuomba sana Mheshimiwa Mjumbe awe na ustahamilivu lakini suala vile vile linaingia katika mambo ya Muungano. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti hapajajibiwa kitu, hii ni sheria si maneno yangu Jaku tumepitisha hapa mwaka 2013 itakuwaje Wazanzibari wetu vijana wamesoma vyuo vipo, halafu tunakuja tunawadanganya hii ni ajira iko wazi wazi haitaki hata tochi, zaidi ya vijana mia 700 mpaka 1000 sasa

wangepata kazi na hii sheria tumepitisha, si maneno ya Jaku Mhe. Mwenyekiti. Sheria tuziheshimu 99(a). Tena ina *capital* A kubwa tumepitisha hapa, sasa tukiachia mambo kama haya tutazoea huku Serikali inalalamika ajira hamna hawa wapiga kura wetu, zaidi ya 700 mpaka 800 na sheria si maneno ya Jaku Mhe. Mwenyekiti, nataka *commitment* aliyesajili Meli hizi awambie kwamba kuna sheria hii kaisahau ili tujiridhishe vyengine vyote hatuwezi kuchezea hii ni sheria, sio maneno ya Jaku Mwanasheria Mkuu nisaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. usirudie hayo kwa hayo tena, Mhe. Mwanasheria Mkuu tafadhali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru masharti ya sheria yatabaki kuwa masharti ya sheria na kila ambaye yanamgusa itabidi ayafuatwe yale masharti ambayo sheria inataka, nadhani Mhe. Naibu Waziri amejibu vizuri kama atalifuatilia na kila ambaye anahitajika afuatwe yale masharti ya sheria basi masharti haya yatafuatwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa hili si langu tupo kwa nia njema tunajenga nchi yetu na hii ajira iko wazi Mhe. Mwenyekiti haitaki tochi kwa nini wakasajili kila kitu sheria toka 2013 zaidi ya vijana 700, mpaka 1000 wangepata kazi sheria ndio hii anasema Mhe. Mwanasheria Mkuu asimamie huyo aliyesimamia hakujua kuwa na sheria watu wawili hawa kulikuwa na watu watano, tukaja mpaka wawili Mhe. Mwenyekiti, kwa nini tukapoteze ajira kama hizi na hii ni sheria na hichi chombo cha sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ushasikika Serikali italifanyia kazi hilo tunaendelea. Naomba sasa kumwita Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda katika kifungu vitatu nataka nizuie. Katika hii programu kubwa ya PP0101 sasa HP01010101 Kuhusu ujenzi wa barabara.

Katika mchango wangu wa maandishi niliandika kuhusu kadhia yangu ya barabara ya Mpendae – Jang'ombe wakati tunazungumzia Wizara Tawala za Mikoa wakanambia watakaa pamoja, itakapokuja Bajeti ya Wizara hii ni pahala pake kulisemea nataka jibu la Serikali kuhusu kadhia ya barabara yangu ya Mpendae – Jang'ombe ambayo imetolewa milioni 100 na Mhe. Mbunge wa pale lakini jibu mpaka lake bado halijakuwa nimeambiwa inasubiriwa lami, lami imekuja kwa barabara nyengine nitaomba hilo sijajibiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba ukae ujibiwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mimi nna imani kubwa sana Mhe. Mwenyekiti Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Idara Maalum ya Vikosi vya SMZ alipokuja hapa alitoa majibu ya ufafanuzi, akasema hili suala tutalifanyia kazi. Sasa naomba atuamini kwamba tutalifanyia kazi na tunasema katika Baraza hili Tukufu na tunalolisema tutalitenda kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani atupe muda na hiyo kazi tutaifanya ili kuhakikisha ile barabara tunainusuru. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana najua tu wakati wa kupitisha Bajeti na baada ya muda si mkubwa itapitisha bajeti, anambie bajeti gani itakayojenga ile barabara kwa sababu muda ushakuwa mwingi na Balozi shahidi wa kupokea milioni mia kuhusu ile barabara sasa hivi haipitiki. Kwa hiyo lazmu isiwe hapo mbele mkatujibu majibu wa kisiasa kwamba tutaanda, tutajipanga hivi na hivi nataka *commitment* Serikali barabara ile itatengenezwa bajeti ipi hiyo ndio nitakayoondoka nayo na nijue iko katika miundo mbinu sio tena kwenye Tawala za Mikoa. Nataka *commitment* ya Serikali barabara ile itatengenezwa bajeti ya 14-19/19-20 halafu tuendelee nikipata hiyo *commitment*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti barabara ile ilibakia sasa hivi kutiwa lami na tumeagizia lami kwa sababu kuna upungufu wa lami sasa hivi, basi itakapokuja lami tutakaa na Waziri mwenzetu tutaangalia tuifanye hii kazi, ni suala la kuwekwa lami na wafanyakazi tunao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Diaspora najua unazo nyengine Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, hii katika hili kanambia itakuja lami mimi *commitment* kwamba kwenye bajeti ya 17-18 nitahakikisha barabara ile imetengenezwa asinambie itakapokuja lami, kwa sababu lami tokea imelipwa ni siku nyingi aji-*commit* yeye kwamba barabara yako.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. samahani Mhe. naomba ukae, Mhe. hiyo barabara yenyewe mpaka awasiliana na Waziri mwengine hii inaonekana sasa unalazimisha lazima la Fungu la Wizara nyengine, lile kwenye Wizara yake inabidi washirikiane na Waziri wa Tawala za Mikoa wataifanya hiyo shughuli ndio maana hilo fungu unalodai hulioni, huoni kwa sababu hiyo nitakuwa lipo sehemu nyengine na sharti tuwe *reasonable* kidogo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. hili suala alilizungumza kwenye Ofisi za Tawala za Mikoa lakini Mhe. Waziri kanambia hili suala si la kwake pale ndo niliposima, akanambia suala hili njoo ulihoji kwenye miundo mbinu kwa hivyo *automatic* yeye si la kwake halimuhusu tena. Ndio maana nikakamata hapa wala hashirikishwi Tawala za Mikoa, Tawala Mikoa keshanawa katika hili kwa hiyo nipate *commitment* ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri naomba msaidie.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyosema zile barabara za ndani na ile barabara kama nilivyosema sisi ndio tulioanza kujenga sasa tutakaa na wenzetu lami itakapokuja tutafanya hiyo kazi. Lami itakapokuja inakuja katika bajeti hii tutafanya hiyo kazi atustahamilie.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri majibu mazuri hatuhitaji kuendelea tunaendelea Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nachangia nilionesha nia ya kutumia kifungu Nam. 111cha kuunda Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti utafiti tulionao sisi wengi huku *backbencher* tumebaini kuwa Kampuni ya MC Abdalla ni Kampuni ya kuhushi na ilipewa *contract.*

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani unacho hoji hapa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ninacho hoji Ujenzi wa barabara HP010101.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. hicho huwezi kukihoji kwa sababu washatimia watu watatu, wanakizungumza hicho hicho.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, wa pili Mhe. Abdalla Maulid Diwani mimi ndio watatu, nimeisabu vizuri sana Mheshimiwa kama unataka nisikilize kiti chako sina maneno lakini nimefuata vizuri sana Mheshimiwa wewe ndio Mwenyekiti hapa lakini mimi.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir alihoji hiyo hiyo. Au vipi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Wa kwanza wa pili Mhe. Abdalla Maulid Diwani wa tatu mimi kwa sababu naandika wote walosema hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bi Panya alihoji kitu gani.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hakuhoji hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Ilikuwa hiyo hiyo HP hiyo hiyo barabara unajua mnapohoji Mheshimiwa sisi kwenye kitabu tuna-*note* au sisi tunaweka *dot* mtu wa kwanza mtu wa pili mtu wa tatu. Na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ndio kakibeba hicho unacho chengine nitakusikiliza hicho cha barabara kiache.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nakwenda HP010103 Uimarishaji wa Miundo mbinu ya Barabara hapo hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. barabara.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. katika fungu hilo hilo.

Mhe. Mwenyekiti: UUB kwa hiyo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilisema nina dhamira ya kuundwa Kamati teule kwa sababu hiyo Mhe. sisi *backbencher* wingi wetu tunaufiti ulokamilika kabisa hii Kampuni MC Abdalla haikuwepo wakati huo na wala haipo na ndio maana nilidai *copy* ya usajili ya Kampuni. Aidha *limited trader* nilidai *copy*. Pia nilidai *Certificate* ya *Tin* namba yake ya Kampuni, pia nilidai *copy* ya vyeti vya *registration* ya Kampuni hii Mhe. kwa kujua kwamba hii Kampuni haipo. Vitu vyote sikupewa basi Mhe. Waziri alinijibu Kampuni hii imekidhi vigezo vyote ndio majibu aliyonambia Mhe. Waziri.

Lakini tunao utafiti hii Kampuni haikuwepo ni kampuni ya kuhushi iliyoletwa na wajanja wachache na pesa wametia mifukoni mwao. Ndio maana Mhe. Mwenyekiti nimeomba kuundwa Kamati Teule tukaichunguze Kampuni hii ili twende sambamba na Serikali matakwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wale wote wanaojifanya wajanja tuweze kuwafanyia kazi. Naomba Mhe. Mwenyekiti kuunda Kamati Teule kwa sababu hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti mimi nataka kumtoa wasiwasi Mhe. Mjumbe hapa kwa sababu tayari hili suala lilipokuja Wizarani kwetu nilihojiwa na PAC na nina imani katika ripoti yako Septemba, Oktoba *PAC* wataleta majibu baadae kama hatoridhika basi mimi nashauri iundwe hiyo Kamati Teule.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. nashukuru tuunde Kamati Teule naomba utaratibu ufuatwe, tuunde Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa, Mheshimiwa amesema *PAC* wameshalichunguza suala hilo na litakuwemo kwenye Ripoti yao, sasa baada ya kusomwa hiyo Ripoti ya PAC kama tutakuwa hatukuridhika yeye asiruhusu, Kamati Teule bado ya Spika mimi nina mamlaka ya kuikataa vile, anaweza akakubali Waziri miye nikaikataa. Kwa hiyo mtapokuwa mmeridhika au hatujaridhika wakati huo tutaangalia *feasibility* ya kuelekea huko unakotaka kwenda. Lakini kwa sasa hivi suala la Kamati Teule halipo kwenye hilo. Naomba ukae Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: (Dimwa) Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana mimi nilikuwa nakwenda kwenye HP 01010302 Uimarishaji na Miundo Mbinu ya Huduma za Usafiri wa Anga.

Nilipokuwa nikichangia nilieleza azma yangu ya kuwa Kamati Teule au nizuie fungu hili moja ambalo lilinisukuma huku kwa sababu Serikali tayari imeshatumia pesa nyingi sana katika Uwanja wa Ndege mpya na wakati nikichangia nilisema bora tuieke makumbusho au sehemu ya kumbukumbu kwa sababu Serikali ilishindwa kulijenga jengo lile tena. Na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kinidhamu, wale waliokosa au waliofanya mambo yale nilikuwa nataka ufafanuzi zaidi ili kuweza kujua na nilishauri na nilishawishi Baraza lako sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nina imani kubwa sana Mhe. Mohamed Said (Dimwa) majibu tuliyoyajibu hapa yametosheleza na nina imani kubwa sana ameangalia namna gani juhudi ya Serikali ilivyochukua mpaka tukafikia hatua ya hapa tulipofikia, namuomba sana kwa hivi sasa hili jambo tushafikia hatua hiyo. Kama ushauri ulivyotoka kwa wajumbe hapa kina Mhe. Miraji na wengine tuangalie hapa tulipo ili hili jambo tulikwamuwe, tuwaunge mkono wenzetu, wenzetu wamechukua *concern* zote mpaka kuja kuridhia namna gani ya kuendeleza huu mkataba kisha leo Tuunde Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti wale ambao wanataka kutusaidia katika hili kulifanikisha watatuona sisi wa maajabu, namuomba sana Mhe. Mohamed Said (Dimwa) yeye anajua namna gani alikuwepo kipindi kilichopita na wao walivyofika na sisi tulivyofika atuachie hii kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Naibu Waziri kuwepo kitu chengine na kutokuwepo kitu chengine, mtu yoyote anaweza akawepo mbele akawepo nyuma tunachozungumza hapa ni *Airport*, Mhe. Mwenyekiti tumetumia milioni 128 *dollar* lakini safari hii tumeombwa kutumiwa bilioni 56 za wananchi walipa kodi hatukuwafanya chochote wale

walioharibika na upotefu au uharibifu ule wale wa mwanzo wala hatukusikia chochote. Hichi si kitu rahisi kama tunavyofikiria mimi bado nitaendelea kulikamata fungu hili.

Mhe. Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, inaonekana Mhe. Mjumbe alikuwa hakufuatilia mpaka sasa hivi nataka kumfahamisha kwa mujibu tulianza Oktoba 2010, Mkandarasi alipatiwa *dollar* ishirini na moja milioni laki moja na ishirini elfu na Novemba 2011 kapatiwa dollar kumi na nne elfu na thamani elfu kwa hivyo *dollar* zote mpaka sasa hivi zlizopatikana hapa ambazo zimetumika ni *dollar* 35,200,000 milioni si kama alivyosema. Lakini gharama zote mpaka itakapofika ndio hiyo sasa pamoja na utengezaji wa *apron* na mambo mengine na jengo litatumia *dollar* milioni 128 namuomba sana Mwenyekiti awe anafuatilia sana wakati ninapojibu. Kwa hivyo si kwamba 128 tumetumia mpaka sasa hivi tumetumia *dollar* 35,200,000 milioni. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti huwa sisemi kwa kubahatisha nina *document* hapa ambazo zimetumika na nina uwezo wa kukupa na kuzichukua sasa Mhe. akisema sifuatilii nafuatilia, na nafuatilia kwa sababu pesa inayotumika ni pesa ya wananchi, wavuja jasho leo hakuna hata chochote ambacho tunakifanya angalau huyu basi kasababisha hasara hii tumpeleke Mahakamani huyu kasababisha hasara hii tumnyonge, maana yake hivi vitu ambavyo tunaingia moyo wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshanga kanambia ana *document* wakati sisi Wizara husika ndio hayo malipo ambayo wenzetu *AZIK Bank* waliofanya na sisi tulikuwa huko China, sasa hii *document* yake imetoka wapi. Mimi namuomba sana Mhe. Mwakilishi hili Baraza Tukufu anaposema kwamba ana *document* nataka atupe uthibitisho kazipata wapi *document* hizo wakati hapa malipo haya yamefanya Serikali. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Mohamed Said (Dimwa) ni mwenzangu na yeye alikuwepo Serikalini lakini anambie *document* hizo kazipata wapi ili tuwachukulie hatua waliokuwa na *document* feki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. mimi nafikiria hatuna haja ya kwenda huko mimi ningemuomba Mhe. Mohamed Said (Dimwa) ukae na Waziri pamoja na Watendaji ili muone namna ambavyo tunaweza kusaidia ku-*solve* hili tatizo. Kwa sababu hili tatizo linagusa pia wahisani nje. Sasa tusije tukalichafua maana mimi *concern* yako naiona ya matumizi mabaya na kuna watu wamefanya ubadhirifu na lazima waadhibiwe lakini twende taratibu maana lilipofika kila mmoja ana hamu lile jambo limalizike ili tuanze kupatumia pale mahali. Lakini sasa tusianze kutafuta vitu ambavyo vitasababisha twende

taratibu.Kwa hivyo nakushauri sana Mheshimiwa hebu kaa na Wizara halafu tena mkae na Waheshimiwa Mawaziri mkae msikilize pointi anazozungumza, sishawishi tuunde Kamati Teule lakini nasema tukae nae ili tupate mashirikiano yake ili tuweze kulikwamua hili jambo liende. *(Makofi)*

Sote tuna hamu nalo lile jengo tushachoka kwenda pale siku hizi limekuwa kama jumba la ndege *Airport* yetu kila baada ya muda mnafanya matengenezo tushachoka tunataka jengo jipya. Mhe. Mohamed Said (Dimwa) nakuomba sana. Hapana Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nimekufahamu sana isipokuwa Mhe. Naibu Waziri asitutishe kwa kusema tunaleta *document* tutazileta kama kawaida lakini nasema tu acha tuendelee kwa busara yako ambayo umeitumia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. tunaendelea. Samahani Mhe. Abdalla Maulid Diwani au kulikuwa na maelezo anayo nani Mhe. Issa Haji (Gavu) hapana Mhe. Abdalla Maulid Diwani twende.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza sana kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa katika hii nakwenda katika kifungu cha HP 01010401 ambalo mwazo alikamata Bi. Asha tu. Kuna tafauti za mahesabu kwa mujibu wa hii ilivyo hapa, katika humu kwenye kitabu ukurasa 45 ilikuwa nilifikiri kuna milioni tumeambiwa kuna milioni 20,000,000 lakini humu 18,000,000 kulikoni kuliko hicho. Humu kuna *twenty million* huku *eighty million.*

Mhe. Mwenyekiti: Ushafahamika Mhe. Mheshimiwa Waziri Milioni 2,000,000 ziko wapi.

Mhe. Naibu Waziri Ujenzi na Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. kama nilivyosema sisi tunakwenda kwa mujibu wa vifungu wa hichi kitabu kwa hiyo maelezo yalikuwemo humu ni sahihi na kwenye kitabu kilikuja taarifa wakati kitabu kishachapishwa lakini Mhe. Waziri alielezea kwamba ni milioni 18,00,000 badala ya 20,000,000.

Mhe. Mwenyekiti: Wamesahihisha kwenye maelezo imekaa sawa hiyo Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. nilipokuwa nachangia pia nilitumia kifungu cha kuzuia fungu kuhusu nasimamia HP01010401

Mhe. Mwenyekiti: Una bahati mbaya sana Mheshimiwa watu watatu tayari. Ehe Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti mimi nitaenda kwenye SP010103 halafu HP01010 hapa nilizungumzia suala hili hili. Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano Mhe. Waziri wa Fedha kuna watu wamefanya ubadhilifu kwenye Wizara yake kaweza kuwasimamisha na kuwachukulia hatua. Kwa nini kwenye suala la *Airport* waliosababisha hasara tusiunde Kamati Teule tukenda tukawachunguza fedha tunaweza tukaruhusu zikaenda lakini wakubali tufanye Kamati Teule ya kuwachunguza waliofanya ubadhilifu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo tumeshalimaliza naomba ukae *please*, *please* nakuomba ukae. Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu PP0101 Miundombinu ya Huduma za Usafirishaji 210,957,913,000
Kifungu PP0102 Programu Kuu ya Uhifadhi

Mhe. Mwenyekiti: Asante naona watu wanne nitaanza na Mhe. Panya Ali Abdalla nitakuja Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Nadir Abdul-latif, Mhe. Dimwa, Mhe. Omar Seif Abeid**.**

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika kifungu hiki nilikuwa nina hoja katika Wakala wa ujenzi ambapo inaonyesha azima yake nikufanya majengo mazuri na uhifadhi mzuri kupatikana.

Hoja yangu iko katika jengo la Wizara ya Fedha Pemba ambalo jengo linaonekana liko vibaya sana. Wizara inampango gani wa kulivunja kiutaratibu lile jengo ili lisijelikaachiwa likavunjika lenyewe likaja likaleta athari au madhara kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Wakala wa Majengo ndio wanaoshughulikia majengo yote ya serikali. Tutakaa na Wizara ya Fedha ili kuangalia utaratibu namna gani lile jengo la kulifanya lisilete athari. Kwa sababu mkandarasi aliyeshughulika na jengo kama mnavyojua yaliyotokezea, lakini namuomba Mhe. Panya atuwachie tukae na Mhe. Waziri wa Fedha kuliangalia hili jambo tunalimaliza vipi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, sisi wengine hatuna tabu lakini tunachotaka tunapotoa hii tahadhari kabla ya athari tunaomba tusikilizwe kwa kuhofia kutokea mengine. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kuna msemo unaosema huruma hailei mwana. Nije kwenye Mji Mkongwe tena. Waziri alipokuwa akijibu, nimesimama ili kuweka *hansard* sawa. Ili suala Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa likininyima usingizi kwa muda mrefu la Skuli ya Vikokotoni na Darajani kwa muda mrefu na msema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba nikuulize ulipokuwa ukijibiwa ulikuwa ukishangiriwa kwa kupiga makofi kwa maana ulikuwa umelikubali. Sasa unazuia kifungu kwa sababu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sithubutu kuzuia kifungu mimi nimesema humu, nataka aweke *hansard* sawa tu.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana Mheshimiwa keshasema, ipo kwenye *hansard* hicho alichokisema Mheshimiwa kipo kwenye *hansard* tukikitaka tutakipata kwa hiyo wala usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa naona una wasiwasi usiwe na wasiwasi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Siyo hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio najua wasiwasi ndio akili.

Mhe. Jaku Hashim: Ndio akili, bora kuweka *hansard* sawa watu wanataka kujua.

Mhe. Mwenyekiti: Ipo kwenye *hansard* tayari naomba ukae naomba tuendelee. Naam.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Katika kitabu chake.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ujenzi wa matengenezo wa nyumba za serikali au usimamizi wa utoaji wa jengo. Katika kitabu humu kuna majumba mabovu na serikali kwa kweli miaka imeshapita wala hakuna dalili yoyote wala harufu yoyote kutaka kuyatengeneza. Nilimshauri mimi wenyewe wanayataka yale majumba wauziwe na wenyewe wenye mali zao wapo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri umefahamu sijui.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu. Nimemfahamu alivyosema Mhe. Waziri kwamba

uhifadhi wa Mjimkongwe unataratibu zake na mambo yote lazima yaende UNESCO. UNESCO wanavyotukubaliana kitu sisi tunakuwa hatuna uwezo wa kupinga. Wakisema hapa mjenge hapa msijenge tunawasilikiliza.

Kuhusu hayo anayosema sisi tuna utaratibu kwamba nyumba zote za serikali sisi ambazo zipo kwenye milki zetu basi tutazifanyia ukarabati sisi wenyewe, hatuuzi nyumba zile. Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, ningeomba kutoa maelezo yafuatayo. Kwanza serikali huwa haizuii jengo lake kufanya matengenezo wakati wanapofuata utaratibu wa kisheria. Lakini kwa majengo ambayo serikali imeyataifisha rasmi majengo hayo ni mali ya serikali na hayana ulazima kwa serikali kumuuzia mtu fulani. Ni pale tu ambapo serikali ikiamua kuyauza itaamua kuyauza kwa utaratibu wake. Na ikiwa haijaamua kuyauza maana yake itaendelea kuyatengeneza kwa utaratibu wake bila ya kulazimishwa na mtu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo ieleweke wazi kama unakaa hata kama nyumba hapo awali ilikuwa yako lakini imetaifishwa na serikali hiyo nyumba siyo yako ni ya serikali na sasa unakodishwa kwa utaratibu wa kiserikali na kama serikali ikiamua kuitengeneza itaitengeneza kwa utaratibu wake kwa wakati wake kwa uwezo wake kwa mujibu wa bajeti yake. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimemsikia mtaalamu sana Mhe. Mohamed Bin Aboud lakini ajuwe serikali ndio watu na watu ndio serikali leo serikali ingekuwepo ingetawala nini miti? Ng'ombe? haya majibu wayafikirie, hii nyumba imeshaanguka iko nchini miaka na miaka. Ndio ile hadithi yangu Mhe. Mwenyekiti, nyoka wa mdimu hukaa kwenye mdimu hana kazi nazo ukenda kuchuma anakurukia.

Mheshimiwa hebu ulizeni, tuna kazi 2020 imetukabili mbele yetu, nyumba ipo chini miaka 30 haipo, mwenyewe yupo tena anakaa hapa hapa ni mzalendo anataka arejeshewe, anaijenga hapa hapa. Tunafanya nini na nini faida yake. Mimi ni mtumishi na mjumbe hauwawi, tuendelee. Mimi wananchi wameshanisikia, tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi ningekuwa na ombi kidogo kutoka kwako. Mheshimiwa kwa kweli huu mfumo uliopendekezwa unatuchanganya kwa ufupi. Kwa sababu hii *system*

tunayokwenda nayo kama mimi nina hoja karibu 12, halafu unanambia kwenye kifungu kama hichi kizima niongee hoja moja. Sasa ningekuomba kwenye fungu hili nina mambo mawili tofauti. Itakuwa kama la *Airport* limeruka bila ya kujijua.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ongea moja tu halafu nitakuruhusu hilo jengine kwa wakati mwengine.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Halafu chengine niendelee...

Mhe. Mwenyekiti: Hebu nenda kwenye hoja moja kwa moja, jambo moja tu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Hivi Mhe. Mwenyekiti, itakuwa tunabanana kweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilizungumzia suala la wale jamaa waliofanyiwa utapeli wa ile nyumba. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kanihakikishia kwamba hili suala tutalimaliza lakini naomba atoe kauli kwamba tutakaa mimi na yeye na watendaji waliofanya hivyo pamoja na aliyeuziwa nyumba halafu uwamuzi watoe, kwa sababu wale watu sio watu binafsi wamefanya kwa niaba ya Wizara wamefanya *officially* wizarani. Mimi nataka *responsible* yote wachukuwe wizara kama watawarejeshea nyumba au duka, lakini hawahitaji fedha wao wamedhulumiwa nyumba kwa kuuziwa kitapeli.

Sasa naomba Mhe. Waziri anipe jibu sahihi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mwenyekiti, alinipa hili suala mimi na sisi serikali tunakwenda kwa mujibu wa taratibu na sheria. Sasa hatuwezi kumuhukumu mtu ikiwa hamna uthibitisho, ndio maana nikamwambia tukae tulizungumze hili suala baadaye taratibu na sheria zifuate mkondo wake. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri ukae na Waziri umpe kwa ukamilifu wake.

Mhe. Nadir Abdul-latifu Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri alikubali akasema kama keshazungumza na wale watu watarejesha fedha watakubaliana, sasa hivi anasema hakuna ushahidi. Mimi naomba tutumie busara tusije tukaadhirishana humu ndani mimi ushahidi ninao, atumie busara kwa sababu mimi siongei kwa mdomo mimi nafanya vitu *research*.

Mhe. Mwenyekiti: Busara yake ndio amesema kwamba wewe na yeye mkae ili mli-*solve* hili tatizo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mwanzo kanambia wakakae hao watu watafahamiana, mimi nataka tukae mimi na yeye tumalize hilo suala.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hilo limekubalika halina matatizo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Haya.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, mimi nipo kwenye HP01020303 nilizungumzia wakati nikichangia majumba ya Kilimani na kadhia yake kubwa sana na matatizo ambayo wanayapata wananchi wa Shehia ya Kilimani, ubovu lakini na maji. Tulifanya ziara na Mhe. Naibu Waziri miaka mingi na hapa kanambia tutakwenda, tutafanya, tutahakikisha nilikuwa nataka kujua hususan *commitment* ya serikali, lini tutaanza kwenda kuwashughulikia wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mheshimiwa kama nilivyosema kuna bodi ambayo sisi pia tumeiombea iombea pesa zake basi mimi namuomba kwa sababu hivi sasa kwa utaratibu kama nilivyosema mwanzo, kuna nyingi ambazo zipo katika milki ya kibinafsi. Tulipokwenda tukasema tukae pamoja tushauriane pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ambaye alikuwepo pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba ili tuangalie.

Sisi pale kulianguka ngazi sehemu fulani Kilimani tukajitolea sisi kwenda kutengeneza na hili linawezekana sana Mhe. Mwenyekiti, atuamini kwa hilo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana ndugu yangu Naibu Waziri lakini hii kukaa tu, kwa sababu tumeshakwenda tukikaa sasa wanaanza kunipiga chenga, lini, kesho, keshokutwa, wote wawili mwisho wananambia mimi niende kwa Mkurugenzi. Mimi nina *responsible* gani ya kuonana na Mkurugenzi. Yeye ndiye amwite tuweze kuzungumza, wananchi wanapata tabu, pataripuka maradhi ya mripuko pale aliona yeye mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, anipe *commitment* ya serikali kuiokoa jamii ile ya Kilimani.

Mhe. Mwenyekiti: Kaeni nae, Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Mhe. Mohamed Said Mohamed

(Dimwa) anajali wananchi wake. Mimi namwambia tukae tutaliwasilisha hili jambo Wizarani tutaangalia namna gani ya kufanya hiyo *commitment*. Lakini linazungumzika na tunakubali kulifanyia kazi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza. Wakati nilipokuwa nikichangia nilihoji kidogo kuhusu jengo la Beit- al Ajaab mimi nasimamia SP01010202. Nilitaka nijue kuhusu Beit - al Ajaab tuliona kidogo na tuliambiwa mwaka jana kwamba kuna utaratibu wa kuliendeleza na sasa hivi linaonekana kama limesita. Nilitaka nijue hasa sababu ya msingi zilizosababisha kwamba jengo lile pamoja na mambo mengine kama ukarabati wake umesimama mpaka leo kuna tatizo gani la msingi ningeomba nijue hilo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mjumbe kama nilivyosema hifadhi ya Mjimkongwe ni urithi wa Kimataifa uko UNESCO, tumefuata taratibu zote, UNESCO wameshatoa kibali na tumeshakaa na serikali ya Oman basi na wao tumewasikiliza na wameshaleta *concern* zao, tunategemea katika bajeti hii ujenzi ule kuanza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa mimi nashukuru kwa majibu mazuri, lakini suala hili linaonekana kama halikuwa vizuri kwa hawa wa Oman lakini kama lipo basi mimi naomba Mwenyezi Mungu alijaalie liende. Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif haya narudi kwenye kile kingine.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekwenda kwenye HP01020201 uhifadhi wa Mjimkongwe. Nilieleza kwamba milioni 503 walizotengewa Mjimkongwe ni ndogo sana kwa mujibu wa kuweka hadhi nzuri ya majengo yale. Tukichukulia mfano jengo moja la Mjimkongwe kulifanyia *renovation size* ya ghorofa mbili basi utafanya *renovation* majengo ya kawaida matatu yana gharama kubwa sana. Imekuwaje hapa Mji ule wa kitalii ambayo majumba mengi mabovu halafu wamewekewa fedha ndogo hizi nikasema hapa nitazuia fungu litolewe sehemu fulani ili waongezewe. Lakini sikupata jibu.

Mhe. Mwenyekiti: Tuchukue kutoka wapi Mheshimiwa, yaani liongezewe kutokea wapi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kwenye utawala.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kumwambia kwamba watu wa hifadhi ya Mjimkongwe yale mamlaka kazi yao ni usimamizi, mambo ya majengo yapo kwa wakala wa majengo kwa hivyo hiyo siyo kazi yao. Hii tumewapa ruzuku kwa ajili ya kazi zao tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani umemfahamu Naibu Waziri wa Ujenzi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, labda linababaisha kwa sababu inasema hapa, Uhifadhi wa Mjimkongwe, Uendelezaji wa Mjimkongwe, sasa hichi kiswahili ukisema uendelezaji maana yake ni kuuendesha. Sasa kuendesha ni moja ya kuweka hali nzuri. Majumba mabovu lakini kama hizo fedha zipo sehemu nyengine basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu PP0102 Programu Kuu ya Uhifadhi na Uimarishaji wa Makaazi	1,645,312,000
Kifungu PP0103 Programu Kuu ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	372,557,000
Kifungu PP0104	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh nakupa nafasi ya kwanza ili usije ukawa una bahati mbaya, lakini subiri niwataje kabisa na wengine, atafuatiwa na Mhe. Mohamed Said (Dimwa), atafuatiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf tutamalizia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya mwanzo. Nasimama kwa HP01040201. Nilipokuwa nachangia nilisema kunako ZMA bilioni za pesa zilizotumika ni nyingi nikataka *breakdown* ya matumizi ya zile bilioni mbili walivyozitumia.

Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri wote wawili walivyojibu hawakuja na hiyo *breakdown* na nilisema nitazuia fungu hili. Mhe. Mwenyekiti naomba majibu ya *breakdown* mapesa haya ni mengi tumetumia, tumeambiwa kumejengwa Ofisi Dubai, wapi kwa bilioni hizi. Tunaomba maelezo ya kina zaidi ya pesa hizi za wakwezi na wakulima zimetumikaje bilioni mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwanzo alitoa maelezo hapa kuhusu namna gani pesa zilizotumiwa. Lakini kama anataka *breakdown* hiyo basi nitampatia

kwa sababu hili suala lilikuja mwisho na yeye alikuwa ni mchangiaji wa mwisho. Namuomba baadaye nitamletea maandishi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa baadaye utapatiwa hiyo *breakdown*.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti aweke *hansard* sawa mimi sikuwa mchangiaji wa mwisho kwa leo nilikuwa ni mchangiaji wa mwanzo kwa leo, kwa hivyo alijue vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa alichokusudia kwa sababu watu walichangia jana kwa hivyo walikaa pamoja na Wizara katika kufanya majumuisho katika kufanya majumuisho. Sasa ulipochangia wewe nafasi hiyo hawajaipata nadhani ndio alikusudia hilo Waziri, hana maana kwamba wewe ndio wa mwisho. Ni wa mwisho sio kwa umuhimu Mheshimiwa *please*.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nimechangia leo saa 4:21 kwa hivyo muda ulitosha.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa lakini ameahidi kwamba atakupatia hizo *document* zipo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kwenye HP01040301 Uratib wa shughuli za Wizara Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tangu mwaka jana nilikuwa nikisikitika sana barabara ya Gando Junguni watu wengi walikuwa hawalipwi pesa zao wale ambao wamekuwa wakibomolewa. Mwaka jana *hansard* ninayo Mhe. Waziri kanambiya kuwa hali ikiruhusu katika mwaka huu tutalipa sijui na mwaka huu utaruhusu naomba ufafanuzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti ni kweli kuna watu wa Gando, kuna watu wa barabara za NORAD vipando vyao. *Concern* hii tunaijua sana na tumesema sisi kwamba hili suala ni kubwa na sasa hivi utaratibu wetu kabla ya kutokea ujenzi wa barabara yoyote kwanza tunalipa mwanzo fidia tunalichukua na tutajitahidi mwanzo fidia. Tunalichukua na tutajitahidi katika mwaka huu wa fedha tuanza kulipunguza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanatupa matumaini.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilichangia kuhusu utafiti ulioweza kufanyika katika Muwekezaji wa Mtoni Marine ndugu Bakharesa. Pale tumaona kuna ujenzi unaofanyika wa Hoteli, na kwa sasa kumejitokeza matatizo makubwa majirani wa pembezoni mwa eneo lile.

Nilitaka kujua labda serikali inalielewa hilo kama tayari kumejitokeza athari pale, lakini kama inaelewa ni hatua gani ambazo wameshaanza kuzichukua ili kuona wanaidhibiti ile athari isiendelee na kama bado basi Mhe. Waziri atakubaliana na nami kwamba akimaliza bajeti yake hapa tuende tufuatane ili ikaonekana athari ile ambayo imewapata wananchi kutokana na ujenzi wa huyu mwekezaji.,Ttunamshukuru anajitahidi na anafanya uzalishaji mzuri na watu wetu wanapata ajira lakini bado katika hili utafiti nadhani haukufanyika wa kina bado inaonekana kuna athari baada ya kuziba yeye ile bahari athari inawapata wananchi wetu wanaingiliwa na maji kwa hiyo mimi nataka kujua kama Serikali inalijua hilo na hatua gani imechukuwa na kama hailijui basi ndio nilikuwa naomba hiyo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali kufuatana na Mhe. Panya alichangia kwa maandishi na miradi yote mikubwa kabla ya kutekelezwa lazima ifanyiwe utafiti wa mazingira, sasa kama kuna tatizo hilo basi tutakaa na watu wa mazingira tuhakikishe kwamba linatatuliwa hilo ili wananchi wasiathirike. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nashauri pamoja na yeye Mhe. Bi. Panya mungeshirikiana na Wizara ya Kilimo sababu ndio inasimamia masuala ya mazingira, Wizara ya Ardhi na Ardhi pia washirikisheni na Ardhi liwe mtambuka liguse kote. Mhe. Bi Panya.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na hekma ya kukuweka hapo moja ni hiyo kukuweka hapo moja ni hiyo ambayo unaitumia unatumia hekma kubwa sana. Ili kuona suala zima la Serikali yetu inafanikiwa na ikifanikiwa Serikali hii maana yake imefanikiwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa nakushukuru na naomba sana naomba hili sana naiomba Serikali yangu kwa umakini iliyonao tuchukuwe hatua ya kwenda kuona kwa sababu raha ya neema ikija basi na yale matatizo ambayo yataka kujitokeza tuwahi kuyadiriki mapema kabla hayaleta athari kubwa kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, HP01040202 Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara nilipochangia jana nilitaka maelezo ya barabara ya

Mitakawani na Kibondemzungu na imeahidiwa ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi hii hapa Miwani narekebisha kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Kasma yake iko wapi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: HP01040202 Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo ilikuwa iwe mwanzo Mheshimiwa siyo hapa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sijasikia Mheshimiwa

Mhe. Mwenyekiti: Yaani hilo jambo muda wake umepita lishapitishwa huku na kasma hamna hapa hiyo kasma haipo angalia hebu angalia vizuri kwenye kitabu Mhe. Jaku sikusikii Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuelimishane kidogo kidogo Mheshimiwa PP0104 njoo chini HP01040202 kinasomwaje.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu iangalie mwisho kuna 000 hakuna bajeti huko kuna sufuri hiyo hiyo ifate mwisho Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 182 kitu gani ngoja ngoja.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo ya kipindi kichopita msipige hizo meza waheshimiwa kipindi kilichopita hiyo Mheshimiwa kwa kipindi hiki haijawekewa fungu lolote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuwahi toka tunakotoka huko nyuma mimi nakumbushia tu Serikali iliahidi katika Ilani.

Mhe. Mwenyekiti: Yaani wewe unavyotaka sasa turudi nyuma nishakuelewa sasa sawa subiri wakujibu Mhe. Waziri kwanini hakuna pesa hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama ulivyosema Mheshimiwa katika kasma hii huku tayari tumezungumzia kuhusu Umarishaji wa Miundombunu na hii barabara ambayo anayosema yeye ni barabara ambayo inatokana na barabara zile tatu za Jendele mpaka Unguja Ukuu Kaibona na baadaye kuna hii barabara ya Jumbi/Koani na baadaye barabara Miwani mpaka Kizimbani kwa hiyo iko katika fungu lile. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Mhe. Jaku endelea nimekuruhusu useme.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa huu mwaka wa pili ndio yale nilokwambia Serikali wakati mwengine itakwambia tuko mbioni muda mfupi mwaka wa pili kama hiyo *issue* Miwani barabara ni muda mrefu na imo katika kipindi cha pili katika ilani na hakuna kinachoendelea kuna wazazi wanapata shida kule kujifungua kuna barabara Kibondemzungu nilizunguza jana tuzifikirie nazo wala haziko jimboni kwangu Mhe. Mwenyekiti za wapiga kura wetu hiyo mara mbili ishaahidiwa ya Miwani, hakuna kinachoendelea ndio ile hoja nilokwambia nikasema sheria tunazipitisha wenyewe tukisha tunazikiuka wenyewe humu ndani 2013 vijana wanataka ajira Serikali imeliona tunashindwa kuwashauri watu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Mhe. Waziri, Mhe.Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwanza barabara hizi zilipewa mkandarasi ambaye anajulikana kwa jina la Shapya alipewa mkandarasi ambaye anajulikana kwa jina la Shapya na ameshindwa kutekekeleza kazi hizi sasa hivi tumefungua naye kesi mahkamani kwa hiyo sisi tuliomshitaki kwasababu ameshindwa.

Lakini la pili sasa inabidi tena tuzi-*tendering* ili sasa watu waanze kufanya ile kazi. Kwa hiyo ndio maana zimechelewa kwa sababu yule mkandarasi mwenyewe alishindwa kufanya ile kazi. Sasa tulilofanya ni kuchukua hatua za kumshtaki lakini majibu ya Mhe. Waziri ni hayo kama sasa utaratibu huo unaendelea.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi niko hapo hapo lakini mimi sihoji kuhusu habari ya fedha kwa sababu nimeona fedha hakuna sina hilo, lakini wakati nilipokua nikichangia nilizungumzia tatizo lililojitokeza kwenye barabara ya Konde/Wete na nikaitaka Serikali ikangalie jinsi athari inayopatikana ya barabara kutoka na utumiaji mbaya wa watu wenye vyombo vya magari mazito wanaobeba mizigo zaidi ya uwezo wa barabara yetu, nilitaka nijuwe Serikali itachukuwa hatua gani kwa wale watu ambao wanaiharibu miundo mbinu ile ambapo Waziri wenyewe alipokuwa akijibu swali langu la ....

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tusikilizane kidogo endelea Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif Abeid: Wakati Waziri alipokuwa akijibu swali langu alisema kweli barabara ile imeanza kuchakaa Serikali imetumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kujenga barabara...

Mhe. Mwenyekiti: Jaribu kwa ufupi kidogo Mheshimiwa maana yake unatuhutubia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mimi wakati wa mchango wangu nillizungumiya...

Mhe. Mwenyekiti: Yote hayo yashafahamika nenda kwenye *point* yako hasa shida yako nini.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mimi *point* yangu nilitaka nijuwe Serikali ina mpango gani wa kuthibiti vile vyombo magari wanaobeba mizigo mizito yanayopita kwenye barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema sheria yetu ile inaelezea wazi kuhusu gari ya aina gani inatakiwa zipite na kwa tani ngapi sasa sisi hapa ni usimamizi tu wa hizi sheria na ninaomba sana Jeshi la Polisi liwe linasimamia hizi sheria na vile vile kama walivyosema wajumbe tutaweka alama ili kuonesha kwa mfano kama Mjini Mkongwe tani mbili zisizidi basi iwe vile vile na watu wasimamie zile sheria kwa mujibu inavyotakiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti mimi nashukuru kwa kauli hiyo Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia na mimi nilionesha nia ya kuzuwia fungu katika sehemu hiyo. Mhe. Wiziri wakati nachangia nilizungumzia suala la wafanyakazi wa Pemba ambao wanafanyakazi katika vyumba ambavyo ni vidogo sana na wanarundikana wafanyakazi wanne mpaka watano katika chumba kimoja na watu hao wanahudumikia watu mbali mbali wakiwemo madereva na makonda na nikakuomba unieleze ni lini utawafikiria wafanyakazi wako wale ambao wanaendesha wizara hizi kuwapataia jengo la kukaa.

Bajeti iliyopita Mheshimiwa ulinambia kwamba suala hili unaliangalia na utalichukulia hatua na pesa hizo umeshazitumia na sasa hivi nataka kukupitishia nyengine naomba unipe ahadi kwamba ni ni lini wafanyakazi wale ambao wanatukusanyia kodi utawaweka katika mazingira mazuri ya kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mwenyekiti, kwanza nimshukuru mjumbe kwa sababu yeye ni mdau mkubwa tulipita na kamati lakini nataka kumuarifu tu hivi sasa tuko katika namna gani ya kuwaimarisha sehemu ya Karakana na nina imani kubwa sana tumetenga fungu zuri la bajeti safari hii basi mojawapo ya mambo hayo kuangalia sehemu ile anayosema ili wafanyakazi wapunguwe msongomano. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Waheshimiwa hizi pesa ni nzuri na mara ile alinambia kwamba ataangalia hivyo hivyo na mpaka sasa hivi hajatekeleza hata moja na wafanyakazi wale bado wanapata kadhia nzito ya kufanya kazi katika eneo dogo, nakuomba Mheshimiwa utowe ahadi hasa safari hii ni lini hasa wale watu wa Idara ya Usafiri na Leseni utawapatia eneo ambalo itakuwa wanafanya kazi katika afya nzuri na usalama wa afya zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema kwamba tuna *concern* hiyo kwa sababu tunajua hata huku kamati ilipokwenda Unguja pia kuna matatizo kama hayo mimi namuhakikishia kwamba katika bajeti hii basi tutaangalia kupunguza ule msongamano kwa hiyo asubiri tunavyoingiziwa pesa tu jambo la mwanzo kama tulivyoaanza huko matengenezo na vile vile kurekebisha na kupanua baadhi ya sehemu basi na Pemba tunafanya hivyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nami nilipokuwa nikichangia kulitajwa masuala ya uwekaji wa taa barabarani, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwamba na Pemba katika mgao huu utapatikana lakini walifikiria pale Chake Chake tu sasa hivi ..

Mhe. Mwenyekiti: Taa zipi hizo.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Walifika Chake Chake lakini sasa hivi watu wa Wilaya ya Micheweni Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu ya Konde ambayo tumeangalia watu wote.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unazungumzia taa zipi taa za kuongezea magari *Okay*.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Hasa pale Konde hebu naomba muongozo wa Mhe. Naibu Waziri vipi anapafikiriaje kwamba watu wote ndio tunakutana pale Konde sikukuu kama zinatokezea ajali nyingi kuna barabara inoelekea Wete inaokwenda Makangale inayokuja Chake Chake na nyengine hebu naomba muongozo kidogo nini atanambia kuhusiana na hizi taa kwenye barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti Pemba tumeweka sehemu mbili kama ulivyosema Chake Chake pale na pale maeneo ya Mtemani. Kwa hiyo kwa hivi sasa tuwachie maeneo hayo na baadaye tumechukuwa ushauri wake hali ya bajeti itakaporuhusu mwakani tunafanya hiyo kazi. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Haya *Inshaallah* tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu PP0104 Programu Kuu ya Undeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Jumla ya Programu Kuu	3,844,520,000
Jumla Kuu ya Fungu P01	**216,820,202,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, nakushukuru sana nalishukuru Baraza lako Tukufu na ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya fedha ya wizara yetu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio haya. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana hoja ya Mheshimiwa wanyanyue mikono wanaokataa, walikubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuruni sana sana kwa mashirikiano mliyoonesha tokea mlipoanza kuchangia hii bajeti lakini pia nikupongezeni kwa kuweza kuipitisha bila ya mabadiliko yoyote. *(Makofi)*

Lakini pia nitowe nafasi hii kuwashukuru wale waliotoa hoja nzito sana ambazo zitasaidia katika kurekebisha mienendo ya matumizi kwenye wizara, lakini pia miongozo yetu itasaidia watendaji katika kusimamia shughuli ambazo umepangiwa.

Mimi niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ushirikiano ambao wameutoa na baada ya hapo kwa kuwa muda bado upo labda nimsikilize Katibu atowe taarifa.

Ahsante waheshimiwa naomba basi nichukuwe nafasi hii kuahirisha shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 8:34 mchana Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 02/06/2017 saa 3:00 asubuhi)